

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Saba – Tarehe 9 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulla Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 55

Kuwajengea Uwezo Wanawake na Vijana Nchini

MHE. CATHERINE N. RUGE aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na jitihada zinazofanywa na Taasisi zisizo za Serikali katika kuwashamasisha na kuwajengea uwezo wanawake na vijana kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika chaguzi nchini:-

(a) Je ni nini mkakati wa Serikali kulifanya kundi hili kushiriki na kupata nafasi za kugombea katika chaguzi zijazo?

(b) Sera ya vijana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki inahitaji uwepo wa Mabaraza ya vijana kwa nchi wanachama: Je, ni lini Baraza hili litaanzishwa?

WAZIRI MKUU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa vijana wanahamasishwa na kujengewa uwezo wa kuwania nafasi za uongozi katika chaguzi zijazo, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Inaratibu programu ya ujasiri na Stadi za maisha kwa vijana, ambapo kupitia programu hizi, vijana wanapatiwa mafunzo yanayolenga kuwaandaa kuwa na uthubutu, kijiwekea malengo na kufanya maamuzi sahihi kuhusu maisha yao ikiwa ni pamoja kushiriki katika masuala ya uongozi kwenye ngazi mbalimbali.

(ii) Kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru, vijana wamekuwa wakihamasishwa kushiriki katika nafasi za uongozi, mathalani, katika kipindi cha mwaka 2016 - 2019 jumla ya vijana wakimbiza Mwenge wa Uhuru 30 waliofanya kazi hiyo kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu wameweza kupata nafasi za uongozi za kisiasa na za kiutendaji katika ngazi mbalimbali.

(iii) Kuendesha mafunzo ya Stadi za Uongozi (*Leadership skills*) kupitia Vituo vya Maendeleo ya Vijana ambapo jumla ya vijana 3,190 kutoka sehemu mbalimbali nchini wamepatiwa mafunzo kati ya mwaka 2016 – 2019. Lengo la mafunzo haya ni kuwaandaa vijana kuwa viongozi bora wa baadaye katika jamii.

(iv) Kupitia Makongamano, Matamasha, Wiki ya Vijana Kitaifa, Siku ya Vijana Kimataifa pamoja na majukwaa mbalimbali, vijana wamekuwa wakihamasishwa kujadili

masuala yanayohusu ustawi wao ikiwemo siasa na kushiriki katika chaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa zimekwishaanza. Aidha, Kanuni za utekelezaji wa Sheria hii zimekwishaandaliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 348 la tarehe 15 Septemba, 2017. Kwa sasa Serikali inafanya maandalizi ya uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa kwa kutoa elimu kwa vijana na jamii nzima kuhusu sheria inayounda Baraza, majukumu ya Baraza, Uanachama, Muundo wa Baraza, uongozi, masuala ya kifedha na majukumu ya Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa Baraza katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Baada ya kazi hii kukamilika, Baraza litaundwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni nilizozitaja hapo awali.

Na. 56

Kuupandisha Hadhi Mji Mdogo wa Mbalizi

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na kasi ya ukuaji wa Mji Mdogo wa Mbalizi zikiwemo shughuli mbalimbali za biashara, uchumi wa viwanda na pia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, imesababisha kuwa na umuhimu mkubwa wa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Mbalizi:-

Je, ni lini Serikali itaupandisha hadhi Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi?

Je, ni lini Serikali itarekebisha mipaka ya Vijiji vya Kata ya Utengule Usongwe ikiwemo Kijiji cha Mbalizi ambacho hakiungani kabisa na vijiji vingine kwa kutenganishwa na Kata ya Nsalala?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijiini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha kuendeleza maeneo ya utawala yaliyopo kwa miundombinu ya Ofisi, nyumba za watumishi, usafiri na usafirishaji na huduma za elimu na afya ili wananchi waanzze kupata huduma kabla ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Hivyo, maeneo mengine ya utawala yataanzishwa baada ya kukamilisha zoezi la uendelezaji wa maeneo yaliyopo ambayo yanaendelea kujengwa.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya swalii la msingi, Kijiji cha Mbalizi ambacho ni Kitongoji cha Mbalizi hakiungani na Vijiji/Vitongoji vingine vya Kata ya Utengule, Usongwe: Je, Serikali itarekebisha mipaka ya Kata hii ili Kitongoji cha Mbalizi chenye wakazi zaidi ya 60,000 kijitegemee?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kutokana na ukubwa wa Mji wa Mbalizi na idadi kubwa ya wakazi; na kwa vile kuna miundombinu ya kutosha: Je, Serikali inaweza kuangalia na kutoa kipaumbele cha kuwepo kwa Halmashauri au hata Manispaa ya Mbalizi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji mdogo Mbalizi, ina Kata mbili za Utengule Usongwe na Nsalala ambapo vijiji vyote vilivyokuwa sehemu ya Mji wa Mbalizi vilipoteza hadhi ya Vijiji na kuwa Vitongoji hivyo kwa sasa katika Kata hizo hakuna Vijiji, bali kuna Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swalii la msingi kuwa mpango wa Serikali ni kuimarisha kwanza maeneo ya utawala yaliyopo kwa kujenga miundombinu yote inayotakiwa na kuyapatia vitende kazi na watumishi ili kuboresha huduma kabla ya kuanzisha maeneo mapya. Ni wazi kuwa Serikali itakapoanza kuititia upya maeneo ya

utawala, maeneo yote yaliyokidhi vigezo yatapewa hadhi inayostahili.

Na. 57

**Kujenga "Gabions" Katika Mto Ujulikanao
kama Shaban Robert**

MHE. GEOGRE M. LUBELEJE aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Mpwapwa upo mto ujulikanao kwa jina la Shaaban Robert ambao unaanza Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa hadi Kijiji cha Ilolo. Mto huo umekuwa na korongo kubwa ambalo likijaa maji ya mvua laweza kusababisha madhara makubwa, lakini hata hivyo limesababisha madhara makubwa kwa majengo kama vile *Central Hapeq* na majengo ya Kanisa la Anglikana, Kanisa Katoliki na majengo ya Mtaa wa Hazina Mjini Mpapwa nayo yapo hatarini kubomoka.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga "Gabions" la kuzuia korongo hilo kuendelea kuchimbika na kuleta madhara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Geogre Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mpwapwa una mto ujulikanao kwa jina la Shaaban Robert unaanza Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa hadi Kijiji cha Ilolo. Mto huu hadi miaka ya 1990 ulikuwa unatiririsha maji mwaka mzima, lakini baada ya miaka ya 1990 umesalia kuwa ni wa msimu kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira hususan katika milima ya Kiboriani na shughuli za kibinadamu kando ya kingo za mto huo na kusababisha kukua kwa korongo ambalo

linakadiriwa kuwa na urefu wa takriban kilometra 11 na upana wa kat i ya mita 50 hadi 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali kuitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau wengine mwaka 2006 iliandaa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyano vya Maji. Lengo la mkakati huu lilikuwa kutatua changamoto za mazingira ikiwemo kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyano vya maji. Mkakati huu umefanyiwa mapitio kwa lengo la kuboresha ufanisi katika hifadhi ya ardhi na vyano vya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kukabiliana na kuongezeka kukua kwa korongo hili, Serikali kuitia Wizara ya Maji chini ya Bonde la Wami – Ruvu imemwajiri Mtaalamu Mshauri "*Geonetwok Consulting Limited*" kuandaa mpango wa kuhifadhi vyano vya maji nchini "*Catchments Conservation Plan*" ambao suala la utatuzi wa korongo la Mto Shaaban Robert limejumuishwa.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa mazingira ya kingo za mito yanalindwa kwa kuendelea kutekeleza mikakati ya kuhifadhi ardhi pamoja na kuhamasisha sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutekeleza mikakati inayolenga kuongoa maeneo yaliyoharibika sana.

Na. 58

Kukamilika kwa Barabara ya Kilwa

MHE. ISSA A. MANGUNGU aliuliza:-

(a) Je, Barabara ya Kilwa imeshakabidhiwa kwa Serikali kutoka kwa Mkandarasi aliyejenga barabara hiyo (KAJIMA)?

(b) Je, barabara hiyo iko katika kiwango kinachotakiwa?

(c) Je, ni nani anagharamia ukarabati usiokwisha wa barabara hiyo kati ya Serikali na Mkandarasi?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa barabara ya Kilwa (Sehemu ya Bendera Tatu hadi Mbagala (Zakheim) chini ya ufadhili wa JICA ulikamilika na kukabidhiwa Serikalini mwezi Desemba, 2015 baada ya Mkandarasi (KAJIMA) kurudia kazi ya matengenezo kwa gharama zake mwenyewe sehemu ya kuanzia Bendera Tatu hadi Mtoni Mtongani iliyokuwa imekarabatiwa chini ya kiwango na Serikali kukataa kuipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa sehemu ya barabara kutoka Bendera Tatu hadi Mbagala katika Barabara ya Kilwa ipo kwenye mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Hivyo, hakuna kazi za ukarabati zinazoendelea katika barabara hiyo nje ya kazi za ujenzi. Mradi huu wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2022.

Na. 59

Hitaji la Kiwanja cha Ndege – Busokelo

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Busokelo ina vivutio vingi vya Utalii kama Mlima Rungwe, Hifadhi ya Kitulo, maziwa ambayo hayatoi maji kama Ikapu, Iramba – Kyungululu na upatikanaji wa maji joto ardhi na gesi asilia ya *carbondioxide*.

Je, ni lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege (*Air-Strip*) ili kurahisisha huduma hizo na watalii kuweza kufika kwa urahisi?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
ali jibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo kuhusu hitaji la Kiwanja Ndege, Busokelo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya ndege vidogo (*Airstrips*) katika maeneo ya kitalii hujengwa na kuendeshwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Taasisi zake zenye uUtaalam katika nyanja ya usafiri wa anga ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam kuhusiana na ujenzi wa viwanja vidogo vya ndege katika maeneo ya kitalii pale utakapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*) hivi sasa inafanya maboresho makubwa kwenye Kiwanja cha Ndege cha Songwe kilichopo Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kukamilika kwa maboresho ya Kiwanja cha Ndege cha Songwe sambamba na mradi wa ujenzi wa barabara ya Katumba – Busokelo – Mbambo – Tukuyu kwa kiwango cha lami, kutarahisisha usafiri katika kuyafikia maeneo yenye vivutio vya kitalii aliyoyaainisha Mheshimiwa Mbunge. Tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake za kuboresha uchumi kwa wananchi wa jimbo lake liliopo katika Halmashauri ya Busokelo kupitia vivutio vya kitalii alivyoviaainisha.

Na. 60

Chanjo ya Ugonjwa wa Hepatitis B

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Hepatitis B* ni ugonjwa hatari ikiwa utampata mtu asiye na chanjo ya ugonjwa huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa chanjo ya *Hepatitis B* kwa Watanzania ambao hawajapata chanjo?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa chanjo ya *Hepatitis B* kwa watoto wote kuititia chanjo ya *Pentavalent* yenye mchanganyiko wa chanjo za Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini na Homa ya Uti wa Mgongo (*DPT-HepB-Hib*) kuanzia mwaka 2002 na hivyo kuhakikisha kuwa wananchi wote waliopata chanjo hiyo wakiwa wachanga wamekingwa. Kwa wananchi wengine ambao wamezaliwa kabla ya mwaka 2002 na hivyo kutokupata chanjo hii, Serikali imekwishaainisha makundi maalum ambayo yatapatiwa chanjo ya HepB kwa kuchangia gharama. Makundi hayo ni:-

(a) Watu ambao kazi zao zinawaweka katika hatari zaidi ya maambukizi ni Watumishi wa Afya wanaohudumia wagonjwa, wanaofanya upimaji katika Maabara, wanaohudumia kwenye vyumba vya maiti "*mortuary*", wanaotoa huduma za uzazi na upasuaji, wanafunzi wanaofanya mazoezi ya vitendo kwenye hospitali wakiwa mafunzioni na wafanyakazi wengine ambao huwa karibu na damu au majimaji kutoka mwilini mwa binadamu kutokana na shughuli wanazofanya:-

(b) Wanaochangia damu;

(c) Watumiaji Sindano wa madawa ya kulevyia;

(d) Wale wanaoshi karibu na wagonjwa au wanaowauguza wagonjwa wa Homa ya Ini;

(e) Wafungwa na watu wenye wapenzi wengi;

(f) Watu ambao hali yao ya ugonjwa inawaweke katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya Homa ya Ini mfano walio kwenye "*haemodialysis*" au walio na maambukizi ya VVU au magonjwa ya TB, kisukari; na

(g) Wasafiri wanaokwenda kwenye maeneo yaliyo na kiwango kikubwa cha maambukizi ya *Hepatitis B* (kwa matakwa ya nchi husika na kwa maombi ya mchanjawaji) na madereva na uthingo wa safari ndefu (*Long distance truck drivers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusitiza kuwa siyo wananchi wote wanapaswa kupata chanjo hii, ila tu wale walio katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya homa ya ini ndio watakaopatiwa chanjo kwa utaratibu wa kuchangia gharama. Utaratibu huu utafanyika kwa awamu, kwa kuanzia kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa na baadaye kwenye Hospitali za Halmashauri ili wananchi wenye uhitaji, ambao wapo katika makundi yaliyoainishwa, wataweza kupatiwa chanjo kwa kuchangia gharama kwa kiwango kitakachowekwa na Serikali.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi nchini Tanzania waliozaliwa kabla ya 2002 hawajachanja chanjo ya *Hepatitis B*.

(a) Je, Serikali ni kwa nini isitoe chanjo ya Hepatitis B bure kama ilivyo kwa magonjwa ya Kifua Kikuu (*TB*) na kama ilivyo kwenye dawa za Ukimwi ambazo zinatolewa bure?

(b) Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya ina mkakati gani wa kutoa elimu ya ugonjwa wa *Hepatitis B* ili wananchi waweze kuelewa unasababishwa na nini na jinsi gani wanaweza kujikinga na ugonjwa huo?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE

NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, Chanjo ya Homa ya Ini bado inaendelea kutolewa bila malipo kwa watoto wote walio chini ya umri wa mwaka mmoja nchini ambapo chanjo hii ipo katika mchanganyiko wa pentavalenti. Kwa watu wazima ambao wapo katika hatari zaidi ya kuambukizwa, chanjo hii hutolewa kwa malipo ya shilingi 10,000/= kwa chanjo kwa jumla ya dozi tatu.

Mheshimiwa Spika, pili, kikosi kazi kimeundwa kwa ajili ya kutoa elimu ya Ugonjwa wa Homa ya Ini kwa wananchi na uelimishaji unaendelea kufanyika kuhusu kujikinga na ugonjwa wa Homa ya Ini ikiwa ni pamoja na magonjwa ya UKIMWI na Kifua Kikuu katika maeneo ya kutolea huduma katika Mikoa, Halmashauri na Hospitali; na mafunzo ya afya kazini ya kujikinga (*Infection Prevention and Control Trainings*) kwa Watumishi wa Umma.

Na. 61

Kusambaza Maji Katika Vijiji Vilivyo Karibu na Mto Ruaha

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kalenga linazungukwa na vyanzo vingi vya maji ukiwemo Mto Ruaha, lakini bado kuna vijiji kama Udumuka, Igunda, Ng'ezza, Itwaga, Ihemi, Ilandutwa, Mibikimitali, Nyabula, Ikuvilo, Kanning'ombe na Makota vina shida kubwa ya maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka maji katika vijiji hivyo?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Igunda na Makota vinapata maji kutoka kwenye chemichemi za Nyanyamba na Makota. Vijiji vya Ikuvilo na Kanning'ombe vinapata maji kutoka kwenye vijito vya Lugala na Wenga na Vijiji vya Ihemi na Mibikimitali vinapata huduma ya maji kutoka visima vitano vilivyopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vijiji vitano vilivyobaki kwa sasa vinapata huduma ya maji kutoka katika vyanzo vya asili vilivyoboreshwa. Vijiji hivyo ni Nyabula, Ng'enza, Ilandutwa, Uдумka na Itwaga. Hata hivyo, katika jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi wa vijiji hivyo wanapata huduma ya uhakika ya majisafi na salama, Wizara kupitia *RUWASA* imepanga kujenga mradi wa maji katika Vijiji vya Nyabula na Ng'enza kutoka vyanzo vya vijito vya Mtangukana Singila-Ibofwe vinavyopeleka maji yake katika Mto Ruaha. Mradi huo utatekelezwa kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo (*Program for Results - PforR*) inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara kupitia *RUWASA* imepanga kuchimba visima virefu vitatu ambavyo vitahudumia vijiji vya Ilandutwa, Uдумka na Itwaga. Uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu utafanywa kupitia Programu ya *Payment by Results (PBR)*. Usanifu wa kina wa miradi hiyo utafanywa katika mwaka huu wa fedha na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha ujao wa 2020/2021.

Na. 62

Kuwasaidia Wavuvi wa Bahari na Maziwa Nchini

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya maisha ya wavuvi nchini katika Bahari na Maziwa ni mbaya; na Serikali kwa mara kadhaa imekuwa ikiahidi kuandaa mkakati wa kuwasaidia vifaa vya uvuvi wavuvi hao wadogo lakini hakuna utekelezaji:-

Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hizo?

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Uvuvi nchini kwa kutekeleza mikakati yenye lengo la kuendeleza wavuvi nchini ili waweze kupata ajira, lishe, kipato na kuchangia katika pato la Taifa. Miiongoni mwa mikakati hiyo ni kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye injini za kupachika (*out boat engine*), nyuzi za kushonea nyavu (*twines*) na vifungashio ili kupunguza gharama za zana na vyombo nya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kulingana na Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Publication (2007) on Common External Tariff*), injini za uvuvi, malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake vinavyonunuliwa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hupewa pungozo la kodi ama kufutiwa kodi ili kupunguza bei kwa wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba wavuvi wanakuwa na zana bora na za kisasa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ili kuwawezesha wavuvi wote kuwa na zana bora na za kisasa. Katika kutekeleza hilo, Serikali imeandaa mpango wa kutoa ruzuku kwa Vyama nya Ushirika nya Msingi nya Wavuvi ambapo injini za uvuvi hutolewa kwa mfumo wa uchangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ruzuku hiyo, Serikali inachangia asilimia 40 na Chama cha Ushirika cha Wavuvi kitatoa asilimia 60 ya gharama ya injini. Mpaka sasa jumla ya injini 60 zimechukuliwa na vikundi nya wavuvi 34 vimenufaika na uwepo wa injini hizi. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge ahimize wavuvi kote nchini wakiwemo wa Jimbo la Tutambile kujunga katika Vyama nya Ushirika nya Msingi ili waweze kunufaika na fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda nya

kutengeneza boti na zana bora za uvuvi. Kwa mfano viwanda vya kutengeneza boti aina ya ''fibre glass'' vya *Songoro Marine Transport* Mwanza na kiwanda cha *Sam & Anzai Boat Builders* na *Seahorse East African* (Ukanda wa Pwani).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, viwanda vya nyavu kama vile Kiwanda cha *Imara Fishnet Dar es Salaam* na *Fanaka Fishnet* (Mwanza) vimeanzishwa. Viwanda hivi vinawezesha wavuvi nchini kupata vyombo na zana bora za uvuvi.

Na. 63

Hitaji la Gari Kituo cha Polisi - Chwaka

MHE. BHAGWANJI M. MEISURIA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Chwaka hakina gari la Polisi.

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la Polisi katika kituo hicho?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bhagwanji Maganalal Meisuria, Mbunge Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Chwaka kipo katika Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. Mkoa mzima una jumla ya magari 17. Wilaya ya kati pekee ina magari mawili mazima. Jeshi la Polisi limekuwa likigawa magari kwa awamu kwa kadri yanavyopatikana. Hivyo kituo hicho kitapelekewa gari la Polisi mara tu litakapopatikana.

Na. 64

Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Umeme Kibaha

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishafanya uhakiki kwa wananchi wa Kibaha waliopisha ujenzi wa umeme wa msongo wa KV 400.

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Dodoma kupitia Chalinze. Mradi unahusisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Kibaha hadi Zinga Bagamoyo. Mradi huu unalenga kuimarisha mfumo wa kusafirisha umeme nchini ikiwa ni pamoja na kusafirisha umeme kutoka mradi wa umeme wa Megawati 2,115 Mwalimu Nyerere (*JNHPP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa takribani kilometra 600 kutoka Kinyerezi - Chalinze kilometra 100, Chalinze – Rufiji kilometra 160 na Chalinze - Dodoma kilometra 340. Mradi unahusisha pia ujenzi wa kilometra 40 njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Kibaha hadi Zinga (Bagamoyo). Mradi huu utaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya kupooza umeme vya Chalinze na Zinga (Bagamoyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 hadi 2016 kazi ya uthamini wa mali za wananchi kutoka Kisarawe, Kibaha

hadi Chalinze ilifanyika ili waweze kulipwa fidia na kupisha ujenzi wa mradi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 taratibu zote za uandaaji taarifa na majedwali ya fidia zilikamilika. Jumla ya fidia kwa ajili ya maeneo kati ya Kiluvya (Kisarawe) hadi Chalinze ni shilingi bilioni 21.569. Malipo haya yanahusisha wananchi watakaopitiwa na mradi katika Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijiini na Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imekamilisha taarifa ya uhakiki wa wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia ya mali zao. Kinachofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za malipo kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi hao wawe na subira wakati Serikali inakamilisha taratibu za malipo hayo.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:-

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, ninayo orodha hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambaeo wameomba kuchangia. Tuaanza na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ajiandae.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima leo kuwepo katika Bunge lako Tukufu, lakini

nikushukuru na wewe kunipa fursa hii adhimu kabisa kuanza kuwa mchangiaji namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipo mpungeza Jemedari wetu, Rais wetu, Mheshimiwa wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi iliyotukuka na uongozi madhubuti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojuua kwamba leo tunajadili Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kweli ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha mafanikio yote yaliyopatikana kwenye elimu, afya, miundombinu, kila eneo. Kwangu pale Kinondoni ni mnufaika mkubwa sana, nimenufaika kwenye elimu, nimenufaika kwenye miradi mkakati. Hivi ninavyozungumza tuna soko letu la Magomeni linakwenda vizuri lakini tulikuwa na mradi wa soko letu la Tandale, nimuombe Mheshimiwa Waziri nimeangalia kwenye kitabu pale nimeona kuna bilioni nne za soko la Magomeni lakini soko la Tandale siaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojuua Soko la Tandale tayari limeshavunjwa na Manispaa imeshatafuta mkandarasi wameingia mkataba. Kwa hiyo tafsiri yake tusipotenga fedha maana yake tutakuwa na deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kanifanyia mambo makubwa sana, kuna mradi wa nyumba kongwe za Magomeni. Mheshimiwa Rais alikuja pale akawahikikishia wananchi wa Kinondoni kwamba nyumba zile atawajengea na watacaa miaka mitano bure. Hivi ninavyozungumza nyumba zile zinapakwa rangi, mambo yako vizuri, tunaamini kabla ya uchaguzi wananchi wetu watahamia katika yale maghorofa, watanning'inia juu kwa juu kama wenzao Wazanzibar wanavyoning'inia katika majumba alijojenga Mzee Karume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu pale kuna miradi mikubwa mikubwa, mradi ya Mto Ng'ombe, tunajenga kingo tunaendelea vizuri, kwa kweli nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru sana sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya tumeshirikiana na Serikali, kama Mbunge wa Jimbo katika ku-support nimetoa milioni 93 kujenga Kituo cha Afya cha Makumbusho. Ni muombe Mheshimiwa Waziri aje kukifungua kituo kile ili wananchi wetu wanufaikie matunda ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mazuri ni mengi lakini pamoa na mazuri haya kuna mambo lazima tukumbushane tuende na *speed* nzuri zaidi ili kuhakikisha tunaleta mafanikio. Sisi Kinondoni tuna *TARURA* wanajenga barabara vizuri lakini wenzangu wengi wamesema hapa, tunaoomba kiwango kile cha *TARURA* sasa kiongezwe kutoka ile asilimia 30 mpaka kwenda walau asilimia 40 twende kwa awamu ili tutapima mafanikio yanakuwaje, lazima tufanye hivyo itakuwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi pale Dar es Salaam *TARURA* wanatoa huduma za *parking*, wanatoa huduma za *service road* pale watu wanaotumia *service road* lakini mapato yale yanakwenda kwenye Mfuko Mkuu. Kama unavyojua Dar es Salaam miundombinu ni shida na tulitaraji wizara iangalie ikiwezekana zile fedha zibaki mahali pale inapokusanya ili kutatua changamoto zinazopatikana katika eneo kwa sababu wananchi wanaotozwa ni haki yao kuhakikisha lile tozo linearudi kuja kutatua matatizo yanayowakabili pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine kwamba tunashukuru sana Serikali, katika Mradi wa *DMDP* Serikali ilituahidi kwamba tusikope badala yake Serikali italipa ghamama za fidia kwa wananchi wetu. Tunashukuru sana hivi ninavyozungumza Wizara ya Fedha imetoa ushirikiano mkubwa, tunapata fedha nyngi, tulishawahi kupata bilioni tano kwa ajili ya fidia na fedha nyngine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo limetokea ambalo tunalionia liko sawa tuliweke vizuri kwamba bahati mbaya sana viongozi wetu wa *TAMISEMI* tumeambawi kwamba kuna fedha tunadaiwa sasa kama bilioni tatu.

Bahati mbaya sisi Manispaa hatujakaa kwenye vikao, Madiwani hatujapitisha tunaona linaweza kutuletea mgogoro, kwa sababu wizara ndiyo wakubwa tunaomba wizara kwa heshima zote kabisa, kaka yangu wa Ukae mnichukulie jambo hili kwa sababu mkituletea pale kwenye bajeti yetu hatujaweka na linaweza likatuletea mgogoro mkubwa katika taratibu zetu za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sisi Kinondoni tuliingia ushirikiano na Mji wa Ujerumani Birmingham ambao wao waliahidi kutujengea kiwanda cha kuchakata taka na kutengeneza mbolea. Mradi huu tuliingia tangu mwaka 2017 na ulikuwa uishe mwaka 2018. Mradi ni zaidi ya bilioni nne na fedha zimeshatoka zaidi ya bilioni mbili na nusu, katika chelewachelewa tulikuwa tunaiomba Serikali itufanyie *exemption*. Tumekwenda, nenda rudi mpaka muda wa mradi umeisha, tumekwenda Wizara ya Fedha wanatuambia mradi umepitwa na wakati, tumeandika barua TAMISEMI kutaka *wa-renew* mkataba. Birmingham tayari wamesha-*renew* mkataba na wao ndiyo watoaji fedha, lakini sisi hapa nyumbani kizungumkuti. Juzi Mtendaji wetu kaitwa kwenye kamati ya watu 30 inaambiwa baada ya hapo ipelekwe kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu ikitoka hapo tena ndiyo hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkataba utachelewa, tutapoteza fedha hizi, na fedha tunaomba *exemption* kutoka Serikali ili mradi uende, mradi ule utatusaidia kutengeneza mbolea, utatusaidia kupunguza taka katika Jiji la Dar es Salaam, tunaomba kwa kweli mambo haya yaende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuna *case* yetu ya Mto Msimbazi, tuna *case* ya *Msimbazi City*. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amelifanyika kazi vizuri lakini vilevile Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira amelifanya kazi vizuri. Lakini kuna ucheleweshaji bado, katika barua ambayo wameandikiana viongozi, barua inatoka TAMISEMI ya tangu Septemba majibu yanatoka Machi, lakini maelekezo yanasema kwamba mradi umepelekwa *TANROADS* anatafutwa Mkandarasi Mshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha zipo, fedha karibu dola milioni 120 na milioni 20 ni *grant* kutoka Uingereza, tukichelewa zile fedha *grant* zinaishia mwaka 2020 fedha zile zitarudi. Huu mradi una maslahi mapana sana kwetu, mradi utajenga barabara, mradi utoipa fidia kwa watu wetu. Ile dhana ya kwamba watu wa mabondeni ni mzigo kwa mradi huu itapatikana fedha ya kulipa fidia, lakini kubwa zaidi katika mradi huu tutapata hekta 54 ambazo zitatengenezwa kutokana na kulipa fidia na kutengeneza, huu mradi unajilipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri apeleke salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu hii ofisi ni ofisi ya Mheshimiwa Rais. Kwamba yale maghorofa ambayo aliahidi pale Magomeni atayajenga kama Mzee Karume, huu mradi unakuja kujenga yale maghorofa, huu mradi unaondoa *squatter* zote katika jiji letu pale hasa inayopitia Mto Msimbazi, Mto Kibangu na Mto Kenge tunaondoa. Mimi hawa ndiyo wapiga kura wangu na mimi siwezi kujiondoa na hawa, najinasibisha na hawa kwa sababu na mimi ni mtu wa mabondeni. Mtu yejote akija akisema pale mabondeni hapana thamani mimi kwa kweli simkubalii, thamani ipo na watu wameonesha, wanatakiwa watu walipwe fidia watoke. Kama tunaona kuna ucheleweshaji basi tuanze na kipengele cha kulipa fidia, tukifanya hiyo tutakuwa tumeisaidia jamii yetu ya Kinondoni lakini tumeboresha jiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza Dar es Salaam mvua ya shillingi 2,000 tu barabara ile haipitiki, sisi tunaambiwa tumekaa mabondeni lakini je, kile kituo cha Mwendokasi pale nacho kimekaa mabondeni? Je, wale waliosanifu ile barabara ya Jangwani pale kila siku panajaa maji na magari ya kuondoa uchafu nao wamefanya uzembe gani? Kwa hiyo, kama utaona kama ni kosa limefanyika lazima tuje na mabadiliko, na mabadiliko chanya kuwatazama vizuri watu waliopo pale mabondeni. Mwenyezi Mungu bahati huu mradi unakuja kutatua lakini sasa sijapata *speed* tunayokwenda na mradi huu napata kizungumkuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini huu mradi ni mzuri, mzuri sana unaweza kuja kuondoa matatizo ya watu wetu na bila shaka tukifanya hivyo na mimi Mbunge kwa kweli nitarudi pale mwemwele mwemwele, nina hakika kabisa ubunge nitarudi. Kwa sababu jamani tuambizane kweli jengo hili ni masikitiko makubwa, sisi wengine vijana jengo hili tunalipenda, ee bwana, unaona suti zinatupendeza! Nimumbe sana kaka yangu alifanyie kazi hili kwa maslahi ya Chama chetu Cha Mapinduzi, kwa maslahi ya ushindi wa Mheshimiwa Rais wetu na Mbunge wao kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na kwa kweli nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi hatimaye nikapata fursa hii ya kuongea mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua watu wengi kila wanapoanza wanamsifu Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano na wengi wanasema amejenga reli, amejenga umeme, nakadhalika. Ukienda mahali kama Namtumbo ninapotoka wana Namtumbo wanamshukuru Mheshimiwa Rais kwa vitu tofauti kabisa. Yaani hivi ni nyongeza tu ukiongelea reli ni nyongeza tu kwao, ukiongelea ndege ni nyongeza tu kwao, wao jambo la kwanza kubwa ni mawasiliano ya simu. Tulikuwa gizani lakini sasa karibu Namtumbo yote kasoro vijiji tisa tu hadi sasa bado havijawa na mawasiliano, hicho kwao ni kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, wanamsifu kwa sababu amewafungulia masoko ya ufuta, mahindi, masoko ambayo hapo mwanzo walikuwa hawana, lakini isitoshe wanamsifu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli kwa sababu amewajengea VETA katika ngazi ya Wilaya. Wanamsifu kwa sababu amewafungulia barabara ni kwa mara ya kwanza Namtumbo imepata lami kwa miaka yote hii ni kwa sababu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo wanavyosikia kaleta ndege wanafurahi lakini wanapoona kule kajenga hospitali ya wilaya kwao ni kitu kikubwa sana wanakiona na hayo ni kwausaidizi wa hawa mawaziri. Nikushukuru sana Mheshimiwa Jafo na Waziri wa Afya umetuwezesha kupata hospitali ya wilaya, umetuwezesha kupata vituo vya afya, umetuwezesha kujenga zahanati, ni vitu ambavyo vimeleta maendeleo makubwa sana Namtumbo. Tunakushukuru sana na ninaomba umpelekee salaam Mheshimiwa Rais wana Namtumbo wanamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya mwisho kwenye ziara yangu ya mwisho kabla sijaja huku muda wowote wana Namtumbo wanassema tafadhalini wabunge hakikisheni huyo Mheshimiwa Rais haondoki, asiondoke huyo Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri wake ili waendelee kutuletea maendeleo makubwa Namtumbo na Tanzania nzima kwa ujumla. Wanaomba barabara, wanaomba reli, kwa bahati mbaya mmeisema sana kwenye redio imewahamasisha sana wanamtumbo na wanassema asiondoke mpaka ile reli ikamilike hata kama itamchukuwa miaka 30. Kwa sababu ni kwa mara ya kwanza Wanamtumbo wanaona vitu vinasemwa na vinatekeleza, tunawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuomba Mheshimiwa Jafo, tuna barabara inayounganisha Namtumbo kutoka Kijiji cha Mageuzi inapita Mawa, inapita Ruvuma, inapita Mbimbi pale inakatisha inaenda Libango na kutokezea Minazini Namtumbo. Barabara hii itatusaidia sana kuiunganisha Wilaya ya Namtumbo, kwa sasa kuna maeneo kama Kata ya Hanga, ni lazima kwanza waende Songea halafu ndiyo waende Makao Makuu ya Wilaya. Hii barabara ndiyo itakayowasaidia hawatalazimika kwenda Songea wataenda

moja kwa moja Namtumbo katika Makao yao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hii barabara mtusaidie na hii barabara ina madaraja makubwa mawili, moja iko pale Libangwe siku nyingi tumeomba gharama yake ni ndogo tu million mia tisa hamsini. Hebu tupeni fedha hizi *TARURA* wameshafanya hiyo *estimate*, ni hela kidogo hebu tuleteeni hiyo hela tukajenge ile barabara inayounganisha Kijiji cha Libango na milazini lakini vilevile ndiyo itakuwa muunganiko mzuri wa kutoka Mageuzi, Mbimbi, Libango hadi Namtumbo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu, kwa kweli leo sikutaka sana kutumia fursa hii kuomba mengi, kwanza ni kuwashukuruni sana. Najua mahitaji ni makubwa sisi mmetujengea vituo vya afya vipyta viwili, cha Namtumbo na sasa kinajengwa cha Mtakanini. Ningkuomba ungejua mazingira ya Wilaya ya Namtumbo nina uhakika ungetuongezea tena walau vituo viwili, vitatu hasa kile kilichoko mbali cha Mputa ambacho kinachukua Kata ya Mputa na Kata Kitanda, lakini vilevile, Kituo cha Magazini ambacho ndiyo kipo mbali sana na mwisho Kituo cha Mchomorwa kama unakumbuka Mheshimiwa Rais aliposimama pale mwezi wa nne mwaka jana alikuambia unatakiwa utoe milioni mia moja kuchangia ujenzi pale baada ya kudhibitisha kama zile fedha milioni sitini zimetumika sahihi. Ninadhani kama unafahamu kwamba imedhibitishwa zile milioni 60 zimetumika vizuri sasa tupate zile milioni 100 ambayo Mheshimiwa Rais aliyowaahahidi wale wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni *WMA*, kwa kweli ukiniuliza tatizo moja kubwa katika wilaya yako nini? Ni changamoto kati ya wahifadhi na wakulima kwa upande mmoja, wakulima na wafungaji kwa upande wa pili. Sualal a wahifadhi na wakulima linakuhusu sababu hifadhi hizo siyo Hifadhi za Taifa, ni hifadhi za ngazi ya wilaya, ni hifadhi za jamii ziko chini yako. Ndiyo maana wakati nimeuliza swali hapa mwaka huu mwanzoni Naibu Waziri wako ndiyo

aliyelijibu Mheshimiwa Waziri George Waitara na alijibu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana niombe tu mrudie tu kwenye yale majibu mliyoyatoa ili hatimaye utekelezaji ufanyike. Pale wananchi wamesikia, wamefurahi sana kwamba sasa yale maeneo yatapitiwa upya kwa mujibu wa makubaliano ya mwaka 1992 na hatimaye wananchi watapata maeneo ya kilimo na maeneo mengine yatatengwa kwa ajili ya ufugaji ili ugomvi kati ya wafugaji na wakulima uondoke lakini wakati huo huo vurugu zinazoendelea kati ya wahifadhi na wakulima nazo ziondoke. Mtusaidie kutatua changamoto hiyo kubwa inaleta migogoro na migogoro pekee iliyobaki kwa sasa ni hiyo. Nimwombe Mheshimiwa Jafo namwaminia sana kama ambavyo Mheshimiwa Rais anamwamini na wana Namtumbo wanamwamini, alifika kule Namtumbo aliyoyasema yale bado wanayakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie tu lile jengo alilofanya kazi kubwa sana kwenye Namtumbo *Marathon* limekamilika na tunataka kuweka jina lake. Nimwombe sana atakapolikamilisha hilo, tutamwomba aje afungue ajue kwamba katika maisha yake kuna mchango mkubwa ametoa kwa Wanamatumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa kwa asilimia mia moja. Kwa kweli Serikali hii naomba sana isiondoke mpaka mambo haya makubwa yaliyoanzishwa kama reli yakamilike na tunapoongelea kukamilika kwa reli hatuongelei kutoka Dar es Salaam mpaka sijui hapa Dodoma au mpaka Mwanza, tunataka mtandao mzima wa reli ukamilike ndiyo waondoke. Kabla ya kukamilisha hii pamoja na ile ya Mtwara - Namtumbo - Songea hadi Liganga kule mpaka watakapokamilisha hizo ndiyo waondoke, wasiondoke kabla hawajakamilisha hayo hata kama itawachukua miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nanakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi na Mheshimiwa Daniel Edwad Mtuka ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kutokana na tatizo kubwa ambalo limeikumba dunia, pia limeikumba nchi yetu tatizo la ugonjwa wa *corona virus* na kutokana na kauli ambayo ilitoka upande wa Serikali kuititia Waziri Mkuu, juu ya tamko lake la kufunga shule zote za msingi, sekondari pamoja na Vyuo, liliikuwa ni tamko zuri sana. Kutokana na hawa watoto leo kuwepo mitaani napenda kushauri, ni vyema baada ya kufunga hizo shule ni jambo moja, jambo lingine lazima tuangalie hali ya hao watoto huko waliko Serikali imejipangaje, lakini pia hawa watoto kitaaluma wamerudi nyuma, kuna njia gani sasa hivi ambayo Serikali wanaitazama juu ya hawa watoto kuendelea kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa nazungumzia suala hilo hilo la elimu, niende kwenye jambo la msingi kwa upande wa Wizara ya TAMISEMI, ndiyo Wizara ambayo imebeba vitu vingi sana. Natambua wanapokuwepo Mawaziri lengo ni kumshauri Mheshimiwa Rais na kumsaidia kwenye hayo majukumu mengine kwa sababu si kila kitu anaweza kufanya, lakini nimefanya utafiti mdogo tu kwenye Mkoa wangu wa Rukwa kwa sababu kuanzia Serikali ya Awamu ya Kwanza mpaka ya Tano zote ni Serikali zinazotokana na Chama cha Mapinduzi, kuna mambo ambayo inapotoka awamu moja kwenda awamu nyingine mkakati ambao uliibuliwa unaishia njiani. Sasa kama ni Serikali hiyo hiyo kwa nini kunakuwa hakuna mwendelezo? Nazungumzia mfano wa maabara, uliibuliwa na Serikali ya Awamu ya Nne, ukiangalia hakuna mkakati endelevu unaoonekana kwenye Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ni moja....

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Seif Gulamali.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nimsahihishe mchangiaji anayechangia muda hu. Nampa taarifa, inawezekana hajasoma vizuri ama hakusikiliza vizuri taarifa iliyosomwa na Waziri wa TAMISEMI, imewekwa bajeti katika taarifa hii ya Waziri, mpango mkakati wa kukarabati maabara zote nchini zilizojengwa na zingine zitakazojengwa baadaye. Kwa hiyo asiseme kwamba hakuna mkakati, upo na ndiyo maana inawezekana hakuisikia taarifa au hakuwepo, kwa hiyo arudi asome upya ndiyo aje achangie. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, unaipokea taarifa hiyo.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa bahati mbaya zaidi huwa siyo mtu wa mizaha kwenye mambo ya msingi, nazungmzia jambo ambalo ni halisia, kutenga ni jambo moja na kutekeleza ni jambo lingine. Halafu majukumu ya Waziri tumwachie Waziri atajibu kwa wakati wake, Mheshimiwa ana kazi nydingi za kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sizungumzii mambo ambayo ni nadharia, natoka huko. Awamu ya Tano mpaka sasa inakwenda kumaliza muda wake, anapozungumzia leo aliyenipa taarifa anazungumzia mkakati, nasema Serikali ya Awamu ya Kwanza mpaka ya Tano ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hayo mambo yaliibuliwa na Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la maboma wananchi wametumia nguvu zao na muda mwingu sana kujitolea kujenga, shule, kujenga madarasa, *survey* yangu ndogo ambayo nimeifanya Manispaa ya Sumbawanga, kumalizia tu yale maboma ya Manispaa mmoja kwenye Mkoa wangu wa Rukwa inahitaji bilioni 17, ukitaka kufikiria kwamba ni namna gani haya mambo yatakelezwa unarudi

kwenye hali halisi ya makusanyo, kwenye vyanzo vya mapato je, hili jambo linawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tunapokuwa tunafikiri tunahitaji kupongeza tuangalie pia vipaumbele vya Taifa letu. Kama tunakwenda kutazama *slogan* ya Serikali ya viwanda, ni lazima tuandae watoto wetu, tunawaandaaje? Tumezunguzia habari ya elimu bure kwenye Serikali ya Awamu ya Tano, haya limezungumzwa ndiyo utekelezaji wake ukoje? Ni lini kabla ya tamko hili hawa wadau wa elimu walishirikishwa kikamilifu wakawaambia kipaumbele chao ni nini kwenye suala la elimu bure. Ni vizuri kama Serikali, Serikali ni ya Watanzania wote, tutafakari nini ambacho Watanzania wanakihitaji kama kipaumbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka kwenye suala la maboma ambalo linahusu suala la taaluma, Watanzania wana maswali mengi sana, swali lao la kwanza baada ya utaratibu wa vitambulisho vya wajasiriamali mpaka leo hawajui zimepatikana kiasi gani kwenye vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema kuna mkakati gani endelevu kwa sababu lile jambo lilikuwa ni la mwaka mmoja mkakati wa hivi vitambulisho ni upi? Kuna mambo mengine Watanzania wanaweza wakaelewa, lakini baadaye likawa na maswali mengi sana, ukiwaambia nimeanzisha hiki waambie na hitimisho lake likoje, likianzishwa halafu likaishia njiani linaacha maswali mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia jambo la tatu ambalo ni malengo ya Serikali za Mitaa, ilikuwa ni kupeleka maendeleo kwa wananchi. Wasimamizi wa haya maendeleo kule chini ni Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Madiwani hawa wanapaswa kulipwa posho zao kutoka wapi, Wenyeviti hawa asilimia 20 inatakiwa ipatikane kutoka wapi, je, hali za halmashauri zetu zikoje mpaka sasa hivi? Madiwani pamoja na kuwa posho zao ni ndogo na imekuwa kilio cha Wabunge wengi waongezewehizo posho, lakini hata zile hazilipwi kwa wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani kama wanaweza wakakosa hiyo posho ambayo ni ndogo usimamizi wa haya maendeleo tunayoyazungumza inakuwaje? Usimamizi wa hawa Wenyeviti hiyo asilimia 20 na hapa wanapaswa kujua tu baada ya Wenyeviti hawa waliopatikana 2019 wa Chama cha Mapinduzi hali ya kiutendaji huku chini ni mbaya kupita maelezo japokuwa ni wa Chama cha Mapinduzi, yaani kila leo ni kesi ambazo hazieleweki, lakini ndiyo hao waliosema wanajua kusoma na kuandika, walioandika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Jafo, wale Watendaji ambao walifanya kwa makusudi kuvunja sheria kuwazuia watu wasichukue fomu, wengine wakafunga Ofisi mpaka leo na wangapi wamechukua hatua na ni hatua gani? Watanzania wanataka kujua kwa sababu ni haki yao na hawa Wenyeviti wanapaswa kutokana na wananchi wenyewe, siyo Wenyeviti wa kuteuliwa, Wenyeviti wanatakiwa wachaguliwe na wananchi. Kwa hiyo ukiwazuia wananchi haki yao ya msingi ina maana umezuia maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nataka nizungumzie suala moja, hili la *corona virus*, maeneo ya mipakani yanahitaji nguvu ya ziada, ninapozungumzia maeneo ya mipaka nazungumzia ile mikoa nikianza Mkoa wangu wa Rukwa. Mimi ni mzaliwa wa Wilaya ya Nkasi, Wilaya ya Nkasi hospitali ya Wilaya inajenga ndiyo, lakini Kituo cha Afya Nkomolo kwa sasa kinabeba mzigo mkubwa kuliko hadhi yenyeve ya kituo cha afya. Lakini kibaya zaidi kituo hicho ambacho tayari na sisi tuko mpakani mwa Congo na Zambia hicho kituo hakina hata uzio, hicho kituo wagonjwa wanaokwenda kutibiwa na kuondoka wanachangia vyoo na wagonjwa waliolazwa. Hii hali tunawawekaji Watanzania wetu, huku ambako tumewaacha watoto waende nyumbani ndiyo wanakokwenda kutibiwa wanakutana na wagonja, ndiyo huku ambako wanalazwa wanakutana na watu ambao choo ni kimoja wanaokuja kutibiwa na waliolazwa wanatumia choo kimoja...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani kuna taarifa Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi haina Kituo cha Afya kimoja tu mpakani kando ya Ziwa Tanganyika ambako ni DRC ya Congo kuna Kituo kizuri sana cha Afya Kirando, kuna Kituo cha Afya kizuri sana Wampembe ambacho ni sawa na Nkomolo, sawa na cha Kirando. Kwa hiyo hatuna kituo cha afya kimoja tu katika Wilaya ya Nkasi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani unaipokea taarifa hiyo.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia Mheshimiwa Keissy uchaguzi unakaribia, atulia tu *brother* tutakutana huko, asiwe na presha, mimi nazungumza kwenye maadhimisho ya wanawake nilikuwa pale. Kwa hiyo kama ye ye anajipanga namna gani atanikabili kwenye uchaguzi atulie, nazungumza mambo ambayo ni halisia ya Watanzania. Mimi najua kwa sababu kwanza ni mzaliwa wa pale anajua, hicho kituo anachokizungumzia nimekwenda pale na sijasema Wilaya ya Nkasi ina kituo kimoja. Kwa hiyo atulize presha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ilivokuwa mbaya kwenye halmashauri tunajua Wakurugenzi wapo baadhi ambao wanajitahidi kubuni vyanzo vya mapato, lakini katika ubunifu huu wa vyanzo vya mapato kuna vyanzo vingine wanavyobuni vinawaumiza wananchi. Pamoja na kubuni hivyo vyanzo vya mapato ni lazima tuangalie ni namna wanakwenda kutekeleza, kuna sheria nyingine ambazo ni Sheria za Serikali za Mitaa zinakwenda kabisa kuondoa haki za binadamu. Kutokana na vyanzo hivyo ni pamoja na chanzo cha kuwaambia watu watekeleze ile siku ya *Magufuli day*, natambua Watanzania si kwamba wanafanya usafi mara moja kwa mwezi. Hiyo wameanza

kuwajengea watu kwamba ikishafika saa mbili asubuhi anawaza kwamba leo ni *Magufulidaynafanya* nini, ni lazima wawaambie kwamba kufanya usafi kuna faida zake, lakini wamewaambia watu wakusanye taka lakini hawajawapelekea Wakurugenzi magari ya kubebeta taka nini maana ya huo usafi tunaouzungumzia? (*Makofi*)

(Hapa kengele iligonga kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani muda tayari, ahsante sana.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Daniel Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nifungue hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai mpaka sasa hivi tuko na afya njema na tunaendelea na majukumu ya kitaifa. Shukrani zangu pia nizipeleke kwa Chama cha Mapinduzi, chama changu ambacho kilipendekeza jina la Mheshimiwa Rais, mpaka sasa hivi tunaye, anaendelea kupiga majukumu kama ambavyo Watanzania walitarajia. Pia nipongeze timu nzima ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulibeba jahazi hili la Serikali ya Awamu ya Tano, wote tunaona jinsi wanavyofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Jafo, tumemuona anazunguka nchi nzima mikoa yote, kipindi hiki ambacho kimepita amekuwa na bajeti ya triliuni 6.2 pamoja na timu yake na Manaibu Waziri wawili pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu wake wawili, kusimamia triliuni 6.2 siyo jambo la mzaha, wala siyo jambo dogo, kuna Wizara zina triliuni moja zingine hata triliuni moja hajijafika, lakini huyu hana triliuni 6.2 na sasa tunapitisha bajeti ya triliuni 7.01. Nampongeza sana ndugu yangu

Mheshimiwa Jafo abarikiwe sana pamoja na timu yake nzima anatutendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Spika wetu pamoja na Naibu Spika mmeendesha Bunge kwa weledi mkubwa sana. Mimi ni mara yangu ya kwanza lakini kwa kweli sijutii kuwa na ninyi katika Bunge hili. Pia niende moja kwa moja kabla muda haujaniishia nidokoe kitu kidogo kidogo yale ambayo Jimboni kwangu tumetendewa, mimi huwaga naenda na *figure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na elimu kwa ufupit, katika kipindi ambacho mpaka hapa ninapozungumza upande wa elimu tumeepata bilioni mbili, tumeletewa kwa maana ya jumla kwa maana ya shule za msingi pamoja na elimu ya sekondari, kwa mfano tumejengewa vyoo, maboma tumeletewa fedha, vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu, matenki ya kuvuna maji ya mvua, hosteli, Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Wilaya tunayo hapo pale ni mpya, pia maabara tumeletewa pia fedha, kwa maana ya kukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa afya tuna vituo vimeshakamilika, pamoja na kituo ambacho tumeletewa fedha kinaendelea kujengwa, tuna jumla ya bilioni 1.3 kwenye vituo vya afya, lakini kuna zahanati 15 zimekarabatiwa jumla ya milioni 150, tuna milioni 93 tumeletewa, tumekarabati jengo la akinamama la kujifungulia, pia tumemalizia jengo la *x-ray*kwenye Kituo cha Afya cha Kintiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *TARURA*, mwanzoni kabla hatujaingia kwenye uchaguzi tulikuwa na kilometra 400 za barabara upande wa *TARURA* kwa maana ya Mjini pamoja na Vijiini, lakini hivi ninavyozungumza kuna barabara zenyе urefu wa kilometra 1,033.59 katika Jimbo langu la Manyoni, karibu mara tatu ya urefu wa barabara zilizokuwepo na zote zimesajiliwa na zimeshaanza kutengewa fedha, jumla ya makalvati 271 yamejengwa na kukarabatiwa, *drift* nane, pia na madaraja madogo saba yametengenezwa, mimi huwa naenda na *data*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Jimbo tumeletewa pia zaidi ya shilingi milioni 230 ambazo zimeweka chachu kwenye maendeleo kwenye maeneo mengi Jimboni kwangu. Nimalizie tu kwa kusema Awamu ya Tano kwa Watanzania tuiweke katika maandishi na hasa katika miyo yetu, Serikali ya Awamu ya Tano kama ambavyo siwezi kwenda kutaja tena yale yaliyofanyika ni mengi wengine wameyataja, lakini niishie tu kusema kwamba yote haya yanafanikiwa ni kwa sababu ya usimamizi wa kukusanya mapato thabiti na vile vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vimefichika fichika vyote sasa vinasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hiyo tu usimamizi thabiti wa matumizi ya mapato haya, ndiyo maana hata mimi Manyoni huku nasimama najivunia fedha hii imenifikasi, vinginevyo hii fedha isingeweza kufika na nisingeweza kusimama hapa kusema kwa niaba ya watu wa Manyoni kabisa usimamizi ni madhubuti, tumeuona nchi nzima kila mmoja anasimulia usimamizi madhubuti wa matumizi haya. Tuipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kuleta maombi machache sana. Manyoni tunahitaji Hospitali ya Wilaya. Mwaka 1992 Kituo cha Afya cha Manyoni Mjini kilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya lakini hakina sifa. Tumetenga eneo la hekari 28, tunaomba sasa tufanye *extension* ya hospitali ile sasa ilete hadhi ya Hospitali ya Wilaya ya Manyoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaomba angalau Kituo kimoja cha Afya hasa kile cha Makulu ambachcho Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa ahadi mbele ya Mkutano wa hadhara akiwa pale Manyoni mwaka jana. Naomba sana fedha ile iende kituo kile kijengwe, ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais mama yetu mpendwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado tunahitaji vyumba vya madarasa, mashimo ya vyoo na barabara maeneo ya vijijini. Kwa mfano, tuna barabara moja ambayo nimekuwa

nikiiomba muda mrefu sana ambayo inaunganisha Kata saba za Bonde la Ufa, inaitwa Yasulungai yenyeye urefu wa kilomita 76. Mara nyingi sana nimeshaiulizia hapa Bungeni, naomba basi ujenzi wa barabara hiyo ukamilike ili wananchi hawa wafanye shughuli za maendeleo katika lile Bonde la Ufa maana mimi nina Bonde la Ufa na nina eneo la mlimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema yote hayo mengi na kama ni machache ni machache, niombe tu kuunga mkono hoja hizi shilingi triliioni saba zipite ziende kufanya kazi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omar Massare, Mheshimiwa Justin Joseph Monko ajiandae.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kusema kweli Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi ambazo kila mtu anaziona, hakuna cha kusema hazioni. Labda mtu akiona chekundu atasema cheusi kwa kutaka yeeye mwenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wilaya zetu za Nkasi, mfano Wilaya ya Nkasi tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, vituo vya afya tumepata vitatu ambavyo vimekarabatiwa ni kama hospitali za wilaya. Namanyere pale mjini tuna Hospitali ya *Mission (DDH)* ni hospitali nzuri sana, haina msongamano na kila kitu kipoa hakuna unachoweza kukosa. Kuna chuo pale kinatoa Manesi na Diploma za Maabara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa Mheshimiwa anasimama hapa anasema Namanyere hakuna huduma za afya, wananchi watamshangaa. Hata kama wamebaki CHADEMA 100 au 200 hawawezi kumpa kura wanajua kazi inayofanywa katika Wilaya ya Nkasi. Kama mimi napita kwenye CCM naapa mbele ya Bunge lako Tukufu sitapita

kufanya kampeni, nitalala usingizi, watanipa kura atashangaa na hao CHADEMA waliobaki watatu au wanne kura hawezi kupata wanajua ninavyofanya kazikatika Wilaya ya Nkasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya yetu haina tatizo la huduma za afya. Kwa sasa Serikali imeimarisha, Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe ameshafika mpaka Wampembe ambako ndiko nilikozaliwa mimi, ni mwisho wa nchi anafahamu, kituo cha afya kimejengwa kama hospitali ya Wilaya. Kirando kimejengwa ambaipo ndipo wageni wanaingilia siyo Namanyere. Jiografia ya Wilaya ya Nkasi wageni hawaingilia Namanyere wanaingilia Kirando, Wampembe na Kabwe. Namanyere ipo mbali na mpaka kama kilomita mia sehemu nydingine kilomita tisini, hao huwa wanapita wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakifika Namanyere kuna hospitali mbili, Hospitali ya *Mission* ni kubwa sana, watu wanaifahamu ina sifa kubwa sana. Katika Mkoa wa Rukwa hakuna tatizo labda Sumbawanga. Sasa kwa nini tunasema uongo mbele ya wananchi, tuseme ukweli jinsi Serikali inavyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Rais Magufuli hawezi kufanya kampeni. Juzi shahidi mjomba, huyu hapa mjomba, wa Tunduma aseme ukweli, napigwa simu na watu kutoka Lubumbashi wanasesma tunamuomba Rais Magufuli aje Congo atawale hata mwezi mmoja. Mjomba Mwakajoka anasikia, Lwakatare anasikia wanalia tunamuomba Rais wenu aje DRC Congo hata kwa mwezi mmoja tuna shida tumwambie aje Congo. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakajoka alikuwepo aseme. Kama atakataa hapa lakini aseme mashahidi wapo na wa CCM walikuwepo akina Mheshimiwa Kitandula. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, naomba ukae kidogo...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ngoja kwanza niweke vizuri jambo moja nitakupa fursa, si unataka kutoa taarifa nitakupa fursa kaa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, subiri kidogo.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, akikataa nina mashahidi.

NAIBU SPIKA: Subiri Mheshimiwa Keissy. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena tunapochangia humu ndani kutaja aidha viongozi ama nchi nyiningine ni kwa upande tu wa mambo mazuri ya hizo nchi nyiningine. Kama kuna jambo lolote ambalo haliendi sawa kwenye nchi nyiningine humu ndani haliwezi kutajwa kwa sababu hii nyumba itaonekana kama nchi fulani inajadiliwa. Unaweza kuitaja kwa mfano mzuri ambaa unatamani nchi iangalie huko lakini si kwa jambo ambalo pengine litaonekana haliendi vizuri huko. Kwa namna hiyo Mheshimiwa Keissy hayo maombi ya mtu mmoja kutoka Congo nayaondoa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwakajoka, sasa unaweza kutoa taarifa yako.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na ambacho nilikuwa nataka kumuambia ni hicho ambacho umekiondoa lakini pia aelewe kwamba Mheshimiwa Aida Khenan ni mama yake kwa hiyo asije akamlaani akatema mate halafu ikawa shida tena. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy unakumbushwa kutambua umama wa mama yako aliyeo humu ndani. Mheshimiwa Keissy unapokea taarifa hiyo. (*Kicheko*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, mama yangu mimi ni wa kabile la Kinyamwanga ye ye siyo Mnyamwanga bwana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kidogo na sasa nizungumzie kuhusu *TARURA*. Mimi *TARURA* sisemi habari ya *TANROADS* kupunguziwa pesa maana hata wao vilevile barabara zao zimeharibika, mvua hazikunyesha upande wa *TARURA* tu ni barabara zote. Nashauri tutafute tu hela sehemu zingine ziongezewe upande wa *TARURA* lakini kupunguza pesa kutoka *TANROADS* itakuwa matatizo. *TARURA* itafutwe pesa sehemu nyininge iongezewe lakini kupunguza kwa asilimia tutapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma habari ya hii *EPforR* wamegawa kila Halmashauri pesa sawa wakati kuna Halmashauri zingine zina kata 4, 6 na nyininge zina kata 28. Nimezungumza hapa halmashauri zingine zimegawiwa kisiasa. Hatuwezi kugawa kila Halmashauri milioni mia nne wakati wengine wana kata 6 wenzao kata 28, hii haiwezi kuwa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile habari ya maboma ya maabara wamegawiwa nane nane kwa kila halmashauri. Kuna halmashauri zingine zipo humu mzee ukizungumza ni aibu zina kata 6 au 8. Haiwezekani Mheshimiwa Jafo ni lazima hili mpitie upya. Mgao wa maboma maabara, vituo vy aya, zanahati msigawe sawa kila halmashauri haiwezekani. Kuna halmashauri hapa wana kata 6 uongo kweli?

WABUNGE FULANI: Kweli!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Kuna halmashauri kata 8, uongo kweli?

WABUNGE FULANI: Kweli!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini wapate vituo vya afya vitatu, maabara nane, haiwezekani. Mheshimiwa Jafo hii haiwezekani, hatuendi hivyo lazima tufuate idadi ya kata ndiyo tutakwenda sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimechunguza wengi wanaogopa kusema lakini msema kweli mpenzi wa Mungu, hatuwezi kwenda hivyo. Kuna Wabunge hapa walipewa Majimbo kisiasa leo wanataka kupewa tena mgao kisiasa? Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jafo na Katibu Mkuu Nyamuhanga namuamini sana pitieni suala hili upya. Kwangu kuna maboma kule ya Zahanati za Itindi, Tambaruka, Masheke, Matala yamepigwa batи hatujamaliza mpaka leo. Nilimkumbusha Mheshimiwa Kabwe anaifahamu na Mheshimiwa Nyamuhanga anaifahamu Kabwe vilivyo inatakiwa Kituo cha Afya kijengwe Kabwe haraka iwezekanavyo, kuna muingilliano sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kabwe peke yake na Korongwe ni sawa na Majimbo mengine yaliyomo humu ndani. Idadi ya watu na umbali kutoka Wilaya ya Nkasi inatakiwa na yenyewe ipewe kituo cha afya. Kuna bandari kubwa, wageni kila siku wanaingia kutoka Congo, Burundi, Zambia, ndiyo hiyo mji amba o uko mpakani. Kwa hiyo, naomba Kituo cha Afya kijengwe pale. Kuna kituo cha afya kidogo hakitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna halmashauri ndogo ndogo nikizitaja hapa mzee ni hatari.

WABUNGE FULANI: Taja!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, wanazjua, Mheshimiwa Jafo anazjua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niongelee ujenzi wa ofisi za Tarafa. Tuna Tarafa ya Namanyere ina miaka Makao Makuu ya Wilaya haina ofisi ya Tarafa. Vilevile Tarafa Kate ambayo ni ya siku nydingi lakini haina ofisi ya Tarafa. Sasa tunaomba Makatibu Tarafa wawe na ofisi zao. Nimeona wengine wanajengewa kwenye halmashauri ambazo zina kata 5 au 6, hajji kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nilizungumza hapa tumejazana Wabunge humu, Tume ya Uchaguzi ipitie upya ugawaji wa Majimbo. Kuna Majimbo yana kata 28 mpaka 30 mengine yana kata 6 au 8. Kuna halmashauri zingine zina kata 5 au 6. Jana kazungumza Mbunge hapa kwa povu kuhusu Madiwani wanadai shilingi milioni 540.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa anakuja kuzungumza humu kudai pesa wakati marupurupu ya makusanyo ya halmashauri kule Jimboni kwake, Mkoani kwake ndio wapewe Madiwani wake, siyo Mheshimiwa Jafo atoe hela za Serikali Kuu. Madiwani wanapewa posho ya vikao kutokana na makusanyo ya Halmashauri. Haifai kuja hapa kumbana Mheshimiwa Jafo apeleke pesa. Tulizungumza hapa Halmashauri kama haina uwezo wa kukusanya fedha asilimia 80 ifutwe. Kwa hiyo, halmashauri yako kama inadaiwa na Madiwani, haina uwezo hiyo siyo halmashauri.

MBUNGE FULANI: Futa tu.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Futilia mbali (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kubembelezana hapa ndivyo sheria inavyosema hapa. Kama Mkurugenzi halmashauri yake haikusanyi aitwe ajieleze hafai. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, muda wako umekwisha, ahsante sana.

WABUNGE FULANI: Bado kidogo.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, bado kidogo nimalizie sehemu moja. Kwa hiyo, mimi nazungumza ukweli.

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha. Mheshimiwa Jafo ameshakuelewa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani sana, naunga mkono hoja asilimia 100 kwa 100 na halmashauri zisizokuwa na uwezo futilia mbali na tugawe upya majimbo. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jafo ni kweli hilo jambo la kugawa sawasawa kuna majimbo mengine kata ni nyingi sana. Kuna jimbo linaweza kuwa na kata 36 halafu linapewa shilingi milioni 140 kwenye maboma ambayo yanawezekana yapo kwenye kata zote 36. Wakati huo huo kuna jimbo lina kata 10, sasa ule ufanisi wake utakuwa haulingani kwa sababu wale wa kata 36 watakuwa wamepunjwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nadhani ni vizuri kuliangalia kwa namna ninyi mliviyoweka hiyo bajeti. Inawezekana ikawa fedha ni hizohizo lakini mzigawanye kwa pengine kuangalia uhitaji na mahitaji ya watu kwenye maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Justin Joseph Monko, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara yetu muhimu kabisa ya TAMISEMI ambayo ndiyo imebeba sehemu kubwa ya wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda sana kuipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita na utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameshasemwa na Waheshimiwa Wabunge na yote yaliyozungumzwa ni mambo yanayoonekana na hata katika Jimbo langu la Singida Kaskazini tumepeata miradi mingi ya maendeleo ikiwa ni zaidi ya shillingi billioni 1.3 kwa upande wa sekta ya elimu, katika ujenzi wa miundombinu ya elimu. Katika upande wa afya vilevile tumepeata zaidi ya shillingi bilioni 2.6 katika huu mwaka wa fedha ambao ndio unaishia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Justin Monko, samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa CCM watakuwa wanachangia kwa dakika saba, Wabunge wa CUF na CHADEMA wanaendelea kuchangia dakika kumi.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kama nilivyosema naipongeza sana Serikali kwa utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi na bajeti iliyopita. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake na Mheshimiwa Jafo kwa kusimamia vizuri miradi mingi maana miradi mingi inayowagusa wananchi ipo katika Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo ombi kwa Serikali, Jimbo la Singida Kaskazini bado tunazo changamoto nydingi. Inawezekana hatukupata fedha ya kutosha katika maeneo mbalimbali. Jimbo lile lina wananchi takribani 250,000 mpaka

sasa pamoja na kupata vituo vya afya viwili ambapo tumekarabati Kituo cha Afya cha Mgori pamoja na Msange na kile cha Irlongelo ambacho tumekuwa nacho maana yake ni kwamba tuna vituo vitatu kwa wananchi 250,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona uwiano ule wa angalau kituo kimoja kuhudumia wananchi 50,000 tunahitaji wituo angalau 6. Kwa muda mrefu nimekuwa nikiomba hapa kumalizia tu angalau yale majengo. Najua inawezekana hakuna fedha za kutosha kuwa na majengo mengi kama tulivyofanya kwa vituo ambavyo tumeshapata lakini kipo Kituo cha Ngimu ambacho wananchi wamekijenga zaidi ya miaka kumi iliyopita na Kituo cha Makulo ambavyo tunahitaji fedha za kuvikamilisha.

Mheshimiwa Jafo tumezungumza sana na wewe, nimerudi kwako mara nydingi naomba sana mtupe fedha angalau ya kukamilisha hayo majengo ambayo yameshajengwa na wananchi ili tuweze kutoa huduma kwa wananchi wetu kwa sababu huduma za afya zinahitajika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya afya, naishukuru pia Serikali tumepata hospitali yetu ya wilaya. Pamoja na kuwa na hivyo vituo vya afya sisi tumekamilisha majengo muda mrefu lakini hatujapata kifaa hata kimoja. Sasa nikuombe sana Mheshimiwa Jafo katika hili najua tulishapeleka fedha *MSD* kwa mfano Kituo cha Msange sisi wenye ndiyo tuliopeleka kwa sababu fedha mlituletea tunahitaji hivyo vifaa ili vituo hivi pamoja na hospitali ya wilaya vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitatufaa kuwa na majengo tu peke yake ambayo hayana kazi na kwa muda mrefu tumeshamaliza na hapa tunasema tumejenga vituo vingi kwa idadi lakini bila vifaa vya kufanyia kazi vituo hivi vitakuwa sawasawa na magofu. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Jafo mliangalie hili tupate vifaa kwenye Hospitali yetu ya Wilaya pale Irlongelo lakini na Vituo vya Afya cha Mgori pamoja na kile cha Msange.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, katika bajeti hii tunaomba nyumba za watumishi. Pale llongelo hatuna nyumba ambazo watumishi wangeweza kukodisha wakakaa. Tunahitaji kuwa na madaktari maeneo karibu na vituo hivi pamoja na hospitali. Niombe sana katika bajeti yako hii mtutengee nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ile hospitali tunaitumia kama ofisi ya muda ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Sambamba na hilo, kwa sisi halmashauri zile ambazo tulifurumushwa na Mheshimiwa Rais kule mijini basi tunaomba sasa mtupe fedha haraka sana tuweze kujenga kwenye maeneo yetu ili kusudi wananchi waweze kupata huduma katika maeneo yao ya utawala kama ambavyo Serikali ilikuwa imekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilko tatizo la barabara hasa zinazosimamiwa na *TARURA*. Pamoja na kwamba sasa katika Jimbo langu la Singida Kaskazini barabara mbili za *TANROADS*, ya kutoka llongelo kwenda Ngamu hiyo ilishajaa maji imekatika kabisa. Jana barabara nyingine inayotoka llongelo kwenda Mtinko nayo tayari imeshakatika na nimeambiwa malori mengi sana yamekwama pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ni wa *TANROADS*lakini barabara ambazo zingeweza zikatusaidia kututoa katika tatizo hili, ni barabara za *TARURA* ambazo nyingi sasa zinaweza kusaidia kuweka mizunguko. Sasa hili ni tatizo wananchi kwa mfano wa Ihanuda na walioko kule Ngamu wametengwa na maeneo mengi. Ili waweze kufika mjini wanahangaika wengine mpaka wakapite Katesh kule, wengine mpaka wazungukie huku kwa Mheshimiwa Kiula ili ndio waweze Mheshimiwa Naibu Spika wengine mpaka wazungukie huku kwa Mheshimiwa Kiula ndiyo waweze kufika mjini kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine mpaka wazungukie huku kwa Mheshimiwa Kiula ndiyo waweze kufika mjini kupata huduma. Pia mnawea mkatusaidia hata katika haya maji, ni fursa, maana watu wanatembea katika maji.

Tupeni boti kama hatuwezi basi kwenda kurekebisha hizo barabara kwa sasa. Kwa sababu kila tukiuliza tunaambiwa kitu ambacho ni kweli, kwamba huwezi kurekebisha barabara sasa wakati sasa mvua zinaendelea kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mtusaidie tuwe na vivuko ili wananchi waweze kupata huduma kwa upande mwingine wa pili, kwa sababu wengine wana mashamba huko. Mtu hawezi kuzunguka kilomita zaidi ya 50 kwenda kufuata shamba lako. Kwa hiyo, tunaomba sana, katika Mfuko wa Dharura wa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwangalie, tumepata madhara maeneo mengi, siyo Kilwa tu peke yake na Rufiji; Singida Kaskazini tumepata maafa; kule kwa Mheshimiwa Mtuka ilikuwa ni balaa tupu. Tunaomba nasi tuangaliwe katika Mfuko wa Taifa ili tuweze kupata fedha za dharura kwa sababu nchi yote hii imevamiwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua maji hayajaletwa na Serikali, ndiyo; lakini tuangalie katika mgao tulionao. Sasa tunaomba sana, *TARURA* pale Halmashauri ya Singida *DC* wameomba fedha za dharura kwa muda mrefu, kila mara wanaambiwa uhakiki, kila mara uhakiki, kila mara tunahakiki, mpaka sasa sielewi hata kinachohakikiwa ni nini. Basi tunaomba, kwa kuwa tayari wataalam kutoka *TAMISEMI* walishatumwa, fedha hizo zitolewe ili zile barabara za kuunganishwa, mfano pale Meria kutoka barabara Kuu ya Arusha iweze kuwasaidia wananchi. Sasa hivi tunashindwa kutoa mazao yetu kutoka mashambani kupeleka kwenye masoko.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja, lakini kwa kweli tunaomba sana hizo fedha tuletewe ili marekebisho haya yafanyike. Ahsante sana. *(Makof)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendega na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo mezani kwetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema ambaye ametuwezesha kuendelea na vikao vyetu vya Bunge. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais ambaye moja kwa moja anasimamia Wizara hii ya TAMISEMI kwa kazi nzuri na miongozo mizuri ambayo inasaidia utekelezaji wa mambo mengi na matokeo tunayaona katika kuwafikia wananchi kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Vilevile niwapongeze wasaidizi wake; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa. Wote ni mashahidi kwamba ameenea katika maeneo yote ya nchi yetu. Anashughulikia *Corona*, anashughulikia mazao ya Kahawa na mazao mengine. Haongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Selemani Jafo kwa kazi nzuri anayoifanya katika Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI. Kwa kweli anatosha na shughuli zake tunazona. Amekuwa mfuatiliaji mzuri wa shughuli za maendeleo mikoani na Wilayani. Vile vile Manaibu wake; Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Waitara, kwa kweli TAMISEMI mmejipanga. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwanza kwa usimamizi na uendeshaji wa miradi ambao tunao kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa sasa hivi. Wote mtakuwa mashahidi kwamba katika Mamlaka na Serikali za Mitaa tulikuwa na miradi mingi viporo, lakini kwa kipindi hiki fedha zikitolewa miradi inakamilika. Hongereni sana. Usimamizi wa Vituo vya Afya 350 na Hospitali 67 tungesimamia kama mazoea tungeingia mwaka wa tano huu vituo hivi bado tunaita ni miradi ambayo haijakamilika, lakini ukamilishaji huu wa miradi ni kwa sababu ya ufuatiliaji na usimamizi mzuri

ambao unafanywa na viongozi wa TAMISEMI na watendaji wake wakiongozwa na *Engineer Nyamuhanga*. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napongeza kwa jinsi TAMISEMI na Mheshimiwa Rais alivyosimamia kuhusu matumizi na nidhamu ya fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Wote mnafahamu kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zamani zilipewa majina mengi ikiwemo sisimizi, mchwa nakadhalika, lakini sasa hivi kuna maboresho makubwa sana katika usimamizi wa fedha ambazo zinaenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na ushahidi upo wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata taarifa ambayo imewasilishwa juzi na CAG, kuna maboresho makubwa sana. Hata taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa ametaja kwamba hati za kuridhisha zimeongezeka kutoka asilimia 81 hadi asilimia 95; na hii tano hii siyo kwamba kuna Halmashauri ambayo imeopata hati mbaya, ni zile ambazo zina mashaka. Kwa hiyo, hongera sana, hati mbaya zimeshafutwa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Kigoma Ujiji ambayo ilikula hati chafu kwa miaka minne, mwaka huu imejikongoja imepata hati ambayo inaridhisha. Kwa hiyo, naipongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo imeifanywa kwa kutoa miongozo na sasa hivi fedha zikienda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatumika kama ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Jafo kwa wazo lake la kununua POSna kuzigawa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Zilinunuliwa POS 7,223 zimegawanywa kwenye Halmsahauri zote. POS hizi zitaimarisha ukusanyaji wa mapato na hivi kuongeza mapato katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimjibu kaka yangu Mheshimiwa Japhary, jana alisema kwamba Serikali hii haina nia ya dhati kuhusu ugatuaji. Mheshimiwa Japhary ugatuaji

ni dhana pana sana. Ugatuaji kwanza unategemea mazingira. Serikali ya Awamu ya Tano ina nia ya dhati kabisa katika ugatuaji. Lengo kubwa la ugatuaji ni kupeleka huduma kwa wananchi wake. Hivi vituo 350 vilivyojengwa vyatya afya kazi yake ni kutoa huduma kwa wananchi; huo ni ugatuaji. Hospitali 67 lengo lake ni kupeleka huduma kwa wananchi. Tumeunga *TARURA* na *RUWASA* ili kuhakikisha barabara na maji yanapelekwa vijijini, huo ni ugatuaji kwa hiyo *concept* ya *decentralization* ni pana na tusikariri tu kwamba kama ilivyozungumzwa kwenye *policy paper* ya mwaka 1998. Ile Sera ya mwaka 1998 huwezi kuitekeleza mwaka huu ni zaidi ya miaka 22. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa hivi, bado kuna ugatuaji mkubwa wa rasilimali kupeleka kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali hii ina nia ya dhati kabisa kutekeleza ugatuaji na siyo kama ndugu yangu, mimi namfahamu alikuwa Meya muda mrefu, anafahamu Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hawezu kusema kwamba Serikali hii haina nia. Nia ya dhati ipo na shughuli ambazo zinapelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ngazi za chini ndio ugatuaji wa kisasa kwa sababu sera lazima iangalie na mazingira ya wakati uliopo, hatuwezi kuzungumzia *policy paper* ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka vilevile niungane na wenzangu kuhusu suala la *TARURA*. *TARURA* inafanya kazi vizuri lakini changamoto kubwa iliyopo ni ukosekanaji wa fedha na wataalam. Kwa hiyo, naishauri TAMISEMI kama walivyosema wenzangu kwamba iongezewewe fedha. Inaweza kuongezewa fedha kutoka kwenye vyanzo vingine, lakini kuangalia ule mgao wa fedha za *road fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo naomba Serikali illichukulie kwa umakini sana kwa sababu mtandao wa barabara kwa *TARURA* sasa hivi ni mkubwa sana. Kwa hiyo, wana majukumu mengi na rasilimali walizonazo ni chache. Kwa hiyo, lazima tuiwezeshe *TARURA* iweze kutekeleza majukumu yake ambayo tumeikabidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa nashauri Serikali iwe na kusudio maalum la kuongeza watumishi hasa wa Kitengo cha Uhandisi wa Ujenzi; baada ya kuanza *TARURA*, watumishi wengi wamepelekwa *TARURA* na hivyo Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazina Wahandisi na wataalam wa Idara ya Ujenzi. Kwa hiyo, tuwaongezee watumishi hao ili waweze kutekeleza miradi kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Grace Victor Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Cosato David Chumi, ajiandae.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba hii iliyoko mbele yetu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza viongozi wangu wa Chama hasa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa ujasiri mkubwa alionao katika kukiongoza chama chetu. Pia namshukuru kwa kuniamini kunipa nafasi ya Uwaziri wa Nishati. Nasema sitamwangusha, nitafanya kazi kama inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kuhusu *TARURA*. *TARURA* imekuwa ni changamoto katika maeneo mbalimbali ikiwepo katika Mkoa wetu wa Iringa katika Halmashauri ya Iringa. Kule *TARURA* wanafanya kazi katika mazingira magumu, pesa ni ndogo na kile kiasi ambacho kimetengwa hakiendi kwa wakati na unakuta katika changamoto hizi za mvua kubwa barabara nydingi zimebomoka na wanashindwa kufanya kazi yao inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuangalia kitengo hiki kwa jicho la karibu. Unakuta wakati mwingine ni afadhali ilipokuwa chini ya Halmashauri, Madiwani walikuwa wana uwezo wa kufuatilia na kupata vile vyanzo vya mapato pale na kuweza kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambazo zinatoka Iringa Manispaa kwenda katika Kata ya Luhota - Magulilwa katika Jimbo la Kalenga ambazo nyingi kuna makaravati yamekatika na kubomoka. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuangalia *TARURA* kwa jicho kubwa na hasa katika kipindi hiki ambacho tuna *Corona* ambapo wananchi wanashindwa hata kufika vizuri katikia Vituo vya Afya. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10, amejikita katika kueleza utekelezaji wa bajeti yake kwa mwaka huu wa fedha. Maelezo mengi ambayo yemetolewa pale yameonyesha kiasi cha kazi iliyokusudiwa na kiasi cha fedha ambacho zimetengwa na utekelezaji wake. Napenda kujua ni shilingi ngapi ambazo mlitenga katika kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa? Hiyo imetajwa tu, haikuwekewa ainisho kama maeneo mengine yalivyoanishwa. Kwa sababu tunaona maeneo yaliyo mengi uchaguzi haukufanyika karibu asilimia 95, watu walipita bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba ile chenji irudi iende kwenye tiba na barabara ili tujue ni kiasi gani ambacho kilibakia kinachoweza kuchukuliwa na kwenda kufanya kazi nyiningine. Nimesema hivi kwa sababu kuna maeneo ambayo wameonyesha ukurasa wa 11 na kuendelea Tume ya Utumishi Walimu, Mamlaka ya Serikali za Mtaa kuna fedha zimetengwa na kazi zimetekelvezeka. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda pia katika miradi ya kimkakati ambayo iko ukurasa wa 34, kuna fedha ambazo zimeidhinishwa zaidi ya shilingi bilioni 70 ambazo zimekwenda

kwa wenye maeneo mbalimbali ya miradi ya kimkakati. Nilikuwa napenda kuuliza, ni lini *Iringa DC* ambayo ina Majimbo mawili; Kalenga na Isimani tutaingizwa kwenye huo mradi wa kimkakati? Kwa sababu ni muda mrefu sasa tumeweza kuweka miradi yetu ya kimkakati lakini tunajafikiwa. Tunaona Majimbo ni mengi pale yameelekezwa lakini napenda kujua *Iringa DC* ni lini tutafikiwa katika hiyo miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika suala zima la utawala bora ambalo amelielezea, kwa sababu hii Wizara ni mtambuka, ina mambo mengi ambayo yanafanyika hapo. Kuna kitendo cha viongozi ambao ni wakubwa katika mikoa yetu; Wakuu wa Mikoa na wengine ambao ni Wakuu wa Wilaya wanawadharau Madiwani. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Iringa na katika Mkutano wake, Waheshimiwa Madiwani walio wengi walitaka kugoma kwenda kwenye Mkutano, lakini ilikuwa ni kwa sababu ya mahusiano yasiyo mazuri kati yao na Mkuu wa Mkoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu akifika anawatambulisha Waheshimiwa Wabunge wanasalimia wananchi, lakini Mkuu wa Mkoa akienda kwenye Kata hasalimishi Madiwani; na Madiwani wamekuwa ni wanyonge hadi hawana hamu ya kufanya kazi na Mkuu wa Mkoa, kwa sababu amekuwa akiwadhalilisha. Kuna Madiwani wawili; Diwani wa kutoka Kata ya Ulanda na Diwani kutoka Kata ya Masaka aliwaweka ndani pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Jafo aweze kuangalia viongozi kama hawa, wanakatisha tamaa viongozi wetu. Madiwani ni viongozi ambao ndio wanawatafutia kura Wabunge na Rais, lakini leo hii tunawaweka mahali mbali kabisa hatuwatambui. Mnasema tuna mafiga matatu wakati wa uchaguzi na tumefika... (*Makofii*)

MHE. MWITA B. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwita Boniface Getere.

TAARIFA

MHE. MWITA B. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampa taarifa Mheshimiwa Grace kwamba ni kweli kuna heshima zipo zinafanyika, lakini sasa labda tuulizane tu, kwamba mimi kama Mkuu wa Mkoa nimekuja kwako, nimekuta umepewa mradi wa wananchi umeiba, umehujumu hela za wananchi, sasa nitakupaje heshima ya kutokukumata?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega endelea na mchango wako.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Ahsante naomba niendelee. Viongozi wanapaswa kuwa na hekima katika nchi hii na tunaona jinsi ambavyo viongozi wetu walio wengi wanafikia mahali ambapo wananchi wanashindwa kuwathamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hao Waheshimiwa Madiwani baadhi ya maeneo wamekuwa hawalipwi stahiki zao. Mheshimiwa Gimbi jana amezungumza. Leo nina karatasi hii hapa, nitamkabidhi Mheshimiwa Jafo. Kuna Halmashauri ya Wilaya ya Biharadulo, Madiwani wamekopa, wanakatwa fedha na Halmashauri, inapaswa ipelekwe benki, lakini haipeleki benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *outstanding* ya shilingi milioni 137 na wanakwenda kustaafu. Hizi pesa wanazipata wapi katika kipindi hiki ambacho tuna changamoto ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu?

Kwa hiyo, hawa Madiwani nina *list* na wapo wameenda kule. Namwomba Mheshimiwa Waziri, fedha hizi, azifuatilie na Wakurugenzi kama hawa ambao wanafanya kitu kama hiki na kuwafanya Madiwani wetu wawe hawafanyi kazi kwa umakini.

Vilevile katika suala la afya katika Halmashauri zetu kumekuwa na changamoto. Kuna baadhi ya maeneo wanasema kuna waraka. Napenda kujua, hivi kuna waraka umekwenda wa uchangiaji wa fedha? Akina mama wanaojifungua wanatozwa shilingi 40,000; wanofanyiwa upasuaji wanatozwa shilingi 150,000; wazee wanatozwa shilingi 15,000/= na hata wale wenye maambukizi ya UKIMWI wanatozwa shilingi 15,000. Hivi Serikali tunaposema tumejenga hospitali, tumejenga zahanati; tunapokuja na vitu kama hivi vya kuchangisha watu fedha hizi zote, kwanza hatujapitisha hivi viwango kwenye Bunge letu.

Napenda kujua, kuna waraka kama huo ama ni hao watu wanatafuta vyanzo vyao na kuwafanya Watanzania wawe na hali mbaya katika utekelezaji wa majukumu yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba mheshimiwa Waziri, kuna masuala mengi ambayo yanaendelea katika Halmashauri mbalimbali na yanawaumiza Watanzania, mwone namna ya kuyafanya kazi ili watu waweze kupata huduma inayostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika ahadi mlisema kutakuwa na bajaji ambazo ni kama *ambulance*. Mimi sijazona Kalenga hizo bajaji, sijui mliishia wapi! Ndiyo maana tunauliza, shilingi milioni 50 ziliishia wapi? Mlisema ni ahadi, tulikuwa na swali la msingi hapa wakati Waziri wa TAMISEMI akiwa Mheshimiwa Simbachawene, akasema, itatekelezwa katika Awamu hii ya Tano na siyo awamu nyiningine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango yuko hapa, atakuja kutuambia zile milioni 50 zimeenda wapi hatujazona katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu spika, suala lingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, ajiandae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenijaalia uzima lakini pia nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambae ndiye anasimamia moja kwa moja Wizara hili lakini pia ambaYe anatuongoza kwenye Nchi yetu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya ndani ya Nchi yetu. Serikali ya Awamu ya Tano inafanyakazi nzuri na ukiangalia kazi inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano unashawishika kukubaliana na yale maneno kwamba ikiwezekana hatuna sababu ya kuwa na uchaguzi wa Rais mwaka huu, Mheshimiwa Rais apite bila kupingwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Jafo na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote na Manaibu Katibu Wakuu. TAMISEMI inafanyakazi nzuri sana, inafanyakazi nzuri, inatusaidia sana na Wananchi wetu ni mashahidi wa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na TAMISEMI. Ni bahati mbaya tu kwamba jana nilisikiliza hotuba ya Mzee wangu Mzee Japhar ambaye namheshimu sana, ukisikiliza hotuba yake ni kama vile haoni kinachofanyika lakini pia ni kama vile hata hotuba yenyewe hakuisoma amekuja na mambo ambayo alikuwa anataka kuyaleta tuje tuyasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika ukiangalia kuna hoja kubwa mbili; hoja ya kwanza tunasema Serikali zetu za Mitaa zimepokwa mamlaka lakini hoja ya pili tunasema tumeoporwa vyanzo vya mapato. Sasa hii ya ugatuaji wa madaraka, RAS Mstaafu Mzee wangu Mheshimiwa Chikota ameshaisema

vizuri. Niseme kidogo kwenye hili la kusema kwamba tumeporwa vyanzo vy a mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza siyo sawa sawa tukitumia lugha kama vyanzo vy a mapato vimeporwa kwenye Serikali za Mitaa. Siyo sawa sawa kwasababu kilichofanyika tunaweza kusema ni mabadiliko ya namna ya mkukusanya mapato na mabadiliko hayo yamefanyika kwenye sehemu kubwa tatu; nani anayekusanya, namna ya kukusanya na matumizi ya makusanyo hayo yanayokusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule vijijini leo wananchi hawatakuelewa wakiambiwa wameporwa mapato kwasababu haya mabadiliko yaliyofanyika ndiyo yaliyotusaidia pamoja na kwamba tulikuwa tunakusanya kodi za ardhi miaka yote lakini tulikuwa kwenye halmashauri hatutengi fedha za kupima wala kupanga na migogoro ya ardhi ikaendelea kuwa mingi. Mwaka huu wa fedha tuliokuwa nao Serikali imetoa bilioni sita kwenye halmashauri kwa ajili ya kusaidia kupanga na kupima Miji yetu kazi ambayo hatukuwa tumeweza kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni wakati tunakusanya kwenye halmashauri, *premium* ukiwa mtu unataka kumilikishwa kiwanja kwa awamu ya kwanza ilikuwa ni 7.5 percent ya thamani ya ardhi. Baada ya kupelekwa Wizarani imeshuka imekuwa 2.5 huku siyo kuperwa, huku ni kuwasaidia Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia haya mabadi;liko yanayolalamikiwa ndiyo yaliyotusaidia mpaka mkulima anayesafirisha mazao chini ya tani moja hatozwi ushuru. Haya ni mabadiliko yaliyowasaidia wananchi na siyo kuperwa kwa vyanzo vy a mapato. Haya mabadiliko ndiyo yametusaidia Wajasiriamali akikata kitambulisho cha shilingi 20,000 hasumbuliwi kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku siyo kuperwa kwa vyanzo vy a mapato, huku ni mabadiliko ya namna ya

kukusanya na mabadiliko haya pia yameonekana kwenye matumizi. Hata tungechukua vyanzo vyote sisi tusingeweza kujenga hospitali ya Wilaya ya bilioni 1.5. Kwa mfumo huu wa makusanyo tumeweza kujenga hospitali za wilaya, tumeweza kujenga vituo vya afya, tumeweza kujenga zahanati, tumebadilisha namna ya kukusanya na namna ya kutumia mapato yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi huu kutoa tu ushauri kidogo kwenye maeneo machache yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Eneo la kwanza ni *TARURA*; pamoja na kazi kubwa inayofanywa na *TARURA* bado tuna changamotoi nyingi kwenye maeneo yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara tunasmhukuru ametusaidia sana lakini bado ziko barabara ambazo kwasababu ya changamoto ya mvua hazipitiki. Kuna barabara ya Makuyuni kwenda Kwemshai, kuna barabara ya Makuyuni-Zege Mpakani, kuna barabara ya Msambiazi mpaka Lutindi lakini pia iko barabara ya Kerenge kwenda Kijangwa mpaka Magoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ziko changamoto ya madaraja; sisi Korogwe tulipata maafa kabla ya hizi mvua za mwaka jana tulipata mvua mwaka 2016 kuna daraja la Makondeko kule Magamba Kwalukonge, kuna daraja ya Mswaha na kuna daraja jingine linaitwa daraja la Msituni kule Kimbo yaliharibika mwaka 2016 lakini mpaka leo hatujaweza kuyenteneza kwanini? Kwasababu hatuna fedha, *TARURA* ina fedha chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe sana Serikali. Hoja ya kuomba *TARURA* kuongezewa fedha ni hoja ya msingi tunaomba ichukuliwe na ipewe uzitoi unaostahili. Lakini jambo la pili; tuwaombe *TARURA* kama wanavyofanya kwenye baadhi ya maeneo ya Mijini kubuni miradi na kuandika maandiko kwa ajili ya miradi mbalimbali mtusaidie pia na maeneo ya vijijini. Yako maeneo tukiandika maandiko tunawezakupata fedha kwa wafadhili, tunaweza kupata fedha kwa wahisani tukasaidia kutengeneza hizi barabara za maeneo ya vijijini ili wananchi wetu waweze kufanya

shughuli vizuri, waweze kusafirisha mazao yao lakini waweze kutoka sehemu moja kwendasehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwaombe TARURA imarisheni sana kile kitengo cha ku-*design*. Haiwezekani daraja moja tuka-*design* tangu mwaka 2016. Haya madaraja niliyoyataja kila tukiuliza tunaambiwa wako kwenye *design*. Ningombaa hiki kitengo kiimarishe ili kazi ifanyike kwa wakati tuweze kumaliza mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ni eneo la afya; niwapongeze sana TAMISEMI kwenye hotuba nimeona mmetenga fedha kwa ajili ya zahanati lakini ningombaa tu nikumbushe; alichokisema Mheshimiwa Keissy ni kitu cha msingi sana. Nitoe tu mfano mdogo na hapa naomba Ndugu zangu wa Korogwe Mji wasinielewe vibaya; Halmashauri ya Mji wa Korogwe ina mitaa 22, ina vijiji saba. Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ambayo ndiyo Korogwe vijijini ina vijiji 118 na ina mamlaka ya Mji mdogo moja yenye Vitongoji 20. Unapotupa zahanati tatu kila Halmashauri unakuwa hututendei sisi wengine ambao tuna maeneo makubwa. Tunaomba sana muangalie namna ya kugawa hizi pesa ndogo mlizokuwa nazo, sisi hapa tuna maeneo makubwa tuweze kupata ambacho kinastahilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipewa fedha kwa ajili ya vituo vya afya. Tumejenga kituo cha afya kule Korogwe kinaitwa Mkumbara, tunajenga kituo cha afya sehemu inaitwa Kerenge, tulipewa milioni 200. Sasa sijaona kwenye bajeti mpango wa kuendelezwa maana yake milioni 200 ni kama jengo moja tu. Sasa tuna mpango gani kwa mwaka wa fedha unaokuja kwa maeneo mengine yaliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine kama nilivyosema pamoja na hizi zahanati tatu tunazopewa, lakini bado tuna vijiji vingi na wananchi wamejenga kwa nguvu sana Maboma ya madarasa na zahanati na fedha hizi ni chache. Tunaomba sana muangalie namna ya kutuungeza tuweze kufanikiwa kufanya hiyo kazi na kuwasaidia wananchi wetu.

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kushauri kwenye eneo la mwisho kwenye...

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha, ahsante sana.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan bobali, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru wka kunipa nafasi, nianze kwa Zaburi 127:1-2 inayosema ... "Bwana asipoujenga Mji waujengao wakesha bure au Bwana asipoulinda Mji, asipolinda nyumba, asipolinda chochote walindao wakesha bure" ... Watu wengi wamesema kuhisiana na corona na mimi nasema tuendelee kuchukua tahadhari kama ambavyo Serikali imekuwa ikituelekeza lakini tusimsahau Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama ulivyotuelekeza muda wetu ni mchache. Napenda kupongeza kwanza kabisa Mheshimiwa Rais umesema tusitaje Nchi lakini sisi tulipokuwa Nchi fulani mwezi Desemba kwenye mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki tukipita mitaani na zile jezi zetu zimeandikwa Tanzania watu wanasema "Magufuli oyeee" na hawa watu wenyewe hata Kiswahili hawakijui vizuri lakini wanasema "Ohhh Magufuli oyeee" mtu unastuka unageuka, kuna nani hapa? "Magufuli oyeee" ni Nchi ya watu. Kwahiyio, sitaki kusema sana mnaweza tu kupata tu picha ya yale yanayofanyika jinsi ambavyo yanakubalika mpaka kwenye nje ya mipaka yetu. Sasa wewe ambaye uko ndani na huyaoni mimi sitaki ule msemo wa kusema "mnyonge mnyongeni hali yake mpeni" hapana wala msimnyonge mpeni tu haki yake maana ukishamnyonga haki ataipata saaa ngapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake wanasema uungwana ni vitendo, hawa ni watu waungwana. Una jambo unakwenda pale kwa Katibu Mkuu au Naibu Katibu Mkuu afya au elimu au Manaibu wake hawa anakusikiliza kwa utulivu na lile lililokupeleka pale linapata suluhisho hata kama siyo kwa wakati huo basi linatafutiwa namna ya kupata suluhisho. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa utendaji wa namna hii. Kweli wanamsaidia Mheshimiwa Rais, wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanamsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais. Tuendelee kufanyakazi kwa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sitakuwa natenda haki kama sitapongeza ushirikiano katika Ofisi yetu ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Katibu Tawala Mkoa wa Iringa lakini katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Mkurugenzi, Waheshimiwa Madiwani, Mkuu wetu wa Wilaya pale Mufindi na hata Chama chetu Cha Mapinduzi chini ya *Comrade Yassin Daudi* tunafanyakazi na ndiyo maana kwa ushirikiano na uchapakazi Halmashauri ya Mji wa Mafinga ambayo hata miaka mitano hajatimiza, kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa katika tatu bora katika suala zima la elimu, kwanini? Kwasababu tumejenga miundombinu ya kutosha, usimamazi umekuwa bora lakini pia ushirikiano umekuwa ukituongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nina ombi moja; wakati Serikali inagawa walimu wa Sayansi, halmashauri zote za miji hazikupewa walimu wa masomo ya sayansi na hesabu. Maana kuna ile dhana kwamba tuliko Mjini pengine hatuna matatizo sana, hapana. Tuna matatizo na uhitaji kwa sababu pia hata shule zetu zina watoto wengi sana. Kwa hiyo, nionome Serikali wakati itakapopanga walimu tena ijaribu kututazama na sisi Halmashauri za Mji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza wadau ambao tunashirikiana nao wakiwepo shamba ya Sao hill misitu na wakala wa misitu-Tanzania. Tunapozungumza hivi kwa ushirikiano wanajenga Bweni pale shule ya Luganga sekondari na shule ya sekondari

Changarawe ili kupungiza *distance* ya watoto kutembea hasa watoto wa kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika afya napenda kupongeza, nakushukuru tumepata kituo cha afya cha Ihongole na zahanati kadhaa sasa zinafanyakazi katika kipindi cha Awamu huu toka imeanza kazi. Hata hivyo ninaomba Serikali iangalie katika kituo cha afya cha Bumilahinga, tumekuwa tukiomba ni muda mrefu.

Mhehsimiwa Waziri, Mafinga wakati naingia wakina Mama wajawazito waliokuwa wanapata huduma katika hospitali ya Mafinga kwa mwezi walikuwa takribani 200. Ninapozungumza sasa hivi ni 650. Kati yao 150 ni kwa *operation*. Kwa hiyo, tukiborseha kituo cha afya cha Bumilahinga maana yake ni kwamba tutapunguza mzigo katika hospitali ya Mafinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako umesema kuhusu kuweshesha Wananchi; napongeza vizkundi vinapata fedha, vikundi vinafanyakazi lakini nikuombe kwasababu hii ni Wizara mtambuka nimewahi kulisema hili hapa Bungeni; Miji ambayo iko kando ya barabara Miji kama Mikumi, Miji kama Ruaha mbuyuni, Miji kama Mafinga tuone uwezekano wa kuwa na taratibu ambazo watu hawa watafanyakazi masaa 24 wafanye uzalishaji wapate kipato wachangie pato la Taifa, kwanini nasema hivi? Kazi ya Dola Duniani kote ni ulinzi na usalama sasa sisi tuwape hawa wakinamama ambaao tumewapa mikopo na vijana muda wa kutosha wa kufanyakazi. Jeshi la Polisi kazi yao iwe ni kuwalinda wafanyakazi na biashara muda wote. Sisi tuna viwanda vya mazao ya misitu, vijana wametoka msituni saa tano anataka aende mahali akapate chakula kumeshafungwa kwasababu Polisi nao wanatimiza wajibu wao kwasababu ndiyo Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri inawezekana lisiwe moja kwa moja kwako lakini kwasabbau ni Wizara mtambuka tuone baadhi ya maeneo watu wafanyakazi masaa 24, watu wafanye

biashara masaa 24. Tunashukuru mlituelewa kwenye suala la kusafiriha mazao ya misitu masaa 24 tunakwenda vizuri na mkija kufanya tathmini mtaona kwa vyovyote mapato yameongezeka. Kwa hiyo, ili kunyanya uchumi wa watu hawa ambao tunawapa mikopo tuwaache wajiache wafanye biashara kwa mujibu wa utaratibu na Kanuni lakini wafanye kazi kwa muda wote ambao inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya wenzangu wamesema sana kuhusu *TARURA*; hali ya barabara zetu kwa kweli tunaiona pamoja na kuwa *road fund* haiwezei kutosheleza kama wengine walivyosema. Hapa katika takwimu yangu Mheshimiwa Waziri *TARURA* itajenga barabara za lami kilometra 35 tu katika bajeti hii tunayoianza Mwaka 2020/2021. Unaweza ukaona mgao ni mchache kiasi gani. Kwa hiyo, niombe, Serikali ni sikivu, ni tulivu. Mkae muone kama kile kinachotoka kwenye *road fund* ni kichache basi tuone tutapata wapi ili kwa kweli tuijengee *TARURA* uwezo barabara angalau zipitike kwa mwaka mzima barabara zinazobeba mazao, zinazobeba mbolea ambazo kwa namna moja au nyingine zinachangia katika kusisimua uchumi na kuongeza kipato cha Wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya naunga mkono hoja na Mungu atubariki wote kama nilivyosema tuchukue tahadhari lakini tusimsahau Mungu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Raphael Japhar Michael ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya TAMISEMI kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kunipa uzima na afya lakini pia itoshe kusema Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri, nimefarijika sana mlipoamua kunihamisha kwenye Kamati niliyokuwa nimehudumu kwa miaka miwili na nusu nikapelekwa kwenye

Kamati hii kwa kweli nimejifunza kitu kikubwa sana. Nimejifunza ushirikiano baina ya Kamati na Wizara lakini pia nimewakuta watu wema wanaojali utu na wanaosikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Katibu Mkuu mstaafu wa Wizara hii Mheshimiwa Mussa Iyombe anaondoka, anastaafu tulidhani kwamba tumepata pengo kubwa lakini kitendo cha kuletwta Katibu Mkuu wa sasa, Eng. Nyamuhanga kwa kweli ni mtu anayechapakazi, anayefanyakazi vizuri sana. Napenda niwe mkweli katika hili na anasikiliza. Ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. Tunafanyanae kazi vizuri, anatoa ushirikiano na wasaidizi wake; Naibu Katibu Mkuu Doroth Gwajima na Gerald Mweri nae anafanyakazi nzuri sana. Kwa hiyo, ningetaka hili nilisema kwamba kama Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI, kiukweli kabisa tunafarijika na namna watu hawa tunavyofanya nao kazi katika kipindi hiki ambacho tumekuwepo Wajumbe wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze hili la Madiwani; jana niliona kulikuwa na mzozo kidogo juu ya stahiki za Madiwani. Sisi kwenye Kamati tumeweke na pendekezo la pili kabisa na Mwenyekiti wetu wa Kamati alilisoma; tunaomba Waheshimiwa Madiwani Nchi nzima walipwe stahiki zao na tumeweke ukomo. Ukipika tarehe 30 ya Mwezi wa Tano, Madiwani Nchi nzima wawe wamelipwa vile viporo vya vya posho ya *sitting*, yale madeni kule Benki na *CHF* ambako wamekuwa wakikatwa fedha lakini halmashauri hazipeleki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati imeonyesha wkamba kwa Mkoa mmoja wa Singida pekee, Madiwani wanadai zaidi ya shilingi milioni 658. Hiki ni kiwango kikubwa na ukizungumza Nchi nzima ni fedha nyngi na Madiwani wengi wanadai. Nikitolea mfano kwenye halmashauri ya kwangu pale, Madiwani wanadai zaidi ya shilingi milioni 90 na hivi karibuni waligma hata kufanyakazi kwa kutoshiriki kwenye vikao mpaka Mkuu wa Mkoo akaingilia kati. Sasa ukikusanya takwimu za namna hii nchi nzima unaona kwamba hali siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri alipokuja kwenye Kamati alisema kwamba atalifuatilia na sisi tunasisitiza kwamba ni vyema jambo hili likafuatiliwa, hawa Madiwani ni wanasiasa wenzetu hali zao kule chini zinajulikana. Kwa hiyo, tukimaliza Bunge, Diwani akimaliza udiwani wake akaondoka akawa anadai halmashauri kwanza hawa Wakurugenzi hata kuwasikiliza sidhani kama watawasikiliza. Kwa hiyo, hili lazima tulisisitiza ili wenzetu hawa na wenyewe wapate stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Jimbo la Mchinga Mheshimiwa Rais alifanya maamuzi ya kulihamisha kulipeleka Manispaa ya Lindi kutoka kwenye halmashauri iliyokuwa ya Lindi vijijini. Jambo hili kama Mbunge nimeshalipongeza humu ndani ya Bunge wakati tunachangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Narudia tena, kwa kweli jambo hili watu wa Mchinga tunalipongeza na tunampongeza Rais kwa uamuzi huu. Kazi iliyobakia ni kwa Waziri na timu yake sasa kufanya ule utaratibu ili ikifika Mwezi Julai tarehe 01 sisi watu wa Mchinga tujue sasa tunawajibika kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi kwasababu kuna mambo mengi ya kujipanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, zile fedha zilizotengwa sasa nimeona hapa imeandikwa Halmashauri ya Mtama na wenzangu wamezungumzia hapa tunapoongeza Jimbo la Mchinga kwenye Manispaa ya Lindi sasa tutakuwa na Kata 32 kwenye Manispaa na maana yake ni kwamba mzigo umeongezeka. Ukitupa zahanati tatu kwenye Manispaa ya Kata 32 na ukubwa wa eneo uliopo kwa kweli utakuwa ni kama siyo sahihi. Kwa hiyo, hapa nadhani falsafa ilipaswa kuwa haki sawa kwa wote siyo haki sawa sawa kwa wote kwasababu haki sawa kwa wote *it depends the rationality* kwamba huyu ni mkubwa, ana Kata nydingi, ana eneo kubwa pia lazima na ye ye apate kingi kwa hiyo, *rationality* lazima itumike na nashukuru umelisisitiza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye *TARURA*; kuna haja ya kushauri ama ya kutafuta vyanzo vypya vya fedha kuiongezea nguvu *TARURA*. Nitawakumbusha Waheshimiwa

Wabunge; *TARURA* mwaka huu imetengewa shilingi bilioni 275 kwa fedha za ndani na shilingi bilioni 28 kwa fedha za nje. Hizi bilioni 28 ni zile za kwenda kutengeneza barabara katika maeneo ya kimkakati kwa ajili ya maeneo yale yanayozalisha mazao ya kilimo. Sasa Nchi yetu eneo kubwa tunategemea kilimo na hizi bilioni 28 ni fedha za nje na kwa bahati mbaya sana mwaka huu tuna hili janga la *corona*, sifirkii Mwenyezi Mungu atuepushie mbali lakini inawezekana fedha za nje zikawa zina shida kwa sababu ya hili tatizo limeikumba dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia vyanzo vipyta vya *TARURA* shilingi bilioni mia tatu kwa jumla yake haziwezi kutatua changamoto ambazo zipo zilizosababishwa na mafuriko kwenye maeneo mengi karibu nchi nzima. Barabara za Jimbo Mchinga zimeadhirika kwa kiwango kikubwa sana, narudia kusema kwa mfano barabara ambayo inaelekea kwenye eneo linalozalisha ufuta mwingi kabisa, barabara ya kutoka Mkwajuni kuelekea Mnyangara kwenda Mipingo na Mkongo zimekufa kabisa hazipitiki na ufuta umelimwa mwaka huu na utapatikana kwa kiwango kikubwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutashindwa kuusafirisha kupeleka sokoni kwa sababu ya barabara kuwa zimekufa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kunasuala la fedha zimetengwa kwa ajili ya vituo vya afya bilioni 50, fedha hizi ni fedha za nje, ningeomba Serikali kuwa na mkakati mwingine wa kuhakikisha kwamba endapo itatokea fedha za nje hazikupatikana, basi sisi wenyewe tutumie fedha zetu za ndani tuweze kugharamia jambo hilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, napenda nizungumzie suala la *corona*, shule zimefungwa ni uamuza mzuri kabisa. Sasa nashauri,Wizara ina mambo mengi ambayo yamesimama kutohana na shule kufungwa sifirkii kama zile fedha ambazo zilikuwa zinapelekwa kila mwezi za kugharamia elimu bure sidhani kama hata kama zikipelekwa zitakwenda kufanya kazi gani, kuna zaidi ya mwezi zilisimama. Nilikuwa nafanya mahesabu kila halmashauri kila mwezi

ilikuwa inapelekewa fedha isiyopungua milioni 50 kwa maana kwamba fedha za sekondari na fedha za shule za msingi, kwanini Wizara isitumie hizi milioni 50 ambazo ziliikuwa zinakwenda kila halmashauri kwa wastani ikatumia kununua *sanitizer* na vifaa wakapewa wanafunzi wale wale ambao wangeweza kuzitumia fedha hizo wakiwa shulenii, sidhani kama kuna haja sasa hivi tena ya kununua chaki na mambo mengine ambayo zinapelekewa hizi fedha zikatumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Wizara iamue kuchukua hizi fedha sasa hivi inunue *sanitizer* na vifaa vingine tuwapelekee hawa wanafunzi walioko huko majumbani kwao huko vijijini kwa sababu hawa wanafunzi wa vijijini uwezo wa kupata *sanitizer* kwa kweli umekuwa ni mgumu na sifikihi hata kama wanao.

Kwa hiyo, naomba fedha zile za elimu bure sasa zitumike moja kwa moja kugharamia vifaa vyatujinga na *corona* na wazitumie wenyewe wanafunzi ambao walikuwa wamekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema la mwisho lakini nimalizie tu kwamba, kuna jambo la Kituo cha Afya pale Milola, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea pale, akalalamikiwa na wananchi kwamba kuna shida kubwa na kiukweli kabisa kuna shida pale Milola, watu wengi huduma ya afya hawana kituo cha afya, mimi kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Jimbo nimeanza ujenzi, tumejenga tumeshamaliza msingi na sasa tunajenga boma, ningeomba hizi fedha zikipatikana za vituo vyatujinga watupelekee pale Milola ili tukamalizie kile kituo cha afya ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi, kwa sababu wananchi ni wengi sana na wanahitaji huduma. Hii ingepunguza kero kwa sababu wananchi wako mpakani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wengi wanaondoka wanaenda kutibiwa Ruangwa katika Kituo cha Afya cha Mandawa wakati pale na sisi tungeweza kupata cha kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Japhet Michael na Mheshimiwa Mwita Getere Boniphace ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia hotuba iliyokuwa mbele yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwezi Novemba, 2015 waliahidi na wametekeleza. Mheshimiwa Rais aliahidi kupambana na rushwa na ujisadi lakini pia aliahidi kuimarisha utawala bora, Mheshimiwa Rais aliahidi kurudisha nidhamu Serikalini, ujenzi wa Tanzania ya viwanda, sisi sote humu ndani mashahidi hayo mambo yanaendelea kutekelezeka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akifanya kazi kubwa ndani na nje ya Bunge, mara kadhaa nimemfuata kumwomba kuzungumza naye kwa masuala yanayowakabili wafanyakazi nchini lakini masuala ya migogoro na wafugaji wa kule Magindu na masuala kadha wa kadha ya Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Waziri Mkuu amenipa nafasi hiyo. Kiukweli Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akitoa nafasi kwa Wabunge wote wa Upinzani na wa CCM, Wabunge wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo, lakini pia Wabunge wa wale wa awamu ya kwanza na wale Wabunge wazoefu, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutupa nafasi hiyo Wabunge wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia mchango wangu kufuatia ugonjwa unaoikabili dunia na Taifa letu la Tanzania, kiukweli nipende kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo imeamua kuchukua kufunga shule za awali, msingi pamoja na sekondari. Hii ni hatua nzuri sana kwa

sababu wale watoto ni wadogo sana kiasi kwamba tungenesema tuendelee kuwaacha mashulenii, basi tungekuwa tumewaweka kwenye *risk* kubwa ya kuweza penginge kupata maambukizi. Sasa licha ya kwamba tunakabiliwa na maradhi haya hapa nchini lazima maendeleo ya elimu yaweze kuendelea, hivyo basi ninaushauri kadhaa kwa Serikali yangu ya namna ya kufanya kuweza kuwasaidia watoto hawa ili tusije tukawasababishia matatizo hapo baadaye na isitoshe hatujui huu ugonjwa utaenda mpaka lini na watoto hawa ndiyo Taifa la kesho na ndiyo viongozi wa kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba, moja tuangalie aidha kama watatenga bajeti ama kutumika hela hiso za elimu bure, vyovyyote vile itakavyokuwa, lakini tuje na mpango wa *home schooling*, lazima watoto hawa wasome majumbani, Walimu wetu waandae andalio la somo, ile sijui wanaita *lesson plan* ambayo wanaweza wakaweka kwenye *flash* ama kwenye *CD* watoto wakaendelea kujifunza majumbani kwa kupitia *television*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine, ni lazima Serikali sasa tuje na mpango wa *distance learning* kwamba hii *distance learning* tunaweza tukatumia *frequency* mojawapo ama *frequency* maalum ambapo Walimu watakuwa wanatoa masomo huko halafu watoto nyumbani wana *tune* kwenye radio na kuweza kupata maendeleo ama masomo jinsi yatakavyoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kuiomba Serikali hizi *facilities* za *distance learning* pia tungejiandaa nazo, suala nzima kwa maeneo ambayo hayana umeme kwa sababu tutatumia teknolojia ya TEHAMA, *Tabletna* simu, vyote hivi vinaweza kumsaidia mwanafunzi kuendelea na masomo yake akiwa nyumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusiana na TAMISEMI, niendelee kuwapongeza sana Mheshimiwa Jafo

na Manaibu Waziri wake, wameendelea kutusaidia Mkoa wa Pwani wametupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Halmashauri. Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti imepata bilioni tatu na milioni mia tano, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha bilioni nne, Chalinze bilioni tano, Mafia bilioni tano na milioni mia saba na kote huku ujenzi uko katika hatua nzuri, tunaishukuru sana Serikali isipokuwa hapa kuna changamoto moja napenda kushauri kwa Serikali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyokuwepo hapa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa utoaji wa fedha, wakandarasi wanamaliza hatua Fulani,Wakurugenzi ama niseme halmashauri ina *issue certificate*,sasa zile certificate zinachukua muda mrefu sana, miezi mitatu mpaka mitano ili kuweza kulipa ujenzi uweze kuendelea. Changamoto iliyokuwepo hapa tunachelewesha huu ujenzi wa hizi halmashauri zetu ama wa haya majengo ya halmashauri zetu. Kimsingi wenzenetu wa hapa Hazina kidogo wanatuangusha, mfano wa Halmashauri ya Kibiti wame-*issue certificate* ya milioni 300 na milioni mia tano ambayo huu ni mwezi wa tatu hatujapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ime-*issue certificate* ya milioni mia moja ishirini na tano, huu ni mwezi wa tatu Hazina hawajatupatia; Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti tume-*issue certificate* ya milioni 470, mpaka leo hawajatupatia. Kwa hiyo, napenda kuwaomba Hazina mwanzoni walikuwa na utaratibu mzuri wanaingiza fedha kwenye akaunti za halmashauri,wenyewe wanalipa, sasa wamerudisha hili jukumu kwao, kwamba tukimaliza tunapeleka *certificate* kwa othen ndiyo wawalipe wakandarasi, wanatuchelewesha, kwa hiyo ushauri wangu turudi kwenye ule utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho, nipende kutumia nafasi hii kuupongeza sana Kata ya Soga wanajitahidi mno, tuliwashauri kulinda maeneo, wamelinda maeneo yao vizuri, leo tumepata pale mwekezaji *Tan Choice*, ametengeneza kiwanda kikubwa ambacho kimsingi kile kiwanda kama si *corona* kingekuwa

kimeshazinduliwa na kuanza kazi, lakini kwa sababu ya haya matatizo ya *corona* ndiyo bado kidogo hakijaanza kazi. Kile kiwanda kikianza kazi Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha tunategemea kwenda kupata bilioni mbili na milioni mia saba kwa mwaka, lakini kwa *turn over* kile kiwanda tunaenda kupata *service levy* ya asilimia 3.2. Kwa maana hiyo nirudi pale pale pa kuendelea kpongeza; napenda kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na sisi Madiwani wa halmashauri hiyo kwa namna tulivyoweza kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere Boniphace na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul ajiandae.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na nimshukuru Mungu sana kwa kupata tena fursa hii ya kuongea baada ya kusoma hotuba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala ambalo ni muhimu na nimelizungumza kwa muda mrefu ninapokuwa Bungeni kwa miaka yangu yote karibu mitano, suala la ugatuaji wa madaraka. Mimi sina tatizo lolote na mambo ambayo sasa hivi yanafanyika katika Serikali hii kwa maana ya kupeleka maendeleo kwenye maeneo mbalimbali kwa sababu hata mimi ninawiwa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi mwenye dhamana anajitahidi kufanya kazi zake kwa uwezo mkubwa na kwa weledi mkubwa na kwa kweli tunapaswa kumpa heshima kwa kazi kubwa aliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba, maana yake hata Moshi leo amenipa milioni 400 kwa kituo cha afya. Nina shilingi za kutosha za kwenye shule kongwe

ambazo zilikuwa zimekarabatiwa,kwa hiyo mimi sibishani na kwamba kuna fedha zinazotolewa kwenye maeneo mbalimbali katika nchi hii. Hoja yangu ni kwamba kuna mahali tulikuwa tumefikia katika Serikali ya Awamu ya Tatu na tukatengeneza sera na mfumo ambao ungetusaidia kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi. Ni kweli kwamba dhana ya *decentralization* pana wala hakuna ubishani na ndiyo maana kuna dhana ya *decentralization by deconcentration*, kuna dhana ya *decentralization by delegation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ninayozungumzia hapa ambayo ndiyo tulifanyia kazi mwaka 1998 chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa ni dhana ya *decentralization by devolution*. Maana yake ni kwamba tulikuwa tunatakiwa kupeleka *autonomy* kubwa katika halmashauri zetu na kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zinajitegemea kimapato. Malengo yalikuwa ni kwamba ifikapo mwaka 2005 halmashauri zetu tuwe tumeweza kujitegemea kwa angalau kwa asilimia 50 ili tuiipunguzie mzigo Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo mtazamo, mkitaka kumsaidia Mheshimiwa Rais lazima mzi-*empower* halmashauri ziwe na nguvu, ziwe na uwezo wa kujitegemea. Tunapokuwa hapa Bungeni kila mtu anaomba kituo cha afya anamwangalia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kila mtu anaomba zahanati anamwangalia Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Yaani tunaipa Serikali Kuu mzigo mkubwa, lakini tungekuwa tumeitekeleza dhana ya *decentralization by devolution* vizuri kwa maana ya *D by D* leo tungeipunguzia Serikali Kuu mzigo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana yangu, mimi nazungumza kwa nia njema ya kuisaidia Serikali Kuu, maana yake Serikali Kuu inafikiria habari ya reli, Serikali Kuu inafikiria habari ya *Stigler's Gorge*, Serikali Kuu inafikiria habari ya ndege, halafu Serikali Kuu tena ifikirie habari ya zahanati. Leo mtu anakuja kwenye Bunge hili anasifu kujengewa vyoo, sasa

ni vitu ambavyo ni vya halmashauri, ambapo kimsingi halmashauri zilitakiwa kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ndiyo ninachotaka kuwasaidia tu, mimi sina ugomvi kwa uamuzi watakaofanya kwa sababu ndiyo wenye Serikali, lakini mimi nilichokuwa najaribu kusema ni kwamba tukitaka twende vizuri ile dhana ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya kuwa na ugatuaji wa madaraka kwa maana ya *D by D* tuitekelezeni, ina msaada mkubwa sana. Faida yake kubwa ni kama nilivyowaambia, ni kuipunguzia Serikali Kuu mzigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni kupeleka madaraka ya mipango na utekelezaji kwa wananchi wanaopanga mipango hiyo; lakini la tatu ni kufanya halmashauri ziwe na uwezo wa kujitegemea kwa vyanzo vya mapato. Sasa wakivichukua vyanzo vya mapato wakati Serikali Kuu ina vyanzo vingi vya mapato, kwa mfano leo hawajaweza ku-*deploy resource* hiyo kubwa mliyonayo kwenye bandari. Bandari ni sehemu ambayo bado inahitaji kufanyiwa kazi kubwa, *Manpower* ya *TRA* sio kubwa kiasi hicho kwamba mpaka ikakusanye *property tax*, ikakusanye sijui kodi za mabango kwa sababu bado kuna vyanzo vingi hawajavifika. Waache hivi vyanzo vingine, ziwezesheni halmashauri kuwa *naskilled manpower* ya kuweza kuvishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala, bado halmashauri zetu haziwezi ku-*hirena ku-fire*, halmashauri zetu haziojiri na kufukuza, bado mwenye kufukuza ni Serikali Kuu. Ndiyo maana nikasema mpango ule wa ugatuaji madaraka ulikuwa na lengo la kusaidia nchi hii kupunguzia kazi kubwa Serikali Kuu ambayo inafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wajibu wenu kuona inafaa kutekeleza au kuona kwamba sasa mpaka tusubiri kila mtu aje kupiga magoti hapa Bungeni kuomba Serikali Kuu, sawa ila ninachofikiri ni kwamba waziwezeshe halmashauri ziweze kujitegemea kwa maendeleo mapana ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwa Mheshimiwa Waziri, tunakwenda kwenye uchaguzi na kwa hali ilivyo na kwa katiba ilivyo na kwa mwelekeo wa Serikali watakaotumika kwenye uchaguzi ni Wakurugenzi na baadhi ya maafisa wa halmashauri, kama ilivyokawaida kwamba baadae wanajigeuza kuwa *ma-returning officer*. Ninachoshauri kwa sababu tayari kuna kauli ambayo ilikuwa inaleta utata kwamba kuna maelekezo, wale Wakurugenzi watakaokuwa wasimamizi wa uchaguzi lazima watangaze watu fulani kuwa washindi, ni vizuri ofisi ya Mheshimiwa Waziri ijaribu kuwaelekeza Wakurugenzi watakaokuwa *ma-returning officer* watende haki katika uchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokihitaji sisi si nani atakayeshinda, tunachokihitaji sisi ni uchaguzi wa salama na amani utaoisha watu wakashikana mikono, Taifa likabaki salama. Hatuhitaji Taifa hili kwa sababu zozote zile, kwa kisingizio chochote kile liingie kwenye vurugu zisizo za lazima. Kama mtu ana-*deserve* kushinda ashinde, kama mtu ha-*deserve* kushinda ashindwe, lakini siyo kwa sababu anataka kubebwa. Namshauri Mheshimiwa Waziri amshauri Waziri mwenye dhamana kwamba awaambie Wakurugenzi watakapopata nafasi hiyo ya kuapa kuwa wasimamizi wa uchaguzi watende haki, haki ndiyo itakayotamalaki katika Taifa hili. Kama wasipotenda haki wataweka historia ya kuliingiza Taifa hili katika vurugu zisizo za lazimanabahati nzuri na yeye yuko katika nafasi hiyo atajitia doa katika kazi yake kubwa hiyo anayosifiwa kuwa ameifanya. Kwa hiyo ni vizuri na namshauri ndugu yangu aweze kuliangalia hilo katika sura yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, ni suala la *TARURA*; *TARURA* inafanya kazi nzuri sana tatizo ni hili ninalozungumza la sisi kutoziamini halmashauri, kwa sababu *TARURA* inawajibika kwa nani, *TARURA* inafanya kazi katika halmashauri, lakini haiwajibiki kwa Madiwani, haiwajibiki kwa Mkurugenzi. Meneja wa *TARURA* hawezi kufika kwenye halmashauri hata akaweza kuwasiliana na Mkurugenzi, yaani utashi wake kuwasiliana ama kutokuwasiliana. Sasa ni lazima tu-review hii *TARURA*, tuone namna gani Madiwani wataingia,

kama hatuwezi kuingiza Madiwani angalau basi *TARURA* iweze kuwepo kwenye baadhi ya maeneo ambayo kimsingi Madiwani wanaweza wakaweka *inputs* zao na zikaheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Madiwani wakiweka hoja yao yoyote kwa maafisa wa *TARURA* ni utashi wa maafisa wa *TARURA* kukubali ama kukataa. Ni vizuri tujenge mfumo ambao utasababisha Madiwani wetu na Wakurugenzi wetu waweze kushirikiana, *whethermaafisa wa TARURA* wanataka ama hawataki na kuwe na utaratibu ambao utawafanya kisheria washirikishe hawa watu katika maamuzi wanayofanya ili maamuzi yale yawe ni ya watu zaidi kuliko kuwa ni ya watu wachache, maana yake maamuzi ya barabara gani ijengwe, ijengwe vipi, ufanisi wake, ubora wake, bado haijulikani ni nani anayefanya hiyo *check and balance*, katika halmashauri zetu. Kwa hiyo ni vizuri hilo suala liangaliwe katika upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni vizuri tuimarishe Vitengo vyta ukaguzi katika shule za msingi na sekondari. Bado tuna tatizo la ukaguzi wa ubora wa elimu yetu na ndio maana leo tukizungumza habari ya *performance* ya elimu tunazungumza habari ya shule za *private* lakini shule zetu za Serikali bado zinafanya vibaya kwa sababu Kitengo cha Ukaguzi hakijapewa umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ukipe umuhimu sana Kitengo cha Ukaguzi ili ubora wa elimu wa shule za Serikali angalau uwe wa kuvutia na utoe elimu tunayotarajia ili vijana wetu wanapomaliza masomo yao waweze kutumika katika taifa hili kuliko tena kuwa *third class* katika taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba Mheshimiwa Waziri Manispaa ya Moshi tumekuomba muda mrefu suala la Moshi kuwa Jiji. Tunaomba sana suala hilo ulichukue na uendelee kulitafakari ikiwezekana likamilike sasa kwa sababu umelifanyia kazi muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mwita Getere Boniphace atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu na wataalamu wa kale wanavyosema. Yuko mtu mmoja mwanazuoni wa zamani anaitwa Albert Einstein alisema kuna tofauti kubwa sana kati ya ujinga na akili. Akasema akili ina kikomo ila ujinga hauna kikomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu humu wanaomba bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi katika maeneo yao au matatizo yanayogusa wananchi katika maeneo yao, wakizungumzia hoja nzito nzito ziende kurekebishwa na zinarekebishwa kwa fedha lakini ikifika kwenye bajeti ukimwambia unasemaje, anasema hapana. Sasa sijui inakuwaje sielewi, umeomba mradi umezungumza kwa uchungu Serikali inafika kuandaa bajeti ya kukupelekea fedha kwa ajili ya miradi unasema hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri wa TAMISEMI, mnafanya kazi nzuri sana. Kusema kweli kwenye elimu ya msingi sasa kwa jitihada zinazofanyika vijiji, mikakati inayofanyika pale inafurahisha. Nadhani kwenye elimu ya msingi kwa ujumla wake kwa sababu elimu ya msingi Wizara ya Elimu na TAMISEMI wanashirikiana lakini kwa sasa hivi wanafanya kazi nzuri sana. Kwa kweli nawapongeza Waziri, Manaibu wawili, Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi nzuri sana mnayofanya na muendelee kufanya kazi hiyo nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini najiuliza jambo moja sasa tunaenda kumaliza miaka mitano ya uongozi wetu ni

muda wa kufanya tathmini, tunafanya tathmini ya kuangalia elimu bure shilingi bilioni 24 tunazopeleka pale shulenii hivi kweli ziko *viable*. Maana imefika wakati sasa tunapeleka hela mashulenii zinarudi kinyumenyume. Kuna kitu kinaitwa UMITASHUMTA, hela zinakwenda zinarudi zote kwenye upande wa pili kuja kushughulikia michezo. Kwa hiyo, tunaomba hili nalo tuliangalie kwamba linafanyikaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ni muda sasa wa tathmini ili kuona hivi hizi nyumba za walimu tunazojenga *two in one*, sasa hivi tunajenga hizi nyumba kwa ajili ya nini? Tuangalie sasa muundo mpya, nyumba ya mwalimu vyumba viatu (3) na sebule vinatosha. Kwa hiyo, tuangalie namna ya kuwajengea nyumba walimu wetu kwani hali siyo nzuri. Kwa hiyo, hilo nalo tuliangalie liweze kuwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina tatizo la halmashauri, halmashauri yangu ni kama nakaa Morogoro, halmashauri ya Easter Bulaya iko Dodoma, halmashauri ya Lugola iko Singida. Sasa mtu anatoka Morogoro anafika Dodoma anapumzika anakwenda kutafuta huduma za halmashauri Singida, ni jambo baya sana. Walimu wanateseka, watumishi wanateseka, kumhamisha mtoto lazima utumie Sh.30,000 kwenda na kurudi, hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, tuangalie namna ya kufanya kama hatuwezi kupata halmashauri turudisheni mjini ili tuweze kufanya kazi vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wanazungumza habari ya Rais Magufuli, wanazungumza habari nzuri watu wengine hawaelewi kinachofanyika. Nataka niwaeleze kuna Rais mmoja alikuwa pale Marekani anaitwa Franklin Delano Roosevelt, amekaa pale *term nne* lakini amekuwa ni Rais wa 32 kwa maana kwamba kulikuwepo na sheria maalum za Marekani kwamba hakuna atakayeongeza muda wake lakini yule Rais alienda mpaka vipindi vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hapa alichaguliwa 33, 37, 41 na 45 na alikufa ndiyo akachaguliwa Rais mwingine. Walikuwa wana sheria zao za kusema

kwamba hakuna Rais mwingine atakayekuwepo mpaka miaka minne (4) lakini yule miaka mitano (5). Sababu gani ilimfanya aendelee kutawala? Ni kwa sababu uchumi wa Marekani ulikuwa mbaya, *economic crisis* ilitokea na pia wakati huo kulikuwa na Vita ya Pili ya Dunia.

Kwa hiyo, wakaona ili Rais huyu aendelee kutatua matatizo yaliyopo aendelee. Sasa leo tunatengeneza miradi ya *Stiegler's Gorge*, miradi mikubwa ya reli na miradi mikubwa ambayo Rais anaitekeleza, kwa nini tuiseme Rais huyu amalize miradi hii kwa uchumi wa nchi yetu, shida ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini leo tutafute watu wa kula, maana Watanzania tumekuwa na tabia mbaya, tumefika hatua ya kusema sasa acha huyu ale na huyu amechoka, halwezekani. Lazima tuangalle watu wa namna hii wanapatikana. Kuna watu wanaitwa wa *Indigo Children*, wale ni watu ambao Marekani wakiwapata wanawatunza maana wana akili nyngi. Rais Magufuli ameonyesha uwezo wake wa kufikiri ni mkubwa, kwa hiyo, tunaomba tumtunze kwa kadri tunavyoona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Franklin Delano Roosevelt anatawala Marekani kulikuwa na vyama vingi na alitokea chama cha *Democratic* lakini wakati anatawala alikuwa anapata asilimia 85 maana yake *Republican* walikuwa wanamchagua na *Democratic* wanamchagua. Kwa nini CHADEMA chini ya Mheshimiwa Mbewe msikubali kwamba Rais aendelee na sisi turudi humu ndani, shida iko wapi? (*Makofii*)

Mhesimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana sana na niseme tu ukweli kama tungkuwa tunachagua mama wa kupewa tuzo, mama maalum ambaye amejitegemea kwa akili ya kufikiri ningekupa wewe kwani unafanya kazi vizuri sana. Unasimamia ukweli, uko kwenye kufuata haki na Mungu atakusaidia uendelee kuwepo. Wala msigombane, huyu jamaa yetu mwingine utashinda wewe na yeye bado kijana ukija kuchoka utamwachia na yeye aendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza habari ya sekondari, tufanye tathmini sasa kwamba elimu ya msingi na sekondari bure, elimu ya kidato cha tano na sita tunapokwenda kufanya bure, shida iko wapi? Tunapozungumzia elimu maana yake tuzungumzie shule za msingi, sekondari na tunapozungumzia sekondari tunazungumzia kidato cha nne na kidato cha sita. Kwa nini sasa elimu ya sekondari ya kidato cha tano na sita, watoto 260,000 tunashindwa nini kuwapa nafasi wasome bure tubakize vyuo vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nilikuwa nataka nizungumze hayo lakini nawashukuru sana watu wa Wizara ya TAMISEMI wamenisaidia sana kwenye jimbo langu, wamenipendelea sana, nawashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Philip Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso ajiandae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara hii kubwa ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo manne; nitachangia kuhusu pongezi, shukrani, ushauri na muda ukiruhusu nitachangia hoja hii ambayo inajengwa ya makusanyo ya halmashauri kuwa ni vyanzo vichache *vis-a-vis* hela ambazo wanapelekewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la pongezi. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na timu yake; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wamewafanya Watanzania. Watanzania wanafahamu Serikali yetu imefanya mambo gani katika kuwatumikia na zile ahadi ambazo zimeahidiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipite kwenye mambo machache ambayo yamefanywa na Serikali yetu. Jambo la

kwanza, kwa miaka hii minne, *TARURA* imeshatumia zaidi ya shilingi bilioni 799 kutengeneza barabara zetu. Katika muda huu, Serikali yetu sasa inakwenda kutimiza suala la *TASAF* kwa vijiji vyote, hili jambo sio la kupuza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bila ada imetumia zaidi ya shilingi trillioni 1.1 na wanafunzi wetu wanasoma. Wanafunzi zaidi ya 200,000 wameongezeka katika udahili wa kupata elimu baada ya Serikali yetu kuona jinsi gani watoto wetu wasome, siyo jambo la kupuuzwa. Shule zaidi ya 228 katika kipindi hiki cha miaka minne zimeongezeka kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa Tanzania wasome, siyo jambo ka kupuuzwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo zaidi ya 433 vimejengwa, zahanati 368 zimejengwa, upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 92, siyo jambo la kupuuzwa. Ni mambo mengi yamefanyika, mikopo ya vijana, wanawake na wale mavu zaidi ya shilingi bilioni 93 zimetolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali yetu Mheshimiwa Jafo pamoja na timu yake na Naibu Mawaziri, wanafanya kazi kubwa sana. Kaka yangu ninyi hamlali usiku na mchana wanazunguka kwenye vijiji yetu, mitaa yetu, vitongoji zaidi ya 64,000 hawa watu wamefika wanafanya kazi. Kwa hiyo, lazima tuwapongeze, endeleeni kuchapa kazi msisikilize kelele za kuwapoteza njia Watanzania wanawategemea na kazi zenu zinaonekana chapeni kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye shukrani katika bajeti hii. Niishukuru Serikali yetu kwa mambo haya yafuatayo ambayo mnakwenda kuyafanya Babati Mjini. Kwanza, kuna mchangiaji alisema kwamba hakuna fedha za maabara ambazo zimetengwa, Serikali yetu imetenga zaidi ya shilingi bilioni arobaini na mbili na milioni mia tatu thelathini na Babati Mjini tumepata milioni 210 kwa ajili ya maabara na naamini Mheshimiwa Waziri maabara yetu ya

sekondari tunakwenda kuikamilisha, nawashukuru sana.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa fedha za *EP4R* shilingi milioni 400 mmetupatia Babati Mjini, maboma ya madarasa shilingi milioni 150, nikushukuru Mheshimiwa Waziri bajeti iliyopita tuliomba mkatupatia lakini zahanati tatu shilingi milioni 150 Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana. Kulikuwa na ahadi ya Rais, zahanati ya Singe na zahanati zingine sasa zinakwenda kukamilishwa. Nikushukuru katika ujenzi wa hospitali za wilaya 27 zaidi ya shilingi bilioni 27 mlizotenga na hospitali yetu ya Wilaya Babati mmeikumbuka. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nishukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri kutuingiza tena kwenye mpango huu mpya wa ujenzi wa barabara za lami mmetupatia kilometra 35 za lami Mji wa Babati. Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana sana na wanababati wanafahamu hili. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nishukuru Serikali kwa kuingiza mpango wa tauzo za kike kwa watoto wetu wa kike wapatiwe kupitia *own source* na maelekezo yametoka. Kamati yetu ya TAMISEMI wamesema kwamba imepokelewa itatekelezwa kwenye mikoa. Hii hoja Serikali yetu imepokea vizuri na inakwenda kutekelezwa. Ilikuwa inajulikana ni hoja ya mtu fulani lakini Serikali hongereni kwa kuipokea hii hoja tauzo za kike zinakwenda kupatikana kwa watoto wetu. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri mambo yafuatayo kwa Serikali yangu. Naomba muangalie mfumo huu wa *Prime Vegar System* wa upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu kwamba hospitali inapokuwa imeishiwa inakwenda kununua kwenye maduka binafsi. Tunafahamu kwamba tuna asilimia 60 ya wamama wajawazito, watoto na wazee tumewapa *exemption* lakini sasa tunapokuwa tunawaachia wakanunue kwa fedha zao kwenye maduka binafsi inaweza ikawa wanapunguziwa na hii asilimia 60 ya wale ambao tumewapa msamaha. Naomba hili ultizame Mheshimiwa Waziri. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili naomba ultizame hili la mikopo ya asilimia 10 wazee waingizwe sasa. Walemavu, akina mama na vijana tayari, nikuombe kaka yangu na wazee sasa waingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinii nikuombe pia kwenye miradi ya kimkakati, sisi Mji wa Babati mmetuingiza kwenye miradi ya kimkakati, niwashukuru. Kwa upande wetu tuna mradi wa stendi. Kwenye ile miradi 38 niombe sasa ule mradi wetu wa stendi uweze kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili la *TARURA*, nafahamu mmetenga shilingi bilioni 275, Serikali yetu hongereni sana. Niwaombe sana tuwaongezee *TARURA* fedha kwa sababu hali si nzuri kwenye barabara zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kushauri ni malipo ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji litizame. Nipongeze posho za Madiwani mmeji-*commit* kwenye taarifa yenu kwamba mnaenda kulipa, naomba muangalie sasa Wenyeviti pia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni hili la makusanyo. Naomba tusiwe tunadanganya. Wizara hii ni kubwa, ina bajeti ya zaidi ya shilingi trillioni 7 lakini TAMISEMI inakusanya shilingi bilioni 814, Serikali inawapeleka shilingi trillioni 7. Kuna watu wanasema vyanzo vyao vimechukuliwa lakini wao wanakusanya shilingi bilioni 814 wanaletewa shilingi trillioni 7. Kwenye maendeleo TAMISEMI wanapelekewa zaidi ya shilingi bilioni 2 wakati makusanyo ya halmashauri ni shilingi bilioni 814. Ileweke tu wazi kwamba Serikali ina nia njema, tusipotoshe kwamba halmashauri vyanzo vimeondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walivyokuwa wanakusanya walikuwa wanatumiae? Leo maboma, maabara na zahanati tunapata. Wao wanakusanya sijui bilioni ngapi halafu tunawapelekea zaidi ya shilingi trillioni 7. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda wangu umeisha, naomba niunge mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Muda mrefu sijamwona Mheshimiwa Dkt. Mpango akitabasamu lakini naona amefurahi.

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Hasna Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mheshimiwa Gerson Hosea Lwenge ajiandae.

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa muda wangu ni mdogo, naomba nianze kwanza na changamoto ambazo ninazo ndani ya Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kutokana na ile hoja ya mgawanyo kwenye pesa za maendeleo zinazotakiwa kwenda Jimbo la Kigoma Kusini ni kubwa sana, tunaomba tuongezewe pesa kwenye TARURA. Tunayo barabara ya kutoka Rukoma kwenda Kalilani ni muhimu sana. Barabara hii ndio itaunganisha kwenye Bandari ya Lagos ambayo itatumia shilingi bilioni 12 ujenzi ukikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunayo barabara ya Mganza - Ilalanguru ina tatizo kubwa. Tunayo barabara ya Itegula - Katumba; Kufubu - Ubanda; Kaliasi - Bwesa. Mheshimiwa Waziri naomba tuongezewe pesa kwenye TARURA ili tuweze kurekebisha barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nizungumzie changamoto niliyonayo ndani ya sekta ya afya. Tunacho Kituo cha Kazoramimba wananchi pamoja na Mfuko wa Jimbo tumeweka jitihada za ujenzi. Pia tunacho Kituo cha Afya cha Kabeba ambacho tulishaleta ombi TAMISEMI ili tuweze kupatiwa shilingi milioni 800 ambapo shilingi milioni 400 ni kwa ajili ya Kazoramimba na shilingi milioni 400 Kituo cha Kabeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna uhaba mkubwa wa nyumba za watumishi na watumishi wa idara ya afya na elimu. Ninayo changamoto kubwa kwenye Shule ya Sekondari ya Nyangabo na Shule ya Sekondari ya Sigunga tumewahi kuleta maombi na umenipokea. Naomba Mheshimiwa Waziri utuangalie kwa jicho la huruma, tupate pesa hizi sekondari mbili ziweze kukamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna changamoto kubwa sana ya watumishi kupandishwa madaraja kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya changamoto hizo za harakaharaka, niende sasa kwenye shukrani. Mimi ni Mbunge mwanamke ndani ya Jimbo la Kigoma Kusini lakini tunafahamu humu ndani tunao Wabunge 25 wa majimbo kwa maana Wabunge 19 kwenye Chama cha Mapinduzi lakini Wabunge kama 5 au 6 kutoka Upinzani. Tunafanya kazi nzuri sana, tunatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kama mlezi wetu wa chama ndani ya Mkoa wa Kigoma. Pia nikushukuru sana mdogo wangu Mheshimiwa Jafo kwa mambo mazuri uliyotekeleza ndani ya Jimbo la Kigoma Kusini. Umeweza kunipatia pesa shilingi milioni 140 kwenye shule mpya ya Mwakisega, umenipatia shilingi milioni 72 kwenye shule mpya ya Sekondari ya Basanza na umenipatia shilingi milioni 370 kwa ajili ya kuendeleza madarasa mbalimbali kwenye shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, mimi nimeingia kwenye jimbo kwenye vijiji 61 hakuna umeme hata kijiji kimoja. Leo tunavyoongea vijiji 15 vina umeme. Hata Nguruka ambayo ilikuwa haitegemei kuwashwa umeme, umewashwa. Wananchi wa Ukanda wa Ziwa walikuwa wanatumia maboti, walikuwa wanatumia meli ya Liemba, leo barabara ya kilometra 250 kutoka Simbo mpaka Kalya,

Mheshimiwa Rais amemwaga mapesa mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, tunavyoongea ninayo Bandari ya Sibwesa imekamilika, ninayo Bandari ya Lagosa ina asilimia 75, ninayo barabara ya kutoka Uvinza mpaka Malagarasi, tayari tenda imetangazwa, wakati wowote ujenzi unaendelea. Jimbo linameremeta namna hii! Nani kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha nini? Inaonesha kwamba kama kwa miaka 40 lile jimbo lilikuwa linaongozwa na wanaume, walikuwa hawawezi kuiomba Serikali, mwanamke amechukua miaka minne, kapiga magoti kwenye Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi, leo jimbo mambo ni ng'aring'ari. Miradi sita ya maji yote inatoa maji; Mradi wa Nguruka, Mradi wa Uvinza, Mradi wa Kandaga, Mradi wa Ilagala na Mradi wa Kalya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais akasema hapana, mama anafanya sana, pelekeni pesa mradi mkubwa wa maji Mwakizega. Leo Mradi wa Mwakizega unatekelezwa. Kwa kweli Jimbo la Kigoma Kusini Mheshimiwa Rais na Serikali imetenda haki sana. Wanachotakiwa wananchi kumlipa Rais ni kumpigia tu kura asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakuombea dua kule Mbeya ukashinde vizuri. Nakuombea dua kwa sababu wanawake wanaweza. Leo kwenye majimbo 214, ni majimbo 25 tu yanayotawaliwa na wanawake, lakini mwanamke anaweza kubeba mtoto tumboni kwa miezi tisa, ananyonyesha, anamkuza mpaka anakua, kwa nini ashindwe kuongoza jimbo? (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake tuna uwezo mkubwa na ile dhana ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba asilimia 50 kwa 50 inapatikana, nawaomba wanawake mjiamini. Mnaoweza kwenda kwenye majimbo, nendeni, tuko imara. Nimeona hili niliseme kwa kujiamini

kabisa. Kama mwanamke anaiangalia nyumba haitetereki, anashindwaje kuwaangalia wananchi? Anashindwaje kusimamia miradi ya utekelezaji? Anashindwaje mwanamke? Nani kama mwanamke jamanii? (*Vigelegele/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Hamna! (*Makofi*)

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na la mwisho. Mawaziri wanaume msinichukie; Mheshimiwa Jafo usinichukie, lete pesa jimboni kwangu. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Pokea zawadi kwanza.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala moja la ugawaji wa majimbo.

MBUNGE FULANI: Pokea, pokea.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala moja la ugawaji wa majimbo. Nimeona kwenye ratiba ya Tume ya Uchaguzi kwamba mwisho wa kuwasilisha vijiji, kata na majimbo ni tarehe 28 mwezi huu.

Namwomba sana kaka yangu, Mheshimiwa Jafo, Jimbo la Kigoma Kusini liko kwenye mchakato wa kugawika tangu 2010. Ni jimbo kubwa, mwenyewe umekuja, umeona. Sasa naomba sana kama inawezekana ligawike, kama haiwezekani acha, mwanamke naendelea kudunda, utaligawa 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya nami nataka niseme uongozi ni *confidence*. Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli ana *confidence*, alikuwa na malengo akasema nitasimamia rushwa, nitasimamia maendeleo, miradi mikubwa ya kimkakati tumeiona na miradi ya vielelezo tumeiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hasna Mwilima. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge; nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Gerson Hosea Lwenge atafuatia, halafu Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, ajiandae.

MHE. SELEMANI M. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa mionganini mwa wachangiaji kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuwatumikia wananchi wake. Pia tuwapongeze wasaldizi wake; Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa sana zinazofanywa na Serikali kwa ujumla katika kupeleka maendeleo, hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Vile vile nawapongeza Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu ambao wanamsaidia katika kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanywa na Serikali ni nydingi na zinaonekana. Natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutoa fedha nydingi kwenye jimbo langu. Fedha hizo zipo kwenye maeneo ya utawala ambapo kumejengwa majengo mengi ya Halmashauri ya Wilaya ambapo tulipewa na Serikali shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namkumbusha tu Mheshimiwa Waziri awe na kumbukumbu, kwenye eneo lile Mheshimiwa Rais aliahidi kutupa shilingi bilioni moja kumalizia lile jengo. Namwomba aweze kukamilisha ile ahadi ya Mheshimiwa Rais ili jengo lile liweze kukamilika na watumishi waweze kupata nafasi ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kutoa shukrani za dhati kwake yeye na Serikali kwa ujumla. Serikali ilitoa Vituo vya Afya viwili; Kituo cha Mishamo na Kituo cha Mwesi. Vituo vile vimekamilika na wananchi wameweza kunufaika. Tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo Kituo cha Afya cha Mnyagala ambacho Waziri alitoa fedha kuwapelekea wananchi wa Kituo cha Afya cha Mnyagala, shilingi milioni 200. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na jitihada nzuri ulizozifanya, zile fedha zilienda kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Mheshimiwa Waziri ashughulikie hizo fedha ziweze kufika kwa wananchi ambaa walijiandaa, wamejipanga kwa ajili ya kutekeleza Kituo kile cha Afya cha Mnyagala. Ninajua hilo alishalfanyila kazi, lakini natoa msisitizo ili aweze kusukuma hizo fedha zitoke kwenye Manispaa ya Mpanda ziende Wilaya ya Tanganyika ambako ndiko kulikolengwa hizo fedha zikafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwani kwenye Sekta ya Elimu imetoa fedha nyngi sana. Mimi ni mionganoni mwa watu ambaa wamenufaika. Kuna mchangiaji mmoja ambaye alikuwa anasema kwamba Serikali hajatoa fedha kwenye maboma, lakini jimbo langu limepewa fedha nyngi; kwenye Sekta ya Elimu tumeputa karibu shilingi bilioni mbili zikiwemo ambazo zimesaidia kukamilisha maboma ya Shule ya Sekondari ya Ilango, shilingi milioni 127; Shule ya Sekondari ya Mishamo shilingi milioni 60; Bulamata shilingi milioni 60; Shule ya Mpanandogo shilingi milioni 86, Shule ya Kasekese shilingi milioni 80. Kwa hiyo, ni fedha nyngi ambazo zimetolewa kwenye Sekta ya Elimu, elimu msingi na elimu sekondari. Tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba zipo changamoto ambazo zipo kwenye maeneo ya elimu, tunaendelea kuiomba Serikali waendelee kuwasaidia wananchi kwenye maeneo ambayo wameandaa hayo maboma. Mwaka huu viro vijiji ambavyo vimejipanga,

tunaomba Serikali itusaidie Shule ya Msingi ya Igulala, Shule ya Sekondari ya Tongwe ambayo inaomba mabweni na tumeshaomba Serikalini, naamini Serikali itafanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaiomba Serikali ni eneo la *TARURA*. *TARURA* wamefanya kazi nzuri, lakini fedha ambazo zimetolewa hazitoshi kwa sababu miundombinu ya wilaya yangu ni mingi na mikubwa ambayo inahitaji fedha za kutosha ili ziweze kunufaisha wananchi. Ipo barabara ya Kijiji cha Kabage ambako kuna uzalishaji mkubwa wa chakula, tunaomba hii barabara uifanyie kazi utusaidie tupate fedha za kukamilisha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Itunya toka Kapalamsenga, tunaomba tusaidiwe kwenye eneo hilo, tutengewe fedha; na maeneo ya Mishamo ambayo yana wakazi zaidi ya 60,000 ambako kuna miundombinu ya barabara iliyoharibika kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kwenye eneo hilo mmetusaidia sana, tumejenga hospitali nzuri na Mheshimiwa Waziri ameishuhudia, lakini kilio chetu, tunaomba wakamilishe yale ambayo yanahitaji kufanya ili hospitali iweze kufanya kazi. Serikali imetoa fedha nydingi eneo lile, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, atenje fedha na alete watumishi wa kutosha kwenye Hospitali ya Wilaya na Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa ili wananchi waweze kunufaika na msaada uliotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kwenye eneo la *TASAF*; Serikali imeendelea kutusaidia, lakini kwenye bajeti hii nimeona kuna maeneo ambayo mmeamua sasa kupeleka huduma ya *TASAF* kwenye vijiji vyote. Naomba sana hili mlifanyie kazi. Hakikisheni mnapeleka fedha kwenye maeneo ya vijiji vyote ili kutoa ile sintofahamu ambayo wananchi wa baadhi ya vijiji vingine wanaona kwamba wanabaguliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali, tunaipongeza Wizara kwa ujumla kwa kazi kubwa ambayo imefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Gerson Hosea Lwenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii na pia kwa kutulinda na kutupa uhai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimpongeze sana Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli. Wengi walikuwa na mashaka naye walivyompa Urais, lakini amefanya mambo mengi ambayo yalioneckana kwamba ni magumu hayawezekani, lakini ndani ya miaka hii minne, mitano ameweza kufanya mambo yale magumu na yamewezeckana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme machache tu, kama sita. Kutoa elimu bila ada, ni kitu ambacho kwa kweli amekifanya na kinaendelea kufanyika. Kufufua Shirika la Ndege, ujenzi wa reli ya kati, ujenzi wa bwawa la Nyerere, kuhamia Dodoma, kujenga Vituo vya Afya 433 katika muda mfupi, Hospitali za Wilaya 98, zahanati 368 na upatikanaji wa dawa kuongezeka mpaka kufikia asilima 92. Hivi vyote ni vigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote magumu kitu cha kwanza, anamtanguliza Mungu mbele na siku zote amekuwa anasema Watanzania tufanye kazi kwa bidii, lakini tumweke Mungu mbele. Kwa hiyo, naamini kwamba mafanikio yote haya anayofanikiwa ni kwa sababu anamweka Mungu mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika janga hili la *Corona*, ni wazi kabisa wengi wanamshangaa, wanaona Tanzania kama mbona sisi hatulioni, lakini ndugu zangu bila Mungu haiwezi kufanikiwa. Kuna mahali tumefanya makosa wananchi, Watanzania na dunia nzima tumemkosea Mungu, likaletwa hili Gonjwa la *Corona*. Sasa jibu liko katika kumtegemea Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wale ambao wanajua injili wakasome Mambo ya Nyakati wa Pili kuanzia Mlango wa 7:12-13. Mungu anasema kwamba ametakasa nyumba ya ibada. Kwa hiyo, hawezekani useme nitasali nikiwa nyumbani na Mungu atasikia. Anasema watu wakienda kwenye nyumba ya ibada, wakamlilia atasikia sala zao. Kwa hiyo, Rais wetu ameruhusu ibada iendelee kwa imani tofauti; Waislamu nao waende Msikitini wakaombe Mungu aondoe janga hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, naomba sana ndugu zangu Watanzania tuchukue hatua. Mungu pia anachuia ulegevu. Lazima tufanye bidii katika kujikinga na gonjwa hili. Wataalam wanaelekeza kila mahali. Naomba sana wataalam wetu washuke mpaka vijijini. Huku mjini tumeshaelewa *Corona* ni nini; tunanawa mikono, tunajitakasa na hivi vitakasa mikono, lakini vijijini kule bado hili somo halijafika. Sasa ugonjwa utakapofika maeneo yale tutakufa kama kideri cha kuku. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu kwa kweli tumpe *big up* Mheshimiwa Rais wetu kwa hatua ambayo amechukua kwa maendeleo haya pamoja na namna anavyopambana na tatizo hili la *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe ambayo mimi nawakilisha, Mheshimiwa Rais wetu alikuja kututembelea mwezi Aprili mwaka 2019. Sisi yale ambayo aliahidi kwetu, kwanza ilikuwa kutujengea lami toka Njombe mpaka Makete. Kazi inaendelea, lami imeshamwagwa zaidi ya nusu ya ile barabara. Kutujengea lami kutoka pale Njombe kuja Igando kazi imeshaanza, inaendelea.

Mheshimiwa Niabu Spika, jambo lingine ambalo alituahidi ni kutuletea umeme. Mpaka sasa vijiji 92 kati ya 108 vimeshapata umeme. La tatu, lilikuwa ni suala la maji, tayari ameshatenga shilingi bilioni 80 kwa ajili ya kutupatia maji. Kwa hiyo, tulimwambia kwamba kwa haya yote ambayo umeyafanya na yale unayofanya kwa Taifa zima, sisi Wanging'ombe usije kuomba kura, sisi kura tumeshampa Rais wetu. Naomba na Watanzania wengine kwa haya makubwa ambayo tulifikiri hayawezekani yamewezekana, tumpe kura za ushindi bila shaka, hata vyama vya upinzani kwenye urais naona mwachieni Mheshimiwa Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri wetu, Mheshimiwa Jafo. Amekuja Wanging'ombe takribani mara tatu katika kuhamasisha maendeleo. Tumepata Vituo vitatu vya Afya, Tarafa ya Wanging'ombe, Tarafa ya Mdandu na Tarafa ya Makoga. Kile Kituo cha Makoga wametoa shilingi milioni 200, naomba tupate shilingi milioni 200 tukikamilishe kile kituo ili kila Tarafa iweze kuwa na Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru pia tumepata fedha za kujenga Hospitali ya Wilaya. Nimeona kwenye bajeti tumeongezewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga wodi tatu. Tunashukuru sana Mheshimiwa Jafo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la TARURA. Ndugu zangu mwaka huu tumepata mvua nyngi sana, ninajua kabisa zimetengwa shilingi bilioni 275. Ninachoomba ni kwamba katika hizo fedha, kwanza ifanyike tathmini ya kutosha ya athari za hii dharura. Barabara nyngi hazipitiki. Jimboni kwangu madaraja matatu yamekwenda na maji na mito imekwenda ukubwa zaidi ya mara tatu. Sasa wakienda na utaratibu wa bajeti ile ya kawaida nina hakika haitawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 tulikuwa na bajeti ya shilingi 1,100,000,000/=, mwaka huu athari hii ya mafuriko inahitajika shilingi bilioni 1.7. Ina maana kwamba hata ile fedha ya bajeti ya mwaka 2019 ikitolewa bado

barabara hizi hazitafunguliwa. Tulishapata maendeleo mazuri na wananchi wanaishukuru sana Serikali. Kwa hiyo, naomba sana katika hiyo bajeti kwanza zitengwe fedha za kurekebisha miundombinu iliopata athari za mafuriko halafu ndiyo iende mipango ile ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tatizo la fedha lipo na ili tuweze kukamilisha miradi yote hii, kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, naishauri sana Serikali kwamba tushughulikie kwanza suala la mafuriko halafu fedha zitakazobaki twende kwenye yale matengenezo ambayo ni ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka pia nichangie linahusiana na masuala ya huduma za afya. Ninajua kabisa tumejenga Vituo vya Afya, vinapendeza sana, lakini tusipoweka fedha ya matengenezo; yaani Vituo vya Afya vinahitaji tuwe na hela za kufanya ile miundombinu kila siku iwe inapendeza. Kwa hiyo, naomba sana fedha ya matengenezo tuiweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga miradi mingi lakini huwa tunasahau kuweka fedha za matengenezo. Sasa naomba sana Mheshimiwa Jafo jambo hili mliangalie. Tumefanikiwa, tumejenga majengo mengi kwenye idara ya elimu na maeneo mengine, lakini fedha ya matengenezo inakuwa hakuna. Naomba sana suala hili mliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Wilaya yangu ya Wanging'ombe pale kuna nyumba ya Afisa Tawala pamoa na maafisa wengine mbili. Toka mwaka 2013 zile nyumba bado hazijakamilishwa na wakati huo zilikuwa zinajengwa na hili Shirika la *TBA*. Najua urasimu wa *TBA* umefanya yale majengo mpaka leo hayajakamilika.

Naomba mwangalie namna bora zaidi, hata ikiwezekana fedha ziitolewe zikamalizie majengo yale kwa kutumia *force account* ili watumishi wetu waweze kupata mahali pa kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda hautoshi, naunga mkono hoja hii na ninampongeza sana Waziri pamoja na Serikali yote kwa utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama na kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Chemba. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Waziri wa Wizara hii ya TAMISEMI, Dkt. John Pombe Magufuli, Waziri Jafo na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Spika, kwa kutuongoza sisi vizuri ndani ya Bunge lako hili kwa kipindi hiki tunachomalizia muda wetu wa miaka mitano. Na niwaombee nyote wawili katika azma yenu na nia njema milyonayo ya kuwatumikia Watanzania, Mheshimiwa Spika kule Kongwa na wewe kule Mbeya unakoomba na sisi wajukuu wa mtume tutaomba dua zetu ushinde kwa kishindo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili uniruhusu nishukuru sana Shirika la *Human Bridge* la Sweden kwakutupatia vifaa vya zaidi ya shilingi milioni 500 vya afya kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Vifaa hivyo vimefika na tunafanya utaratibu sasa wa kuvigawa kwenye vituo vinane vya afya katika wilaya yetu pamoja na zahanati zilizopo katika Wilaya ya Chemba, ni vifaa vya kisasa kabisa kwa kweli, mtu akilazwa kwenye vitanda vile anaweza hata asiondoke hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chemba, kilichobaki sasa ni kumalizia na nimeona kwenye baeti ya mwaka huu wametenga karibu tena *1.5 billion* kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa hospitali ile. Tumejenga vituo vitatu vya afya Mrijo, Hamai na Kwamtoro. Ni mafanikio makubwa sana kwenye Wilaya mpya ile ya Chemba na kwa kweli, kwenye afya tuko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niipongeze sana Serikali kwenye suala la elimu, tumejitahidi sana. Leo tunajenga mabweni Shule ya Sekondari ya Kwamtoro, Mrijo, tumefanya maandalizi kwa ajili ya shule ya Sekondari Sanzawa, Kuriotae, hali kadhalika Ovada, Msakwalo pale, Farkwa tayari na tunajiandaa pia kujenga kule Mpendo. Tuna changamoto kubwa sana katika ile Kata ya Mpendo kwa sababu, ule Mto Bubu kuanzia mwezi wa 11 wanafunzi wanaotoka vijiji vya Hamia hawaendi shulenii kwa sababu mto ule unakuwa umejaa na hawana uwezo wa kuvuka tena, lakini tunashukuru Serikali kwa kutuahidi kwamba, itajenga mabweni pale ya wavulana na wasichana kwa hiyo, tutakuwa tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua zilizonyesha mwaka huu ni kubwa mno, barabara nydingi zimeharibika katika maeneo *almost* karibu Tanzania nzima. Niiombe Wizara, niiombe Serikali iharakishe kupeleka pesa kwa ajili ya watu wa *TARURA* ili kukamilisha barabara hizo na hata kwa *TANROADS* vilevile. Leo mawasiliano kati ya Dodoma na Kwamtoro yamefungwa karibu miezi miwili, Mto Bubu umejaa pale Bubutole na Mombosya, hakuna anayeweza kuvuka na barabara pale madaraja yale maji yanapita ju. Barabara za kutoka Chemba kwenda Jangalo, kwenda Farkwa, kwenda Sanzawa zipo katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bure, tumefanikiwa sana kwenye elimu bure, lakini nitoe ushauri tu. Tunatoa elimu bure, tunapeleka fedha moja kwa moja kule shulenii, nani ana-*monitor* hizi fedha kama zinatumika vizuri? Hili ni eneo

ambalo tunahitaji kufanya tathmini ya kutosha kama Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili kwenye utawala bora. Katikati hapa tuliongeza sana maeneo ya utawala na tukaongeza sana hata maeneo ya Madiwani. Chukua *case study* ndogo ya Gairo, mapato yanayopatikana pale kwenye Halmashauri ya Gairo ni machache mno, kuwalipa madiwani imekuwa ni ngumu ni kwa sababu, tulijiongeza maeneo ya utawala bila kufanya tathmini ya kutosha, Waingereza wanaita *elite positions*, una-create eneo ili fulani awe kiongozi, lakini bila kujuu atalipwa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili eneo tuliangalie vizuri. Nimesikia hata hapa Mheshimiwa Mwilima anazungumza kuhusu kugawa majimbo, kuongeza majimbo; nilidhani ipo haja ya kupunguza majimbo. Kama tunafanya tathmini ya kutosha na tuna malengo mazuri na Taifa hili, tuna halmashauri 185 ni vema kila halmashauri ikawa na Mbunge mmoja badala ya halmashauri moja ina Wabunge wanne, watano, hii ndio tunaita *elite position*. Unatengeneza eneo ili fulani awe kiongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika kuongeza maeneo ya utawala, hili amelisimamia vizuri sana. Ni jukumu sasa la Serikali na Tume ya Uchaguzi kuangalia kwamba, hivi mtu mmoja ana kata 26 pale Chemba, mwingine ana kata 6, mwingine ana kata 7, halafu wote mna haki sawa. Eeh! Majimbo mengi yaligawanywa kisiasa, kata nyingi ziligawanywa kisiasa, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli hili amelisimamia vizuri sana ndio maana haukuona hata dalili ya kuongeza kata, wilaya, mikoa, hili kwa kweli, mimi nampongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa mwisho, miradi ya kimkakati. Katika ngumi kuna viwango, kuna *heavy weight*, kuna *light middle*, sasa haiwezekani mtu wa *heavy weight* akapigana ngumi ulingoni na mtu wa *light weight*. Sasa leo kwenye miradi ya kimkakati mnashindanisha

halmashauri na majiji, kwa vyovyote vile halmashauri hazitashinda, majiji ya *resources* kubwa, yana vitu vingi ndio maana hata kwenye mapato yanayochangiwa Serikalini halmashauri zinatoa kidogo. Kwa hiyo, ushauri wangu nimalizie kwa kuomba Halmashauri zishindanishwe kwa Halmashauri n majiji yashindanishwe kwa majiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho fanyeni tathmini ya *force account* kwenye miradi tunayoitekeleza. *Force account* ni *program* nzuri, lakini nina wasiwasi kwa sababu, halmashauri nyingi zinakotekelezwa miradi hii inayotumia *force account* hazina wataalam wa kutosha. Hatuna mainjinjina huko halmashauri ndio maana unakwenda unakuta jengo limejengwa ukiangalia upande huu limepinda, upande huu limeenda songombingo ni kwa sababu ya matumizi ya hii *force account*. Na nina wasiwasi mkubwa...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kunijalia afya na kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niunge mkono hoja hii na ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Niwapongeze wasaidizi wake, nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, hongereni sana kwa jinsi mnavyofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama kwa ajili ya kutoa shukrani. Mkoa wa Kigoma ni kati ya mikoa ambayo imekuwa nyuma kwa muda mrefu, lakini nafurahi sana kusema sasa Kigoma ni mwanzo wa fursa. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutujengea barabara ya Kidahwe – Kasulu na tarehe 21 mwezi wa tatu Serikali ilisaini ujenzi wa Barabara ya Kabingo – Kasulu mpaka Buhigwe kwa kiwango cha lami. Kwa sasa hivi Mkoa wa Kigoma tangu hiyo tarehe 21 walipoweka saini kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kabingo – Kasulu mpaka Buhigwe hii ndio habari ya Mjini, Mjini Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hiyo wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma macho yao yalikuwa kwenye vyombo vya habari kuangalia historia inavyoandikwa ndani ya Mkoa wa Kigoma. Tunamshukuru sana Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuweza kutujengea barabara hiyo ambayo itaunganisha mikoa na nchi za nje, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunamshukuru sana kwa ununuaji wa ndege. Sasa hivi ndege za ATC zinatua kila siku ndani ya Mkoa wa Kigoma, watalii wanaingia kila siku, pesa za kigeni zinaingia na pato la Taifa linaendelea kukuzwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika afya. Nimeangalia katika kitabu cha Waziri, jumla ya vituo 434 vimejengwa, Mkoa wa Kigoma tumeweza kupatiwa vituo 20 vilivyojengwa na vingine vilivyokarabatiwa. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, wanawake wa Mkoa wa Kigoma wanshukuru sana. Sasahivi wanawake wanapatya huduma kwenye vituo vya afya, hawapotezi mara kwa mara maisha kutohana na umwagaji wa damu pale wanapokuwa wameenda kujifungua kwa sababu, huduma zimewasogelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, tuna kila sababu ya kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendelea kuwajali wanawake, watoto na wazee, huduma

zimesogezwa hapo. Siku za nyuma watu walikuwa wanapoteza maisha kutokana na ukosefu wa vituo vyatya afya kwa sababu, walikuwa wanasafiri umbali mrefusana kwenda kutibiwa na kukosa huduma kwa mfano za uongezaji wa damu pale wanapokuwa wamepungukiwa na damu, lakini kwa sasa hivi vituo hivyo 20 vilivyomo ndani ya Mkoa wa Kigoma na vingine ambavyo vinaendelea kujengwa kwa kweli, Serikali ya Awamu ya Tano ina kila sababu ya kusifiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi wanawake wa Mkoa wa Kigoma na Wananchi wa Mkoa wa Kigoma shukrani zetu mtaziona mwezi wa 10. Wamesema nenda ukaseme shukrani zetu utaziona mwezi wa 10, tutampigia Mheshimiwa Rais kura nyngi za kutosha kwa sababu ameufanya Mkoa wa Kigoma uweze kutambulika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme katika llani ya CCM, ukurasa wa 116 mpaka 17 uwezeshaji wa wanawake kiuchumi pamoja na vijana. Katika llani hii imetekelzeza na wanawake wameweza kuanzisha vikundi vingi sana na ninaishukuru Serikali kwa kuweza kutekeleza ahadi hii, halmashauri nyngi zimeweza kutoa asilimia 10 kwa wanawake na vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, naomba Halmashauri zile ambazo hajizjaweza kutoa pesa hizo ziweze kutoa na zile ambazo zimetoa kiwango kidogo ziweze kuongeza kiwango. Kwa mfano badala ya kutoa milioni moja au milioni mbili waanze sasa kutoa kuanzia milioni tatu, milioni tano na kuendelea, ili wanawake waweze kufanya vizuri katika ujasiriamali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu vilevile, elimu bure. Nimeshukudia kabisa katika mkoa wetu watoto wengi wameweza kwenda shule kwa sababu, tangu Rais wetu aliposema watoto watapatiwa elimu bure, hata wale amba walikuwa hawana uwezo wa kwenda shulenii sasa wanaweza kupelekwa shule, watoto wanasona, watoto wameitikia wito huo, wazazi wamewapeleka shule. Niishukuru Serikali

imeweza kujenga shule za msingi zile ambazo zilikuwa nyingine hazina pesa zimeweza kukarabatiwa na watoto wanasoma shule, na niishukuru Serikali tunajengewa sasa shule ya VETA katika Kijiji cha Nyumbigwa, Wilaya ya Kasulu. Shukrani zangu hizi kwa Mheshimiwa Jafo. Siwezi kumsahau Profesa Ndalichakokwa sababu, naye amekuwa akishirikiana naye katika kutusaidia katika ujenzi wa shule hizi za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niseme tena ninawapongeza Mawaziri wote wakiongozwa na Waziri Mkuu, mara nyingi wamekuwa wakifika Mkoani kwetu Kigoma. Na nimshukuru Waziri Mkuu kwa kuweza kufika Kigoma kuhamasisha zao la mchikichi na ninaomba nimwambie kazi yake imeanza kuzaa matunda, Wananchi sasa wanachukua mbegu za michikichi kwenda kupanda kwenye mashamba yao. Niwaombe wakurugenzi waweze kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kupeleka mbegu katika vijiji vile ambavyo tayari vinahitajika kuanza kupanda michikichi, ili waweze kuunga juhudzi za Mheshimiwa wazii Mkuu. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Stanslaus Shingoma Mabula ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza niungane na wenzangu katika kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye ametujalia afya njema na kuweza kukutana na kuendelea na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili nitoe tu pole kwa Chama changu Cha Wananchi – CUF kwa kuondokewa na aliyekuwa Katibu wetu Mkuu, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ambaye alikuwa ni Mbunge wa Gando kwa takribani vipindi vinne. Kwa hiyo, natoa pole hizo pia kwa Bunge kwasababu, naye alikuwa ni Mbunge na ameshiriki sana

katika shughuli za Bunge letu kwa muda wa miaka 20.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kutoa pole hizo, nianze kuchangia kama ifuatavyo; tunazo Serikali za aina mbili, tuna *Central Government* yaani Serikali Kuu. Lakini pia tunazo *Local Government* ambazo ni Serikali za Mitaa au Serikali za wenyeji. Serikali hizi za Mitaa kwa kweli ndizo ambazo zipo karibu na wananchi, zinafanya majukumu mengi, zinafanya shughuli nyinyi za kuwahudumia wananchi pamoja na majukumu yake ya kwamba, ya kukusanya kodi, lakini pia kutoa huduma, lakini pia zimekuwa zikitengeneza ajira kwa wananchi wetu, hususan katika shughuli mbalimbali za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jafo kwa namna ambavyo ameweza kuitumia vizuri Wizara hii ya TAMISEMI. Pamoja na kwamba, zimekuwepo kasoro ndogondogo, lakini sitaacha kumpongeza isipokuwa tu nimuombe, kama alivyoomba Mheshimiwa Jafari hapa kwamba, haya yaliyopita ya Serikali za Mitaa sote tunajua nini kilifanyika na hususan katika halmashauri yangu tuliathirika sana na hususan katika kipindi hiki cha gonjwa la corona ambalo tunatakiwa tuwe na umoja wa Kitaifa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale ambapo hata iliyosomwa bajeti ya Waziri Mkuu na kusema kwamba, Serikali za Mitaa CCM wameshinda kwa kishindo kwa kweli, wapo watu ambao ukisema maneno hayo yanawauma; sasa hofu yangu wasije kukerwa kwao wakaacha kutoa ushirikiano katika kipindi hiki kigumu cha mpito cha gonjwa hili la corona. Kwa hiyo, niseme tu namuomba Mheshimiwa Jafo Uchaguzi Mkuu unapokuja basi yasije yakatokea kama yaliyokuwakatika Serikali za mitaa. Tukikumbuka hapa sisi tumeapa kila mmoja kwa imani ya dini yake, tupo tuliotumia misahafu, lakini wapo waliotumia Biblia na sote tumeapa kulinda, kutii na kutekeleza Katiba na kutoa haki kwa wale ambao tunawatumikia. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niombe tu kwamba, kwenye Serikali za Mitaa ni kweli kuna vituo vya afya vimejengwa vingi, kuna zahanati. Pia kuna shule ambapo kuna maboma mengi sasahivi ya nyumba za walimu, kuna maboma ya nyumba za madaktari na wauguzi. Sasa yote haya yanahitaji fedha sasa hivi ili kuweza kukamilisha kwa sababu, watumishi wetu wamekuwa na upungufu mkubwa wa nyumba za kuishi. Wengine hasa wale ambao wamekuwa nje ya miji wamekua wanapata tabu kutoka asubuhi majumbani mwao na kwenda katika sehemu zao za kazi, lakini kama fedha zitapelekwa, nyumba za walimu zikikamilika, nyumba za wauguzi na madaktari, itakuwa tumewasaidia kuishi karibu na sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nitoe mfano tu; katika Jimbo langu kupitia mfuko wa Jimbo kuna kata ambayo ilikuwa ina tatizo kubwa la walimu, lakini nimeweza kutumia Mfuko wa Jimbo ule kupeleka umeme kuunganisha takribani nyumba tatu. Sasa hivi walimu wale katika kukagua shughuli za Mfuko wa Jimbo wameweza kuishukuru Serikali, lakini pia kunishukuru Mbunge kwa kutoa wazo hilo kwamba, kuwapelekea umeme katika nyumba zao. Kwa hiyo, niombe sasa isiwe kama Mbunge nimetumia Mfuko wa Jimbo, niiombe TAMISEMI sasa kule ambako ni sehemu za vijijini kama umeme wetu huu wa *hydroelectric power* haujafika, basi tupeleke hata *solar*, ili wafurahie na wao maisha waone taarifa mbalimbali pamoja na burudani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niingie katika sekta ya afya; niishukuru sana Serikali kwamba, sisi Tanga tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, lakini kupitia kumkera Mheshimiwa Selamani Jafo pamoja na Katibu Mkuu wake ambaye wa sasa hivi amehamishiwa Wizara ya Afya tumeweza kukamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya na sasa hivi mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, nimshukuru kwa hilo, lakini pia nitakuwa ni mchoyo wa shukrani kama sikushukuru fedha zilizoletwa na Serikali kwa kujenga vile vituo vitano vya afya katika Jiji la Tanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunacho Kituo cha Makorora ambacho tulipata milioni 500, tuna Kituo cha Ngamiani ambacho tulipata milioni 500, Kituo cha Mikanjuni tulipata milioni 400, Duga tulipata milioni 500 na Mikanjuni milioni 500. Alituahidi pia alipokuja kukagua Hospitali yetu ya Wilaya kwamba angetuongeza shilingi milioni 400, nimshukuru kwa hilo. Pamoja na hayo naona ipo haja ya kuboresha yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga vituo vya afya vizuri sana, lakini vituo vyetu vya afya havina uzio. Kuna zahanati moja ambayo pia nilitoa milioni 20 kwenye Mfuko wa Jimbo kukamilisha kupata vifaatiba, ilipata matatizo makubwa kutokana na kukosa uzio. Watu wasiotaka maendeleo walibba feni, *switch* na mabomba ya maji. Sasa naona pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Serikali, lakini vituo vya afya havina uzio. Sasa niishauri Serikali kujenga vituo vya afya bila kuvivekea uzio ni sawasawa na mtu uvae suti yako nzuri lakini chini umevaa kandambili, itakuwa hatujafanya kitu. Naomba ziletwe fedha kwa ajili ya kujenga uzio, vile vile pia suala zima la kujenga hivi vituo vya afya na hospitali za wilaya liendane sambamba na kuajiri sasa watumishi. Tupate Madaktari wa kutosha, tupate watumishi wa kutosha na maafisa wengine wa Idara ya Afya ambao wataweza kufanya kazi ili sasa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali iwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulisema ni kwa watumishi nao kuboreshewa maslahi yao. Kwa mfano, kwenye suala zima hilli la *corona*, watumishi wanahuksika na kupima pamoja na kuwahudumia wale ambao tunaona labda hawa wana maambukizi ya virusi hivi, lakini sijui kuna mpango gani wa kuwakinga hasa pale ambapo watumishi hawa wataambukizwa virusi vya *corona*. Tunaona kuitia mitandao namna *corona* inavyoambukizwa kwa urahisi, hata Daktari anavyomsogelea mgonjwa tu tayari inakuwa imempata. Vile vile baada ya hilo niseme pia vifaativa navyo visikosekane. Vipelekwe vifaatiba imara na vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niende kwenye Sekta ya Elimu. Kwenye elimu bure, niseme bado kuna upungufu, kwa mfano baada ya kuja suala la elimu bure sasa hivi wazazi hawatoi michango. Wakiulizwa hasa kutokana na ukali wa maisha wanasema elimu ni bure. Sasa shule zimekatwa umeme na maji.

Niishauri Serikali sasa, ikibidi shule zetu za msingi na sekondari maji na umeme iwe ni bure *no charge* kwa sababu tunaona matatizo yanayowapata wanafunzi. Leo wanafunzi hawana hata maji ya kunywa shule, ashakum si matusi, mama zetu, dada zetu na shangazi zetu, watoto wetu wa kike wanapokwenda msalani, lazima wapate maji. Sasa shule imekatwa maji, shule imekatwa umeme, mazingira yakoje hapo? Nashauri tupeleke maji, tupeleke umeme katika shule zetu ikibidi iwe *free no charge*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine pia kwenye suala zima la matundu ya vyoo. Napata ukakasi kidogo kuona tuna uhuru zaidi ya miaka 50 lakini mpaka leo bado tunazungumzia matundu ya vyoo, sasa hili jambo nalo lifikie mwisho. Kwa sababu Serikali yetu sasa hivi kwa mwezi inakusanya 1.9 *trillion*, basi tutenge fedha maalum kuhakikisha kwamba tatizo la matundu ya vyoo shulenii tunalimaliza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali, lakini kama matundu ya vyoo bado miaka 58 ya uhuru tunajadili, mimi naona hapo bado hatupo sawasawa. Tujitahidi kuhakikisha kwamba matatizo hayo tunayamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala la *capitation*. Katika vitu ambavyo nitaendelea kumkumbuka Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Awamu ya Nne ni kwenye suala zima la *capitation*. *Capitation* wakati wa Mkapa ilikuwa kila miezi sita mwanafunzi anapatiwa Sh.12,000 lakini leo imerudi chini mpaka imefikia sasa kwa mfano kwenye shule yangu ya Ngamiani Kusini inafika mahali wanapelekewa Sh.300,000 shule ina wanafunzi 700. Ukiwaganya hapa ni kwamba kila mwanafunzi anapata shilingi 428.60. Hivi 428 kwa maisha ya sasa hivi itasaidia nini?

Kwa hiyo, niiombe Serikali iongeze fedha kuliko ilivyokuwa Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilisemee hapa ni kwenye suala zima la utawala bora. Tumekuwa tukithibitisha na kusikia na mimi kwenye Halmashauri yangu limetokea, baadhi ya Wakurugenzi wanatumia madaraka vibaya. Siamini kama Mheshimiwa Magufuli amewatuma Wakurugenzi wanunue Madiwani, wawabembeleze Wabunge kurudi Chama cha Mapinduzi. Mtu aone ni utashi wake. Sasa baadhi ya Wakurugenzi wamekuwa wanatumia vibaya majengo ya Serikali kufanya vikao visiviyokuwa halali kuwarubuni na kuwahadaa Madiwani warudi kwenye Chama cha Mapinduzi. Nafikiri aachwe mtu mwenyewe kwa akili yake, kwa sababu zake arudi, lakini sio kwa kuwahadaa!

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sekunde tu nimalizie.

NAIBU SPIKA: Hapana kwa sababu unaanza jambo jipya ndiyo maana nilikuacha umalizie lile ulilokua unamalizia. (*Makofifi*)

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Ahsante. (*Makofifi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu kidogo kwenye hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii, lakini zaidi kwa kunipa uhai. Nikushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Wasaidizi wenu wote kwenye Kiti hicho kwa namna mnavyotuongoza na kututendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayofanya na kuwatendea haki wananchi wa Taifa hili. Kwangu mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Ukerewe, ametutendea haki sana, nina kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru na wananchi wa Ukerewe wanamshukuru, wanampongeza sana. Mheshimiwa Waziri naomba afikishe salamu hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais sisi Ukerewe kwa sababu ametutendea mambo makubwa sana. Tuliomba atusaidie tuwe na Chuo cha Ufundı Stadi (*VETA*), tumepata zaidi ya bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa chuo ambao umeanza. Tuna zaidi ya bilioni 4.0 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ualimu Lutunguru pale, lakini sekta nyine, afya, elimu na kadhalika Mheshimiwa Rais ametutendea haki sana tunamshukuru sana.

Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa namna ya pekee anavyotimiza majukumu yako na wasaidizi wake. Tabia yao ya kufikika kila wanapohitajika ni tunu waliyopewa na Mwenyezi Mungu na azidi kuwajaalia waendelee kuwa namna hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametutendea haki kwetu Ukerewe, namshukuru sana. Niliomba vituo vya afya ametupatia pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Buisya na cha Mliti na bado ametuboreshua mazingira mengi sana. Ombi langu tu kwenye eneo hili kama ambavyo nimekuwa namwomba, Mheshimiwa Waziri jiografia ya Ukerewe anaifahamu na bahati nzuri amefika kule na Naibu Mawaziri wote wamefika, kuna Kisiwa cha llugwa ambacho kutoka llugwa kuja Kisiwa kikubwa ni usafiri wa maji kwa zaidi ya saa tano. Wananchi wa kule wanateseka sana na ndiyo maana nimekuwa naomba sana kwamba tupate pesa tuweze kujenga kituo cha afya kule. Nashukuru sana amekuwa anatoa uelekeo mzuri na waliahidi kwamba watatusaidia, niombe sana atusaidie kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, baada ya ajali ya MV Nyerere pale Ukara alitupatia zaidi ya milioni 800 kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Buisya. Kituo kile sasa hivi kimekamilika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Kituo kile kimejengwa vizuri katika mazingira mazuri sana. Ombi langu kwenye eneo lile watusaidie kupata wataalam ili lile lengo la msingi lillilotarajiwa kwa ajili ya kutumia kituo kile liweze kufikiwa. Zaidi ya hapo, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Naibu Mawaziri wako wametutendea haki sana wananchi wa Ukerewe hasa kwenye eneo hili la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie kwenye maeneo mawili. Wizara hii ya TAMISEMI ambayo kimsingi inabeba taswira nzima ya Kitifa kupitia utekelezaji wake wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta zote kwa sababu ni Wizara mtambuka, imefanya mambo makubwa sana kwa miaka hii minne na nusu kwenye Taifa letu. Kwenye Sekta ya Elimu, Afya, Miundombinu na kadhalika imefanya vizuri sana, lakini pamoja na miradi hii ambayo imekuwa inatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ukamilikaji wake na ubora wake unategemea vitu vingi lakini usimamizi ni jambo muhimu sana kwenye miradi hii. Sasa bahati mbaya sana bado hatuna wataalam wa kutosha kwenye halmashauri zetu hasa kwenye fani ya uhandisi. Kwa hiyo niombe Wizara iweze kuliangalia hili na kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zinapata wataalam hasa wa ujenzi, Wahandisi wa Ujenzi kwenye Halmashauri zetu waweze kusimamia maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii inakamilika chini ya usimamizi wa viongozi wetu walioko kwenye maeneo ya chini hasa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji. Bahati mbaya sana viongozi wetu hawa bado mazingira yao pamoja na kwamba wanafanya kazi kubwa sana, lakini maslahi wanayoyapata kama posho na kadhalika ziko kwenye mazingira ambayo sio mazuri sana. *Imagine* kwenye halmashauri nyingi wanalipwa Sh.3,000 kwa mfano kwa mwezi ambaao ni wastani wa Sh.100 kwa siku. Sasa huyu Mwenyekiti wa Kijiji/Kitongoji kutwa nzima anasimamia mradi

halafu anapata Sh.100, achilia mbali kwamba wanagombea nafasi hizi kama kujitolea lakini hiyo ni nadharia, katika hali halisi, hizi sio nafasi za kujitolea. Kwa hiyo niombe Wizara iangalie namna gani tunaweza tukawasaidia watu hawa ili angalau kuwatia moyo wa kuendelea kusimamia shughuli zetu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kidogo kwenye eneo la *TARURA* ambalo wamechangia watu wengi. Nawapongeza sana *TARURA* kwa namna wanavyotimiza wajibu wao pamoja na kwamba pesa walizonazo ni kidogo sana. Kumekuwa na mchango mbalimbali kwenye eneo hili lakini mawazo yangu pamoja na kwamba tunahitaji waongezewe pesa, ile asilimia 30 wanayopata ni kidogo, asilimia 70 iliyoko *TANROADS*kwa ushauri wangu isingeondoka kwa sababu barabara zillizoko chini ya *TANROADS* bado zitahitaji matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na kupendekeza tuangalie chanzo kingine cha pesa ambacho tunaweza tukakibuni ili kuweza ku-top up hii pesa ambayo *TARURA* wanaipata waweze kutimiza wajibu wao vizuri kwa sababu ni wakala muhimu sana kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu za vijiji. Pia nimekuwa nikiomba kwa Mheshimiwa Waziri pale kwetu Ukerewe angalau tuweze kupata hata kilometra mbili tu za lami pale mjini. Tutashukuru sana ukitusaidia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya msingi kwenye eneo hili, tufikirie namna gani tunaweza tukabuni chanzo kingine ili *TARURA* waweze kupata pesa ya kutosha lakini sifikirii na sidhani kama tutakuwa sahihi kupunguza kwenye pesa za *TANROADS* ili kuongeza pesa za *TARURA*. Tukiweza kubuni chanzo kingine, vyote viwili vikawa na nguvu kuweza kushughulikia barabara zetu, tutakuwa na miundombinu bora ambayo itaweza kutusaidia hata kiuchumi kwenye Taifa letu kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutoa mchango huo kwenye maeneo hayo mawili muhimu. Nashukuru sana kwa fursa hii na Mwenyezi Mungu akubariki. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule ajiandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi mchana huu kwa ajili ya kuchangia kwenye hotuba hii muhimu kabisa. Pamoja na wenzangu wengi waliotangulia nami nianze kwa kukishukuru sana na kukipongeza chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuandaa Ilani ambayo hakika imetekelzeza kwa asilimia kubwa na kiwango cha hali ya juu sana. Haya ndiyo matokeo ya chama kilichoijanda kuwatumikia wananchi na kuongoza dola kwa miaka yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo nataka nizungumze leo, nianze pale ambapo amemalizia mwenzangu Mkundi kutoka Ukerewe. Ni kweli kwamba *TARURA* ni chombo ambacho kimekuja wakati muafaka na *TARURA* ni chombo ambacho kimekuja kutusaidia sana hasa kwenye nyanja nzima ya uimarishaji wa barabara zetu. Sasa niseme kwamba tusipoangalia namna nzuri ya kukisaidia chombo hiki, tutakiacha kuwa mzigo na wananchi kila wanapokwenda wataendelea kuona ni chombo ambacho kimekuja kutupa matatizo badala ya kututatulia matatizo tuliyonayo. Ukweli ni kwamba toka *TARURA* wamekuja nikitolea mfano wa Jimbo ambalo natoka mimi la Nyamagana tulikuwa na kilometra za barabara zisizopungua 457, mtandao mzima. Leo wamekuja *TARURA* wamefanya utafiti na kugundua barabara ambazo wameanza kuzishughulikia na zinazotakiwa kushughulikiwa zaidi ya kilometra 1,026.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sio jambo dogo. Tukiendelea kuwanyima fedha *TARURA* hawatafika mbali na Mheshimiwa Waziri kwenye Taarifa yake amesema vizuri.

Pamoja na fedha alizoziaanda ku haki kisha kwamba mtandao wa barabara kilometra 23,000 zinashughulikiwa, lakini kati ya hizo ni kilometra 35 peke yake za lami ndiyo zitakazojengwa. Sasa nadhani hapa kwanza tuongeze mtandao wa barabara za lami na hii itawezekana tu kama tutawapa *TARURA* fedha za kutosha na sio lazima tupunguze *TANROADS* kama wenzangu walivyosema, tuangalie mfumo mwingine wa upatikanaji fedha ili tuweke hapa na kazi iweze kufanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, *TARURA* wanafanya pia kazi ya kukusanya ushuru wa *parking* kwenye Majiji, sasa niombe pale Mwanza ndipo ilipokuwa inafanyika *pilot study* na hii *pilot study* baada ya mwaka mmoja mpaka sasa hivi kwanza inaonekana imeshindwa kufanya kazi vizuri kwa sababu moja kubwa kwamba bei ambayo iliwekwa mwanzo haikidhi uhalisia kutoka Sh.500 mpaka Sh.1,500, kwa hiyo tumeshazungumza na mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri hili alichukue tuone namna ya kurudisha kwenye uhalisia wa bei ili watu wengi wawe *comfortable* kupaki magari yao mijini na kulipa hii fedha ili tupate hii kodi kwa wingi. Yasitukute yale yaliyotukuta kwenye kodi za ushuru wa mabango.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hii *pilot study* inaonekana *study* yenye ya ule mfumo ambao tulikuwa tunautumia umeonekana kufeli kwa sababu mtu akiwa hajalipa ndani ya siku tatu, siku ile ile ule mfumo unaweza ukagoma na siku tatu zijazo mfumo ukagoma. Hawezi kulipa fedha yote kwa mara moja, hata kama anadaiwa Sh.60,000 analazimika kulipa 1,500, 1,500 mpaka itakapofika kiwango ambacho alikuwa anadaiwa, hii sio sawa. Sasa kwa sababu mwaka umeisha, wakae chini wafikirie upya kwanza ku haki kisha bei inashuka kutoka iliyokuwepo na kuupitia upya mfumo ili hii *pilot study* kama itawenza kufanya kazi ifanye kazi maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa sababu leo sio siku ya maombi sana, lakini nataka hili lifanyiwe kazi. Niishukuru sana Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo imefanya kwenye Jimbo la Nyamagana, kwenye Sekta ya

Barabara, leo ukifika Mjini Kati pale Mwanza, hakuna kipande cha vumbi. Zimejengwa zaidi ya kilometra 7.5 kwa kiwango cha lami chini ya usimamizi wa hii *TARURA* ambayo tunadhani ikipewa mashiko itafanya vizuri zaidi. Tumejenga miradi mikubwa ya maji kupitia *RUWASA* na *MWAUWASA* na tunaendelea kufanya hivyo kwenye Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo, kupanga ni kuchagua. Mwanzo alichagua tuanze na ujenzi wa hospitali za wilaya, hospitali za kanda, zahanati na vituo vya afya na sasa amechagua kupeleka vifaa na waajiriwa kwenye hospitali zote zilizojengwa na sasa amechagua kutoa elimu na ajira za mkataba ili watu wote ambao walianza na wale watakaoingia waende sasa kufanya kazi kwenye miundombinu hii ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Dkt. John Pombe Magufuli ina milango na haya ni maono ambayo huwezi tu kupata kazi hii bila kuwa na maono. Niwaambie wenzangu, lazima wajifunze kufuata maono inawezekana maono ya upinzani ni kushika nchi, bado, kwa hiyo watulie waache wenye maono waendelee mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kazi ni nzuri, na mwendelee kuchapa kazi mpaka tutakapofika mwisho. Mwisho kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Jaffo, *DC* wangu gari lake ni bovu mno, hapa amemkumbuka kuna milioni 220, gari hili lipatikane haraka, Nyamagana ni Mjini jamani, wasifanye mchezo. *Second of the largest City in Tanzania unaongelea Mwanza, Mheshimiwa Jaffo, hebu gari hili liende haraka, DC wangu naye ajisikie kama anafanya kazi mjini akishirikiana na mtoto wa mjini.* Mheshimiwa wangu Mkuu wa Mkoa na watendaji wote wa Mkoa wa Mwanza, Mungu awabariki sana kwa ushirikiano mkubwa ambaou umeleta mafanikio na mabadiliko makubwa Mwanza. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola ajiandae.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya ya kusimama hapa na kusema mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumshukuru Mungu sasa kwa kuwa ametupatia nafasi hii ya kuwepo hapa, lakini pia llani ni mkataba kati ya mtawala na mtawaliwa. Naomba tena nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa jinsi anavyofanya kazi hii ambayo tumempa sisi Watanzania kwa kura zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jafo, kwa kweli anafanya kazi hii usiku na mchana. Mimi nimeshuhudia kuona akifanya kazi hii alivyofika Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu hawa pia Naibu wake wote wawili; Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara, hawa wote wamefika Jimboni. Pia Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii Mungu awabariki sana na muendelee kuchapa kazi kwa sababu mnamsaidia sana Rais kwa majukumu haya aliyowapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposifu pia unaongeza nafasi ya kuomba. Pamoja na haya yote llani imetekelezwa kwa kipindi hiki cha miaka hii mitano kwa kweli kwa asilimia kubwa sana. Chama cha Mapinduzi kimeonekana kizuri sana kwa wananchi na wananchi wanampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu tu ya utekelezaji huu wa llani na ni mkataba mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia upande wa Biblia, Biblia nayo ni mkataba kati ya Bwana Mungu wakati wa Ibrahimu na Yesu wakati huu wa Agano Jipy. Kwa hiyo, mikataba hii inakwenda vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, nishukuru sasa tumejengewa Hospitali kubwa ya Wilaya

inafanya kazi ndani ya Jimbo langu. Hata hivyo, shilingi milioni 300 zinatakiwa tu kuongezwa pale Mheshimiwa Jafo ili hospitali ile sasa ikamaliziwe kabisa. Umeiona ilivyo nzuri, nina hakika umeona inavyosifiwa sana hospitali ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakati tunaingia katika awamu hii ya uongozi wetu hatukuwa na hospitali kabisa, leo tunakuwa na hospitali ya wilaya na Kituo cha Afya cha Dongobesh. Mungu awabariki sana na nashukuru kwa ajili hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mpelekee Rais shukrani zetu za kutujengea jengo la halmashauri ambapo sasa tunakwenda kuingia kwenye jengo letu, wananchi tulikuwa tunatembea kwenda kilometra 50, 80 kufuata huduma. Sasa hivi tuna jengo hili linakwenda kumaliziwa, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, niombe sasa utaratibu huu wa *certificate* ambao unapelekwa kwenye Wizara ya Fedha muone namna gani ya kutusaidia. Tuna *certificate* yetu ambayo imekwenda pale ili jengo lile likamaliziwe. Sasa hivi linakwenda ghorofa ya tatu, naomba Mungu akubariki *certificate* itoke jengo lile limaliziwe tuweze kuingia mle ndani tukafanye kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limesemwa sana jambo la *TARURA* na mimi niongezee. *TARURA* kwa Jimbo la Mbulu Vijijini tulikuwa tuna barabara inayojengwa ya kilometra 42 sasa hivi tuna kilometra 1,000. Naomba tusaidiane tu kidogo, pamoja na kwamba najua fedha zimekuwa na changamoto, kwa kweli sasa hivi barabara zimeharibika sana, niombe tutafute namna yoyote ya kuisaidia *TARURA* ili barabara zilizoharibika ziweze kujengwa kipindi kinachofuata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni maboma. Nishukuru sana Wizara hii imepanga kumalizia maboma mengi. Nimeona kwenye bajeti mmetenga na mmefanya kazi vizuri sana. Tunayo maboma katika Jimbo la Mbulu Vijijini

yanayopaswa kumaliziwa. Mheshimiwa Jafo najua wewe ni mchapakazi endelea kufanya kazi hii na Mungu akubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna vituo vya afya, nishukuru umetujengea Kituo cha Afya cha Dongobesh. Hata hivyo, tuna Vituo vya Maretadu, Haydom na tumeleta maombi hayo, utuangalie katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Kata tatu kwenye Tarafa ya Eda Chini, tumeleta maombi tupatiwe tarafa tu maana siyo gharama kutuanzishia tarafa. Tunaomba tuanzishiwe Tarafa ya Eda Chini ili eneo lile liwe vizuri katika kutawaliwa kwa sababu kule kuna Wahadzabe. Mara nydingi unajua watu wale wanapenda kutafuta miti na wanakaa vijijini na ndani ya msitu sana, ili warudi basi maeneo ya mijini na tumeshajenga sekondari yao, nishukuru mmejenga sekondari pale tumepata shillingi millioni 215 basi tuwape eneo la utawala ili waweze kujitawala ili mambo yawe mazuri Wahadzabe katika eneo letu nao wapate eneo lao la kujitawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kukushukuru pia kwa kweli tunaona jinsi ambavyo unatusaidia sisi katika utawala bora. Mimi najua wazi kwamba Mheshimiwa Rais anapita bila kupingwa na naona kabisa sura za Wapinzani kule zinaenda kumkubali. Tunachotaka sisi ni kazi ifanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muungwana ni vitendo, ukiangalia jinsi anavyotawala, kuna kitu kinachoitwa uhalali wa kutawala. Binafsi yangu namuombea Mungu na namuombea sana ampe afya njema ili mambo yaende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niombe sasa kwa sisi tunaosali tuombe sana jambo hili la *Corona*. Kwa kweli *Corona* ni ugonjwa mbaya na mimi naomba tu tuangalie vizuri. Nimshukuru sana Waziri Mheshimiwa Ummy pamoja na kwamba nikipata nafasi nitazungumza siku hiyo lakini leo nimshukuru sana anafanya kazi nzuri. Sisi Wabunge tufanye maombi ya jumla kusaidia, Mungu ukishamuomba anakubali

kuondoa kitu kinachoitwa ugonjwa. Pia tuchukue tahadhari kuhakikisha kwamba tunajikinga na ugonjwa huu na wananchi wetu wanajua. Katika hili niipongeze Serikali kwa sababu wamechukua hatua kubwa ya kupambana na ugonjwa huu na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Jafo pia wamechukua suala la taulo za kike. Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la mwisho, muone namna ya kuwasaidia Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji zile asilimia 20 kulehaziendi. Kwa hiyo, mkijaribu kusaidia asilimia zile zikaenda ni wazi kwamba ugatuaji wa *D by Dutakwenda* vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Joseph Leonard Haule atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola na Mheshimiwa Jumanne Miraji Mtaturu ajiandae.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kutuongoza vema kwa weledi na ukakamavu mkubwa. Namwambia tu kwamba giza linapozidi kuwa totoro kunakaribia kukucha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa kingine nimshukuru sana kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri Kivuli wa Madini. Naahidi sitamuangusha nipo vizuri sana mpaka najikaribia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa TARURA. Kama umesikiliza vizuri kwenye Bunge lako la

Jamhuri ya Muungano, watu wengi sana sasa wamekimbilia TARURA kwa sababu hali huko kwenye mitaa yetu imekuwa mbaya sana. TARURA imekuwa na kiwango kidogo cha pesa lakini kumekuwa na maafa mengi sana kwa mwaka huu katika maeneo yetu mbalimbali. Mfano kwenye Wilaya ya Kilosa hapa sasa hivi ninavyoongea watu wa Masanze, Manzese na Mbumi wapo kwenye maji na barabara zao hazipitiki lakini tumekuwa na mafuriko mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mingi tumekuwa tukija Bungeni na kuiomba Serikali itusaidie miundombinu imekuwa mibovu sana kule Kilosa. Hiyo yote inatokana na Mto Mkondoa ambao unaleta maji mengi kutoka Bwawa la Kidete. Nilishauliza hapa Bungeni mara kadhaa kwamba hili Bwawa la Kidete litajengwa lini tukaambiya hapa na Serikali iliahidi imeshatenga shilingi bilioni 2 wanafanya upembuzi yakinfu lakini mpaka leo imekuwa kimya, bwawa lile linatutesa sana wananchi wa Kilosa. Pia limeleta maafa sana kwenye Kata za Masanze, Kilangali, Manzese lakini pia maeneo ya Kata za Magomeni ambapo maji yote yanakwenda kuharibu miundombinu ambayo Serikali wanajenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama alifanya ziara pale, tulimuomba aweze kutujengea tuta kwenye Mto Miyombo ambao unaleta madhara makubwa sana kwenye Kata za Tindiga, Mabwelebweli na maeneo mengine ya kule Kilosa. Naiomba Serikali ituambie ni lini itatujengea hili tuta la Mto Miyombo lakini lini itamalizia ujenzi wa Bwawa la Kidete ili angalau litufanye na sisi wananchi wa Kilosa tuendelee na shughuli zingine za maendeleo maana kila siku imekuwa kilio ni kuhusu maji na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu imekuwa ni tofauti kidogo maji ya mvua pamoja na kwamba kila siku tumeyazoea lakini sasa kuna maji mengi sana ambayo yanakuja kutoka pale TANESCO kwenye Bwawa la Kidatu ambalo linazalisha umeme. Bwawa la Kidatu linatuna maji lakini yanazidi kiwango inaonekana wanayafungua kwa

makusudi, sasa hivi yametaka kuleta maafa makubwa lile daraja la pale Ruaha linaloenda Kilombero limekuwa likitetemeka likitaka kuanguka mpaka *TANROADS*wamekuja pale kulitengeneza. Wananchi wamepata tabu sana, makaburi yamekwenda na maji lakini pia Kijiji cha Kitete kilichokuwa katika Kata ya Ruwembe chote kimepotea na maji kwa sababu ya yale maji ambayo yametoka kule *TANESCO* - Kidatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Serikali, tunajua kwamba utaratibu wa hali ya hewa kuwaambia wenzetu wa *TANESCO* wanapoweka maji kuna kiwango fulani, basi wasiwe wanayaacha yawe mengi ili kuyamwagia kwa wananchi utadhani hawana sababu za kuendelea kuishi pale. Tunaomba sana Serikali itusaidie kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia *TARURA* wamekuwa na uwezo mdogo wa kifedha. Nakumbuka mwaka jana niliwaomba Serikali itusaidie gari la *TARURA*, inaonekana kwamba sasa hivi angalau wanaweza ku-move. Wilaya ya Kilosa ni kubwa sana, ina Kata takribani 40 kuanzia hapa Kiyegea ambapo daraja la *TANROADS* lilikuwa linasumbua mpaka kuelekea Ruaha Mbuyuni, linakwenda mpaka Kibakwe kule kwa Mheshimiwa Simbachawene, ile yote ni Kilosa *TARURA* wanashindwa ku-manage kufanya kazi za kutengeneza barabara zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa navyoongea barabara kutoka Ruaha Mbuyuni kwenda Malolo, Uleling'ombe inatokea mpaka Mpwapwa ambayo inaunganisha Mikoa ya Iringa, Dodoma na Morogoro haipitiki kabisa. Pamoja na hiyo kuna barabara nyingine ya kutoka Kidodi mpaka Vidunda, Waziri wa Nishati ametuletea pale nguzo za umeme kwa ajili ya kupeleka kule Vidunda barabara haipitiki, nguzo zimekaa pale takribani miezi sita sasa. Tunaona sasa hata yale mambo ya Serikali wanayopanga kusaidia hayawezি kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara kutoka Ulaya - Madisini – Malolo nayo haipitiki kabisa kwa sababu

hali imekuwa mbaya. Mbaya kuliko zote ni hii barabara ambayo imeharibika sana sasa hivi kutokea Kilosa - Mkotani - Mabwelebweli - Kimamba, hiyo ndio haipitiki kabisa. Kwa hiyo, tuone ni jinsi gani ambavyo tunatakiwa kuipeleka pesa ya TARURA ifike maeneo yale iweze kuwasaidia wananchi wa kule Kilosa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa suala la afya. Tuna vituo vya afya vitatu; kimoja ambacho Waziri alikuja kukikagua pale Mikumi kimeshakamilika, kinafanya kazi na Waziri Mkuu alipokuja alituambia tujenge wodi ya wazazi. Tumeshajenga wodi ipo kwenye lenta tunamalizia kwa kutumia pesa za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Kituo cha Afya cha Kidodi na Kituo cha Afya cha Malolo ambacho wananchi wanajenga kwa nguvu zao binafsi na mimi kama Mbunge wao nimewachangia mifuko 400 sasa ili tuweze kukikamilisha. Hata hivyo, bado inaonekana nguvu ya Serikali inatakiwa kuwa pale kuweza kutusaidia wananchi wa pale tuweze kumalizia Kituo cha Afya cha Malolo. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niliomba Serikali itusaidie kuboresha Kituo cha Afya kikongwe cha Ulaya kinachohudumia Kata ya Ulaya, Mhenda na Zombo lakini bado mpaka leo kituo kile hakijapata msaada wowote. Naomba Serikali itusaidie pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kwamba barabara ya kutoka Dar es Salaam - Zambia inapita pale Mikumi, kumekuwa na ajali nyingi sana ambazo zinatokea pale Mikumi hasa kwenye maeneo ya Msimba na kwenye kona za lyovya mpaka Ruaha Mbuyuni hakuna mtandao wa simu. Niliomba Serikali itusaidie, watu wengi wanapata ajali lakini wanashindwa kuwasiliana na ndugu zao wanapopata matatizo kama hayo, tunaomba tupate mtandao wa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kutoka pale Mikumi kuelekea Kilosa ni kilomita 78, kutoka Mikumi kwenda Morogoro ni kilomita 120, kutoka Mikumi kwenda Iringa

kwenye hospitali kubwa ni kilomita takribani 200; tuliomba tusaidiwe *ambulance*. Mimi kama Mbunge nimekuja huku Bungeni muda mwingu nikikimbizana na Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na msaidizi wake kuwaomba *ambulance* na nimeambiwa *ambulance* zimefika. Naamini sasa tutaenda kuokoa maisha ya Watanzania ambao wanaumia sana kwa ajali mbalimbali sasa wataweza kupata rufaa za kupelekwa sehemu mbalimbali kwa sababu *ambulance* mbili zimeshafika. Tunashukuru kwamba zitaweza kufanya kazi ile tuliyoiomba kwa muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya, nataka niongelee kuhusu ziara ya Waziri Jafo kule Mikumi. Mheshimiwa Jafo ulikuja Mikumi ukakagua Daraja la Ruwembe ambapo ulipokuja tulikuomba shilingi milioni 700 ukasema hii kwenye tathmini ulioifanya tulikuwa tunahitaji karibu billioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa kule mvua kama hizi sasa hivi hakuna shughuli inayoendelea, watu wanazidi kufa. Mheshimiwa Jafo ulipokuja watu walipata matumaini sana na watu wanakuamini wakasema kwamba iwapo Waziri amesema atatutengea shilingi bilioni 1 basi tutaweza kupata daraja letu. Yale machuma ulitupa kutoka kule Kiberege yapo pale nchini mpaka leo karibu mwaka wa pili Mheshimiwa Jafo hakuna kinachoendelea. Matatizo yamekuwa mengi, wananchi wa Ruwembe bado wana imani kwamba unaweza ukawasaidia kupata zile pesa ulizowaahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yametokea mambo mengi ya sintofahamu katika maeneo mbalimbali lakini Mheshimiwa Waziri amenyamaza kimya. Kulikuwa na sintofahamu nyingi na kubwa katika maeneo ya Serikali za Mitaa kwenye uchaguzi ule, watu wakawa wanaku-zoom tu umenyamaza kimya. Sasa hivi Mameya wanaanza kuenguliwa kwa hila, figisu na vitu vingine; haya mambo bado yanaonekana kuwa umenyamaza kimya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote yanayoendelea, huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu, tunaamini wasimamizi wa uchaguzi watakwenda kuwa na imani na wataenda kusimama katika haki ili tuweze kupata hiyo haki. Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri watu wana imani na wewe, wala mimi siwezi kusema kitu kibaya lakini kwa hili anaponyamaza kimya maana yake ana-endorse na anakubaliana na utaratibu unaoendelea, anatufanya tunaomwamini tuanze kuwa na mashaka na hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na haya mambo yaliyotokea wamepita viongozi wengi, kuna mwingine alikuwa anasema: "Jembe si jembe", ana llani hapa na mifuko yenyе bendera lakini leo anapambana peke yake kule Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Waziri usije ukapata tabu Tanzania ikaingia kwenye matatizo wewe ndiye Waziri mwenye dhamana baadaye ukachafua mikono yako ya kazi nzuri uliyokuwa unaifanya kwa sababu ya mambo kama yale. Mwenzetu wa 'jembe sio jembe' sasa hivi anataabika mwenyewe, leo TAKUKURU kesho Polisi, yasijeyakakukuta wewe ndugu yangu kwa sababu tunajua umefanya kazi nzuri, nimeona nikuhusie katika bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, halmashauri zetu zina hali mbaya sana. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ina hali mbaya, pesa zote zimeenda kwenye Mfuko Mkuu. Pamoja na pesa zote kwenye Mfuko Mkuu hata kujenga stendi pale, Waziri Mkuu alikuja akashangaa Mikumi haina stendi, akashangaa Mikumi malori yote yanapita pale lakini hatuna maegesho ya magari kwa sababu Halmashauri yetu ina hali mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba zile pesa za Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa zije kule. Mkurugenzi anapambana kuangalia jinsi gani ya kutafuta pesa, sasa hivi anapambana na wafanyabishara wa Mikumi, wamejenga vibanda vyao, wametengeneza biashara zao, Halmashauri imepora wafanyabiashara wa Mikumi inasema vile vibanda ni vya Halmashauri. Nitakuletea hawa watu, nasubiri *Corona* ipite tena mzee nitakujazia watu kwenye ofisi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Amen.

Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na kutoa pongezi kwa viongozi wetu wakuu, nikianza na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa taifa letu. Hakuna mtu anayebisha kazi tumeziona kwa macho yetu, masikio yamesikia, Rais anafanya kazi nzuri sana na nchi yetu imekaa mahali pazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye Jimbo langu kwa kweli viongozi wa Serikali wamenifanya jambo jema. Mawaziri 8 wametembelea kwenye Jimbo langu ndani ya miaka hii minne iliyopita. Viongozi wakuu nikianza na Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wamefanya mkuutano kwenye Jimbo langu na kila jambo walilotamka limefanyika. Mimi nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuna changamoto nyingi sana lakini sasa hivi asilimia 98 changamoto zimetatuliwa. Nikianza na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Jafo nakupongeza sana na ulikuja hata kule kwangu. *High school* zilikuwa mbili tu sasa hivi zimeongezeka mbili tuna *high school* nne, siyo jambo dogo kwenye Jimbo moja tu. Nakushukuru sana Makamu wa Rais alipokuja pale Mgololo tulimuomba *high school* na amekubali mwezi Julai wanaanza, ametoa kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mbalamaziwa tumejengewa *high school* ambayo imegharimu karibu zaidi ya shilingi bilioni 1, Serikali imeleta pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo kwa kazi nzuri unayoifanya Mungu atakubariki na anaendelea kukubariki, akulinde sana katika afya yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepewaa hospitali moja kubwa sana na imeisha na sasa hivi tunasubiria tu umaliziaji ili hospitali ianze kutumika. Wana Mufundi tulikuwa tuna hospitali moja tu, tulikuwa tunapata tabu sana lakini hospitali mliyotujengea ile tunawashukuru sana na wananchi wa Mufundi wanasema mbarikiwe sana na Mungu atawabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejengewa kituo cha afya kikubwa sana, zote hizo ni fedha, kituo cha afya kipo pale Malangali kinahudumla Kata nne. Zile kata nne zillikuwa zinapata shida sana kwa sababu mimi kule napakana na Mbeya lakini Serikali imefanya jambo jema kujenga kile Kituo cha Afya pale Malangali na sasa hivi wananchi wanatumia kile kituo na wanawapongeza na wanashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii imefanya kazi nyingi sana. Mimi napongeza hata Chama cha Mapinduzi, Katibu wetu Mkuu, Dkt. Ali Bashiru amefanya kazi nzuri sana kuweka chama kikae vizuri. Nakupongeza sana Katibu Mkuu wetu na sisii Wabunge tunamshukuru kwa kutuweka vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja kwenye Ofisi ya TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo nimeshakwambia. Kwanza, tumpongeze sana Rais wetu kwa kusema kwamba halmashauri zile mpya watumishi wahame waende kule kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Lile jambo ni jema sana. Bahati nzuri mchakato ulifanyika vizuri sana lakini mimi nimepata changamoto nadhani niliandika na *copy* niliwapa. Bahati nzuri nilimuomba Mkuu wa Mkoa aweze kuingilia kati suala lile na katika Kanuni ikaonesha kwamba hana mamlaka ya kutengua yale maamuzi mengine yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Jafo lile suala la Mufindi hebu lifuatilie. Haiwezi kuhama Igohole Makao Mkuu ambayo Baraza la Madiwani lilichagua mara ya kwanza tuseme tunaenda kwa mara ya pili walipochagua Misana Itulituli. Jimbo la Mufindi Kusini tuna kata 16 na vijiji zaidi ya 76. Ukitoka pale Igohole mpaka kule Kwa Twanga karibu kilometra 140. Ukitoka pale Mafinga mpaka kule Idete kilomita karibu 160, kule napakana na Morogoro. Kwa hiyo, ukiangalia jiografia yake utaona Igohole pale walipochagua mara ya kwanza ndiyo sahihi. Bahati nzuri watu wengi sana na viongozi wanasema tukihamisha pale italeta matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka kule Mafinga mpaka kule Idete kuna kilometra karibu 160; kule kunapakana na Morogoro. Kwa hiyo, ukiangalia jiografia yake utaona Igowole pale walipochagua mara ya kwanza ndiyo sahihi. Bahati nzuri sana watu wengi viongozi wanaongea, wanasema tukihamisa pale tutaleta matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingine ambayo imetubana sana. Jiografia ya Mufindi ni ngumu hasa barabara. Barabara imekuwa tatizo Tanzania nzima kwa sababu ya mvua na mvua hatuwezi kusema isinyeshe, mvua ni baraka, lakini barabara za Mufindi zimeharibika sana. kuna barabara hii ya kutoka Mafinga mpaka kule Mgololo, ile barabara ni ya kibialashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa naangalia kuna gari moja lilikuwa limechukua chai, kule *Uniliver Company*, imekwama; imekaa siku nne na chai pale. Ile barabara bahati nzuri Rais alishapitisha kwamba ijengwe kiwango cha lami, nampongeza sana. Wataalamu walishafika na upembuzi yakinifu ulishafanyika namshukuru sana kwenye hilo. Naomba sana, mwezi wa Sita au wa Saba tukifika, basi mchakato ule uanzé kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *TARURA*, kuna barabara moja kutoka Sawala mpaka lyegeya kilomita 33.3 saa hizi wako *site*. Ile barabara inajengwa kiwango cha lami,

nawapongeza sana kwenye hilo na wale wafadhili wanaofadhili ile barabara nawaombea kwa Mwenyezi Mungu waendelee wasipate matatizo ili waijenge barabara ile vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kuna tatizo hili la *Corona* na ninapenda niwaambie sana wananchi wangu wa kule Mufindi, kweli ni ugonjwa hatari wa dunia nzima. Huu ugonjwa ni hatari na bahati mbaya masharti yake ni magumu. Wanasema uwe na *sanitizer*, sasa vijijini kule hakuna. *Sanitizer* unapata mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine wanasema kwamba masharti ukigusa pua umeambukizwa, ukigusa mdomo ni tatizo; haya masharti ni magumu sana. Naona kwamba jambo jema, tumwombe msamaha Mwenyezi Mungu, tumrudie Mungu. Hata tukisema tukae ndani ya chumba tujifungie, tujifungie tusome *Quran*, tusome *Bible*, ile itatuongoza. Naona kama sasa hivi maisha yamekuwa magumu na hii haina ujanja. Ukiangalia masikini na tajiri wote tunakutana mahali pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Miraji Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, tutamalizia na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali.

MHE. JUMANNE M. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu kabisa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ndiyo inashughulika na kusukuma maendeleo ya wananchi wengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaongea neno la shukrani na pongezi na kuleta mchango wangu, nianze kwa kukumbusha kidogo. Kumekuwa na hoja zikitolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa kwenye Bunge letu na

wengine wameendelea kusema kwa kubeza hata baadhi ya mambo ambayo yamefanyika na wengine wakitoa mfano kwamba miaka hamsini leo inaenda na nane bado tunazungumzia namna ya kujenga vyoo; na kwamba labda Vituo vya Afya havijakamilika na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza lazima watambue kwamba maendeleo ni mchakato, kuna hatua na hatua. Mahitaji yanabadiilika kulingana na idadi ya watu. Wakati tunapata uhuru mwaka 1961, tulikuwa na idadi ya Watanzania milioni takriban tisa hivi. Tukikumbuka wote leo tunakaribia Watanzania zaidi ya milioni 50. Maana yake ni kwamba lazima hata bajeti zetu zitabadilika kila mwaka kulingana na idadi ya watu. Kwa hiyo, hili lazima kwanza waweke kumbukumbu sawa sawa wakati wanakuja kuchangia, siyo suala la kuleta ushabiki kwenye mambo ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niseme nchi yetu ni kubwa. Ina takriban kilomita za mraba 900,000. Ni nchi kubwa sana kuliko hata nchi yoyote hapa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa hiyo, naomba tu wakati tunajadili hilo kama Watanzania ambao tuna nia njema wote, tuzungumze tukijielekeza hapo, kwamba tunayo kazi kubwa kwa pamoja, idadi ya watu tulionao lazima tuendane na namna ya kuwatengenezea mazingira ya kuwapatia huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo hayo ambayo nadhani ni vizuri sana yawekwe vizuri katika kumbukumbu zetu, ni kwamba nchi yetu, viongozi wetu na awamu zote zimeendelea kujitahidi sana kuifanya nchi yetu iendelee kuwa na maendeleo ambayo leo tunajivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maneno hayo ya mwanzo, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujalia uzima kuendelea kuwa hapa kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nachukue nafasi hii kwa kweli kwa heshima kubwa kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa hakika tumepata kiongozi ambaye ni mahiri, jasiri ambaye ameamua kujitoa kwa ajili ya Watanzania kama anavyosema mwenyewe. Hili lote Watanzania tunajivunia na kwa hakika hakuna mtu ambaye ana dhamira ya kweli anamwogopa Mungu, akasimama akasema eti Mheshimiwa Rais hajatimiza wajibu wake. Amefanya kazi nzuri nasi wote kama Watanzania tuendelee kumuunga mkono ili aendeleze kazi nzuri ambayo anaifanya na ambayo ye ye mwenyewe amesema yuko tayari kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri chini ya wasaidizi wake; yuko Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, amekuwa akizunguka sana kwenye nchi yetu kumsaldia Mheshimiwa Rais, tunampongeza sana. Zaidi ya hapo, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni mratibu mkuu wa shughuli ya Serikali. Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Jafo na wasaidizi wake, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jafo mwenyewe, binafsi mimi ni shahidi, nimekuwa Mkuu wa Wilaya kwenye maeneo yale, amekuwa akinitembelea na kwa hakika ametutia hamasa. Tunampongeza sana, anafanya kazi nzuri, asonge mbele kwa sababu Tanzania inahitaji viongozi vijana ambao wanaweza kuisimamia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Manaibu Waziri wake ni wazuri, wanafanya kazi nzuri; Mheshimiwa Kandege pamoja na Mheshimiwa Waitara. Namwambia na Mheshimiwa Waitara asichoke, kule Tarime pia ni sehemu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, aendeleee kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya shukurani, basi niendeleze maneno machache sana kwenye hayo ya utekelezaji. Wilaya yetu ya Ikungi ni Halmashauri, inafanya kazi nzuri ya uratibu. Tumeendelea

kuona matunda ya yale yanayofanywa, tumeendelea kupokea fedha takribani shilingi bilioni tatu katika kipindi hiki ambacho tunamaliza. Siyo fedha ndogo, ni fedha nyingi zimeendelea kuboresha Vituo vya Afya, zimeboresha barabara, na hivi tunavyoongea tumeepata fedha kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ambayo kimsingi hili nilitaka nimwombe Mheshimiwa Jafo kwamba fedha zile tulizoomba bado hatujaletewa tuanze ujenzi ule.

Naomba sana shilingi milioni 300 zile zije tuweze kuanza kujenga Hospitali yetu ya Wilaya iweze kuwashudumia wananchi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la afya, tumeepata Vituo viwili vya Afya kwenye Halmashauri yetu; Sepuka na Ihanja. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja mwaka 2019 tulimwomba Kituo cha Afya pale Ntuntu ambacho pia kumekuwa na changamoto ya huduma. Zaidi niongeze kwenye eneo hili, tutakuwa na eneo la Isuna pamoja na kule Misughaa, nako tunaomba tupatiwe Vituo vya Afya kusogezza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, wameongea maneno mengi, nakuomba sana, kuna eneo hili la watumishi. Katika Halmashauri yetu tunahitaji watumishi takribani 3,600 lakini tulionao ni 1,900. Kwa hiyo, tuna upungufu karibia 1,540 ambayo inafanya kada ya elimu pamoja na afya kushindwa kufanya kazi zetu vizuri kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuja basi atuambie namna ambavyo tutaendelea kuboresha eneo hili. Pamoja na yote haya, tumeendelea kusukuma suala la mapato na Halmashauri yetu imeendelea kupata hati safi. Naomba nikuhakikishie kwamba sisi Wabunge tutaendelea kuwaunga mkono watumishi walioko kwenye Halmashauri yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 kwa ajili ya Watanzania ambao tunaenda kuwaongoza. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mch. Msigwa dakika nne, tutamalizia na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi naanza kwa kumpongeza Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini tena na kunitfea kuwa Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii. Vilevile na maswaibu makubwa ambayo tumepitia kama viongozi, Wazungu wanasesema, "*smooth water never develop a skill for sailor.*" Nadhani michakato hii inatuimarishe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja kubwa nataka nizungumze. Manispaa ya Iringa ni moja ya Manispaa nzuri na bora katika nchi ya Tanzania. Kwa kipindi cha miaka mitano nimekuwa Mbunge, tumekuwa na hati safi, maana yake ni *value for money*; tumekuwa tukipata zawadi hata kwenye masuala ya usafi, tumepata na trekta, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitupa; tumekuwa tukikusanya mapato na Madiwani kutoka sehemu nydingine wamekuwa wanakuja kujifunza kwenye Manispaa yetu, kwa mfano, Morogoro, Singida, Sumbawanga na maeneo mengine. Hata Moshi kwa rafiki yangu Mheshimiwa Japhary wamekuja kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmekuwa mkisema mnataka wizi usifanyike katika maeneo, mnataka kazi ifanyike katika maeneo hayo, lakini Mheshimiwa Jafo cha kushangaza wenzangu wamezungumza hapa, Manispaa yangu ni kati ya Manispaa zinazong'ara, hata Kamati ya LAAC ni mashahidi. Manispaa ya Iringa iko ng'aring'ari, ni kati ya Manispaa nzuri hata kama hutaki. Cha kushangaza, tumekuwa na Meya ambaye ni mmoja ya Mameya bora katika nchi hii aliyesimamia kazi hii. Kumekuwa na *impunity* ya hali ya juu sana katika nchi yetu. Kanuni na taratibu zinasema kumwondoa Meya ni lazima umtoe kwa *two third*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uongozi wa Serikali ya Mkoa na Mheshimiwa Jafo nilikushirikisha, wamefanya fitina kwa fujo kabisa. Wamemtoa Meya katika uongozi, mtu

anayefanya kazi kubwa ambaye ni mfano katika nchi hii kwa uongo na tuhuma za uongo. Wamemtoa Madiwani 14, tuko Madiwani 26. Madiwani 14 unapataje *two third*, hesabu za Darasa la Nne; *two third* inapatikanaje? *Two third* ni Madiwani 17, lakini Serikali inabariki. Haya mambo ya *impunity* tunajenga *precedence* ambayo siku za *future* itakuja kutuletea tatizo katika Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliomshaki Meya hawaonekani. Muda wa kujitetea Meya kwa mujibu wa kanuni, haupo. Tunajaribu kudai hao waliomshaki ni akina nani? Fujo zinafanyika, tunabariki, tunawasiliana na vyombo vinavyohusika, hakuna msaada. Sasa hizo Serikali za Mitaa ambazo mnawapa mamlaka, hawa watu hawakujichagua wenyewe, tunaendeshaje nchi? Nchi inakuwaje kwa uonezi wa namna hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, eti fisadi ana ka-*Spacial* ambako alikuwa nako hata kabla hajawa hajawa Diwani. Najua unaweza ukaja hapa ukasema kanuni na taratibu zinasema akate rufaa, aandike barua; lakini Meya wa Dar es Salaam ameandika barua zaidi ya mwezi hujamjibu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba haya mambo, hili ni Taifa la sisi sote, tutende haki. Tuwatendee haki! Mkuu wangu wa Mkoa ameshindwa kufanya kazi, anatafuta sababu za kupata sifa ambazo hazipo. Naomba Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa, ahsante sana. Shukurani. Tutamalizia na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii adimu kwa siku ya leo, nami kuchangia katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa inayoongozwa na Mheshimiwa Waziri Jafo, Waziri

kijana. Kwanza binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Jafo, anafanya kazi nzuri na anatuwakilisha vijana walio wengi katika nchi hii kwamba tukipewa nafasi tunaweza tukasimamia vizuri na nchi hii ikasonga mbele. Hongera sana kaka yangu Mheshimiwa Jafo kwa kazi nzuri unazozifanya. Tumeona...

Mheshimiwa Mdee, kidogo sikiliza huku! Mheshimiwa Mdee! (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naona wenzangu wanapiga kelele humu ndani ya Bunge na leo wamepoa sana kwa sababu hoja zinazokuwa zinawasilishwa hapa toka asubuhi mpaka muda huu wamekuwa baridi kama vile wamemwagiwa maji. Ni kwa nini? Ni kwa sababu yaliyozungumzwa humu hakuna yanayodanganywa, yote ni ya ukweli. Tukisema zimejengwa hospitali 77 au 100, wote mnakubali kwamba kazi imefanyika. Kwa hiyo, leo hii Wapinzani wetu wamepoa, wamekuwa wadogo kama *piriton*. Majibu wameyapata. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zamani kipindi kama hiki, huwa Bunge linawaka moto kwa sababu tunaelekeea kwenye uchaguzi. Sasa kwa sababu muda huu leo wamepoa, tunaelekeea kwenye uchaguzi, wanajua tayari hapa ngoma imeshamalizika hii! Tunakwenda kuwapiga kama vile kumsukuma mlevi na kopo lake la gongo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wizara kwa kazi nzuri. Tumeona hapa 2015 hospitali zilikuwa 77, leo kuna hospitali zilizojengwa mpya na kukarabatiwa 175. Ni kazi nzuri na kazi ya kusifiwa. Katika hizo hospitali 175 mpya zilizoongezeka na kukarabatiwa, naomba Mheshimiwa Waziri aongeze na ya Igunga iwe ya 176. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuongzee pale jengo la *mortuary*, jengo la mama na watoto na jengo la kufulia. Hospitali yetu ya Wilaya ya Igunga inahitaji na yenyewe ipate fedha kwa ajili ya

kuongeza hizo idadi au hizo hospitali ambazo zimetengenezwa na kukarabatiwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwai tumeona Vituo vya Afya 535 kutoka mwaka 2015 mpaka kufikia Vituo vya Afya vilivyojengwa 968. Ni ongezeko la Vituo vya Afya vinya 433, hongera sana Mheshimiwa Waziri na pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kazi ni nzuri na inaonekana. Naomba Mheshimiwa Waziri aniongezee kituo kingine cha afya. Amenipa kile Kituo cha Afya cha Simbo tunamshukuru sana. Nasi hatuachi kushukuru, ila tunaomba tena kingine kwa maana tupate pale Choma, shilingi milioni 200, tupate Ziba, tupate na Mwisi, kwasababu Jimbo ni kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wengine wamezungumza, majimbo mengine yana Kata nane. Jimbo langu lina Kata 19; Wilaya nzima ya Igunga ina Kata 35. Unaweza kuona huu mgawanyo wa maeneo haya tofauti tofauti. Mheshimiwa nakuomba sana uniongezee fedha kwenye baadhi ya Vituo vya Afya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna maboma na maabara ambayo tayari tumeona ni jinsi gani tunaweza kukabiliana nazo. Tunazo Shule za Sekondari 13 ambapo zote zina maboma ya maabara. Maboma haya tukipata fedha na maabara hizi zikikamilika, tutakuwa na shule ambazo zimekuwa na ukamilifu na wanafunzi watasoma kwa ufaulu mzuri. Kwa sababu Jimbo langu lina Kata 19, ukichukua na jirani yangu Kafumu mwenye Kata 16 ni jumla ya Kata 35. Kwa hiyo, ukitupa uwiano sawa, hapo utakuwa hututende haki. Nakuomba uangalie Majimbo makubwa yenye shule nydingi, utupe fedha za maboma ili tuhakikishe kwamba tunakamilisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kabla sijaacha kuchangia, nizungumzie *TARURA*. Mheshimiwa Waziri, *TARURA* iongezewe fedha. Kwa Mkoa wa Tabora, mkoa mkubwa kuliko mikoa yote Tanzania yenye ukubwa wa *square meter*

75,000 ikifuatiwa na Morogoro *square meter* za mraba 70,000; Mkoa mzima una *square meter* za urefu wa barabara zile kilometra 8,400, tunapata kilomita 900 za kutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Igunga peke yake tuna kilomita 1,404, tunazotengeneza ni kilomita 40. Mheshimiwa Waziri tuongezee fedha, mkoa wetu ni mkubwa. Mkoa wa Tabora inawezekana ikawa ni mikoa mingine mitatu; mkoa wa Tabora ukubwa wake unaichukua Rwanda, Burundi, Zanzibar, Comoro na visiwa vingine, bado mkoa na chenji zinabaki.

Kwa hiyo, Mkoa huu wa Tabora bajeti yake ya barabara Mheshimiwa Waziri unatakiwa uipe upendeleo wa kipekee. Usilinganishe na mikoa mingine; ni mkoa ambao unatakiwa ugawanywe zaidi ya mara tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maombi kwamba mkoa upatikane wa Manonga; tunatambua mezani kwako hayo maombi yapo. Kuna mkoa mwingine kule wa Urambo. Kwa hiyo, hayo yote, kama ni kuugawa huu mkoa, unaugawa mara tatu, lakini katika mgawanyo wa fedha mnazotoa za Halmashauri za mkoa huwa mnazitoa katika /eve/moja, lakini Mkoa wa Tabora mnatakiwa muupe kwa upendeleo wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho nililotaka kuzungumzia ni suala zima la mapato yanayokusanywa. Siyo kwamba mapato yameenda Serikali Kuu kwamba hatupati, haiwezekani. Halmashauri ya Igunga mfano tunakusanya shillingi billioni 2.2 kwa mwaka; ni makusanyo mengi, lakini pia ukiangalia fedha zinazokwenda kwenye miradi ya maendeleo, tunasema ni asilimia 40. Tunatenga fedha asilimia 40. Asilimia 40 hizo unaonyeshwa kwenye makaratasi, tumefanya hivi, tumefanya hivi! Ukienda kwenye uhalisia, huoni. Kama ni shule imejengwa, tunaishukuru Serikali, fedha zinazotoka kwenu tunaziona, zinajenga madarasa, zinajenga mabweni, lakini za Halmashauri hazionekani. Inawezekana nisiseme mimi, au nikisema, hata Halmashauri nyininge ni hivyo hivyo.

Naomba mwangalie kwa jicho la ukaribu. *Monitoring* ya hizi Halmashauri, miradi inayotekelawa na *level* ya Halmashauri ni tatizo. Siyokwamba hakuna fedha, fedha zipo. Ndiyo maana wakati mwingine Mheshimiwa Rais alifika pale Igunga akawa anatukana, anafofa, analalamika, ni kwa sababu ya nini? *Monitoring* ya hizi Halmashauri, fedha wanazokusanya wao wanafanya nini? Nani anawasimamia kwa ukaribu kuona kama ni kweli shule wamepeleka fedha? Madiwani leo hii utawaona tu migogoro yao ni posho na nini, lakini mwisho wa siku hawawezi kuangalia miradi mizima ya Halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri nitazame kwa ukaribu sana hasa katika fedha ambazo zinakusanywa, achilia mbali za nje, zile tunazozikusanya. Zile ambazo zina...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja ya shilingi trilioni saba *point something* ya Wizara hii ya TAMISEMI. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wenu. Tunawashukuru kwa michango ambayo naamini Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri yuko hapa na Manaibu Waziri wote watayachukua mawazo yenu mazuri na kuyafanya kazi kadri wanavyoendelea kupokea michango yenu.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumanne saa 8.00 mchana.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)